

19 JUNI, 2013

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 19 Juni, 2013

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

#### D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

#### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Ifuatayo Iliwasilishwa Mezani na:-

#### NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Chuo Kikuu cha Ardhi kwa Mwaka 2011/2012 (*Ardhi University Annual Report and Audited Financial Statements for the Financial Year 2011/2012*).

#### MASWALI NA MAJIBU

Na. 421

**Haki ya Kupiga Kura**

**MHE. YUSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa haki mwananchi kuchagua au kutochaguliwa katika madaraka ya Ubunge au Urais:-

Je, ni Sheria ipi inawanyima haki wananchi wa

Tanzania Visiwani kwenye Majimbo yao kupewa haki ya kura moja tu ya kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumnyima haki ya kumchagua Mbunge kwa kura za Muungano?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yusuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 21 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kila Raia anayo haki ya kuchagua ama kuchaguliwa katika madaraka ya Ubunge au Urais.

Mheshimiwa Spika, aidha, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 (12) (a), inaanisha utaratibu wa uandikishaji wa wapiga kura Tanzania Zanzibar. Kifungu hiki kinafafanua wazi kuhusu wanaostahili kuandikishwa na kushiriki katika kupiga kura za kumchagua Rais au Wabunge kwa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi huwaandikisha wale tu ambao hawakuandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Zanzibar, hivyo kuwa na haki ya kumpigia kura Rais wa Jamhuri ya Muungano na sio kwa Wawakilishi katika Bunge la Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo, Kisheria ni wazi kwamba, kuna baadhi ya Watanzania waishio Zanzibar wanapoteza haki ya msingi ya kuwachagua Wabunge wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Serikali kwamba, kasoro hii ya Kisheria pamoja na nyinginezo zitarekebishwa katika mchakato unaoendelea wa kuandika Katiba Mpya

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, namwomba Mheshimiwa Mbunge na wengineo wavute subira hadi zoezi hili muhimu kwenu, litakapokwuwa limekamilika.

**MHE. YUSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Sheria hii ipo kwa Tanzania nzima, lakini ilionesa kuwabagua watu waliopo Unguja, Pemba wamechagua Mbunge na Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa sababu zihi za msingi, nataka kujua?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, swali hili nimeshawahi kulijibu hapa. Tatizo ni Sheria ya Zanzibar na sifa za Mpiga Kura wa Zanzibar ndizo zinazotatiza kwa sababu, mtu anayeandikishwa kule lazima awe ameshaishi kwa kipindi fulani. Pia sifa za mtu anayestahili kupiga kura kwa Zanzibar yenyewe zilizoainishwa na Sheria ya Zanzibar, zimetajwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, inasimamia jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na mkanganyiko huo ndio nilisema na nasema tena kwamba, inakuwa vigumu sana kwa Tume ya Uchaguzi ya Bara kusimamia jambo hili kwa sababu, yule Mzanzibari anayeishi Zanzibar, anaishi kwa Sheria ya Zanzibar, ndio maana hili jambo limetokea, lakini na sisi tumeliona.

Mheshimiwa Spika, ni gumu kulifanya, kwa sababu yako mengi ya namna hii ambayo tunafikiri utaratibu huu wa Katiba mpya unaweza ukarekebisha, ili angalau tuwe tuna uelewa mmoja na utaratibu mmoja ambao tunaweza kuutumia.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata kwa sababu sikumwona mtu mwingine. Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, kwa niaba yake Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed!

Na. 422

**Biharamulo Kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. DKT.  
ANTONY G. MBASSA)** aliliza:-

Je, ni lini mchakato wa kutangaza Mamlaka ya Mji Mdogo wa Biharamulo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA  
MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Anthony Gervas Mbassa, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tangazo lake Namba 355 la tarehe 17 Septemba, 2004, chini ya Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982, ilitangaza nia ya kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Biharamulo. Aidha, katika kipindi hicho hicho Serikali, ilitangaza kuigawa Wilaya ya Biharamulo ili kuanzisha Wilaya ya Chato, ambapo mwaka 2005 mchakato wa kuigawa Wilaya hiyo ulikamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa 2007, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilianza kutekeleza azma ya kuunda Mamlaka ya Mji Mdogo wa Biharamulo, kwa kuanza kupima eneo la kiutawala la Mamlaka hiyo. Mchakato huo ulihusisha upanuzi wa eneo la kiutawala kwa kuanzisha Kata mpya mbili, ili kuafanya idadi ya Kata kuwa tano. Mchakato huu wa kuanzisha Kata ulikamilika mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Vikao vya kujadili uanzishwaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Biharamulo, vilianza mwaka 2010 na tayari *agenda* hiyo imejadiliwa na kuridhiwa na Vikao vyote vya Kisheria vya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo. Aidha, Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*), ambacho kimepangwa kukutana mwezi Novemba, 2013,

kitajadili *agenda* hiyo na mapendekezo ya Kikao hicho yatawasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, washirikiane na uongozi wa Mkoa wa Kagera ili kuharakisha mchakato wa uanzishaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Biharamulo.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, nchi yetu imeongezeka katika maeneo makubwa ya kiutawala na mgawo wa Kata na Halmashauri umeongezeka. Kwa hiyo, moja kwa moja ni kwamba, hata mgawanyo wa rasilimali fedha ambazo zinapelekwa katika Halmashauri zetu, sasa inabidi uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali, kupitia Wizara husika, itatoa mwongozo maalum wa Idadi za Kata katika kila Halmashauri ili hizi Halmashauri ziwe na uwiano katika idadi hizi za Kata na ziweze kupata mgawo wake kisawasawa?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, mchakato wa kupata Kata au Halmashauri unakuwa ni mrefu sana kupitia Serikalini. Je, Serikali, haioni kwamba, sasa iko haja ya kuanzisha mchakato mwengine mpya ambao utarahisisha maombi yanayotoka katika Halmashauri yakafanyiwa kazi haraka?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, yako mambo mawili ameyasema hapa, kama nitakuwa nimejichanganya, basi nitaelimishwa. La kwanza, hili la rasilimali kwa maana ya fedha zinazokwenda na vigezo vinavyotumika. Hata ukichukua ule Mfuko unaoitwa *Constituency Development Catalyst Fund*

umesema kwamba, cha kwanza, unaangalia idadi ya watu, 25% inakwenda kule, unasema wote tunapigwa *flat*, aliyetoka Urambo, aliyetoka Siha, aliyetoka wapi, popote ulipotoka atakupiga hiyo 25%.

Pili, atakwenda ataangalia kiwango cha umaskini na tatu kuna mambo mengi ambayo anayaangalia kule, miundombinu na vitu vingine vy a namna hiyo. Hiyo nina hakika na ye ye mwenyewe ndio maana nimemtaja kwa nafasi yake kama Mwenyekiti wa *Local Authorities Accounts Committee*.

Mheshimiwa Spika, *formula* hii na wenyewe watu wa fedha wako hapa wanafahamu, ni *formula* ambayo ina-*apply* kote mpaka kule kwako Njombe, ndio hiyo hiyo tunayoitumia.

Mheshimiwa Spika, sasa la pili anakwenda kwenye suala la Kata kwamba, zinakuwa ngapi na vitu vingine vy a namna hiyo. Hizi Kata tunazozzungumza hapa, ukiangalia tunakozungumzia, kule Chato, wakati walipogawana pale, wale waliobaki kule Biharamulo, walipotaka kuunda Mamlaka ya Mji Mdogo pale walihitaji uwe na Kata tano. Nina hakika hata akisimama Moses Machali, atauliza hilo swali hapa kwamba, ni kwa nini sasa ile Mamlaka yake haijafikia hatua hiyo?

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa kifupi kwamba, hawa jamaa wanaozungumza hapa, wanaoelezwa hapa wa Mamlaka hii ya Mji Mdogo wa Biharamulo, wamefika laki moja na moja. Wao wanatakiwa wawe na watu 10,000 tu, yaani hawa wameshavuka kile kwango.

Mheshimiwa Spika, ndio maana nimewambia hivi, kilichobakia hapa, ingekuwa kama *Regional Consultative Committee*, ingekuwa haijakaa kwa sababu, zinakaa mara mbili tu kwa mwaka na watacaa tena mwezi Novemba. Hili jambo analozungumza Mheshimiwa Rajab, litakuwa *taken*

*into account* na namwomba radhi kama kuna mahali ambapo nimejichanganya, basi tunaweza kukutana tukakaa vizuri, ili tuweze kuzungumzia hilo.

Mheshimiwa Spika, hili analozungumza la pili la kwamba, huu mlolongo ni mrefu; huwezi ukaenda Kasulu pale au ukaenda Siha, ukagawanya eneo la watu bila kuwahusisha wenyewe wanaohusika. Kwa dhana ya *D by D* huwezi, huwezi kuvunja Kijiji hapa mpaka Mkutano Mkuu wa Kijiji ukutane, useme tuko tayari kuvunja Kijiji hiki kiwe Vijiji viwili. Nenda kasome Ibara ya 145 ya Katiba ya Nchi, nenda kasome na Ibara ya 146 ya Katiba ya Nchi, inatambua Mamlaka hizi ninazozisema hapa. Nenda kasome Sheria Namba Saba na Sheria Namba Nane, Cap 207 na 208 ambazo zinatambua kuwepo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maana ya *D by D*.

Mheshimiwa Spika, huwezi ukauacha utaratibu huu ukagawa nchi hapa baada ya hapo, kama ni Wilaya utakwenda kwa Rais wa Nchi, kama ni Kata utakwenda kwa Waziri Mkuu; hizi nydingine huku chini zote zinapitia hapa, zinaishia hapo, ndio utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama Mheshimiwa Rajabu anafikiri kwamba, kuna namna nydingine nzuri ya kuondoa huu urasimu nilioueleza hapa, basi, tunaweza tukakaa tukajadili, tutamshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ndiye mwenye dhamana ya kugawa na Mheshimiwa Rais, anayegawa Tarafa, Wilaya pamoja na Mikoa katika nchi kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali hebu uliza swali tukusikie.  
(*Kicheko*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nimuulize swali moja dogo. Eneo linaloitwa Halmashauri ya Mji wa Kasulu, halitakiwi kumegwa lipelekwe eneo lingine kimipaka, ni hilo ambalo linaunda Jimbo la Kasulu Mjini, ambalo lina Kata zipatazo nane.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mujibu wa taarifa ya Serikali, imeonesha kwamba, Halmashauri ya Mji wa Kasulu, haiwezi ikaanza sasa mpaka baada ya uchaguzi wa mwaka 2015, lakini ukienda, llemela imeanza ina Kata tisa. Siha anakotoka Mheshimiwa Waziri Halmashauri ile ilianza ikiwa na Kata tano.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata sababu za Serikali, ambazo zimesababisha kwamba, sasa Halmashauri ya Mji wa Kasulu, isianze? Kwa sababu, kama maeneo mengine yameanza yakiwa na Kata chache na hii Halmashauri ya Mji wa Kasulu, nayo ina Kata ambazo zinafanana na nyingine kuzidi hata baadhi ya ambazo zilianza.

Mheshimiwa Spika, ni nini Kauli ya Serikali? Kwa nini isiflikirie upya uamuzi wake, Halmashauri hii ya Mji wa Kasulu ikaanza sasa?

**SPIKA:** Haya, ndio hilo swali ulikuwa unalijua? Naomba sasa ujibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kila mtu anafahamu kabisa kwamba, tulijua hizi Mamlaka zote zingekuwa Mamlaka za Miji, ikiwemo Mamlaka ya Mji wa Kasulu. Ndivyo tulivyoelewa kwa Nzega, ndivyo tulivyoelewa kwa Masasi na kwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, zile Kata za kwake ambazo zinatamkwa kule wakati zinatamkwa hizo Kata, zilikuwa hazijaingizwa sasa katika hiyo Mamlaka Mpya ambayo tunaizungumzia. Ziko pale na anafahamu kwamba, ziko pale zinatamkwa, lakini zilikuwa hazijaingia; kuingiza Kata mle ndani maana yake ni kwamba, una Kata, una Diwani wake, una *Ward Development Committee* na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, tumezungumza na Mheshimiwa Machali sana, hivi anavyozungumza hapa ni kwamba, anataka na wananchi wa kwake kule Kasulu wajue kwamba,

Mbunge anafuatilia jambo hili. Nampongeza sana kwa jambo hilo. Ukitesema sasa tunakwenda kuzivunja zile Kata pale, tuziondoe, ujue *implications* zake ni kwenda kuunda tena hii Mamlaka na kwenda kuitisha Uchaguzi mwingine mpya ambao utaku-affect hata wewe mwenyewe, kama uko tayari. Lakini nasema hivi wame-*qualify* na kila kitu kimemalizika, wala hakuna tatizo lolote. Nataka niseme tu ni suala la kuvuta subira.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna kitu amekisema hapa na Mheshimiwa Spika wa zamani anafahamu jambo hili, Mheshimiwa Sitta. Anasema unajua bwana hata Siha ilipoanza pale, kwanza nataka nisahihishe hapo, Kata zilizoko pale sio nne, ni Kata 12 zilizoko pale na Madiwani walioko pale ni 17. Najua humu ndani akifanya hiso hesabu ataziona pale, lakini yale yote yalikuwa *determined* kabla ya kuanzisha hiso Mamlaka, ambacho ndicho kina-*miss* katika Mamlaka ile anayoizungumzia ya Kasulu.

**SPIKA:** Jamani mmeshapata *lecture* ya Kata, sasa twende Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Mheshimiwa David Silinde atauliza hilo swalii, kwa niaba yake Mheshimiwa Felix Mkosamali *Agent. (Kicheko)*

Na. 423

### **Viwango vya Michango ya Hiari**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE)** aliuliza:-

Michango ya Sekondari Majimboni ni hiari kwa wananchi kuchangia ili kuendeleza elimu katika maeneo yao:-

(a) Je, ni nani mwenye jukumu la kupanga kiwango cha michango hiyo?

(b) Je, ni hatua zippi atachukuliwa mwananchi endapo atashindwa?

(c) Je, viwango vya michango ya hiari vinafanana kwa nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Waraka wa Elimu, Namba Nane (8) wa Mwaka 2011, Serikali inaelekeza jukumu la kuchangia maendeleo ya elimu kwa wanajamii wote, chini ya utaratibu au uratibu na udhibiti wa Kamati ya Shule kwa Shule za Msingi na Bodi za Shule kwa Shule za Sekondari na pia Bodi za Vyuo kwa Vyuo vya Ualimu, baada ya kupata kipata Kibali cha Kuchangisha Michango hiyo kutoka katika Halmashauri husika.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Uongozi wa Shule, Bodi ya Shule ya Sekondari na Wanajamii ndio wanaohusika kupanga viwango vya michango na kuomba Kibali cha Kuchangisha kutoka katika Halmashauri zao, hao hao ndio wanaoweza kuamua kwa pamoja hatua za kuchukua dhidi ya wananchi wanaoshindwa kuchangia michango hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, michango ya hiyari ya kuendeleza elimu katika shule inategemea mahitaji ya shule, kibali cha kuchangisha na uwezo wa wachangiaji katika Halmashauri husika, hivyo viwango vya michango havifanani kati ya shule moja na nyingine. Kwa mantiki hii, viwango vya michango ya hiyari kwa wananchi kuchangia ili kuendeleza elimu katika maeneo yao, havifanani kwa nchi nzima.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa, Wizara ndio iliyotoa Mwongozo wa uchangishaji na sasa hivi kuna

watu wanaweka michango kiholela, ovyo ovyo, kwa nini Wizara isilingilie kati ikaweka vigezo vya kuanzisha hii michango? Kwa sababu, kuna watu wanaanzisha Bodi, zinakaa miaka 20 mpaka 30, hazibadilishwi kwa sababu ya maslahi ya hawa Wakuu wa Shule, kwa nini Serikali, isilingilie kati suala hili?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, elimu ni moja ya vigezo vya haki za binadamu. Sasa watoto wanaposhindwa kulipa ada, wamekuwa wanafukuzwa shulenii muda wa masomo. Serikali, inasemaje kuhusu kuwafukuza watoto muda wa shule wakati wao hawana uwezo wa kutafuta ada hizo?

#### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Mkosamali hapa siyo kweli, Serikali tayari ina Waraka. Kama nilivyo sema kwenye jibu langu la msingi, upo Waraka wa Elimu namba (8) wa mwaka 2011 wa kukithiri kwa michango mashuleni na huo Waraka ni huu hapa, kama Mheshimiwa Mkosamali hana ningeomba nimtolee *photocopy* nimpe.

Mheshimiwa Spika, lakini hayo mambo mengine yanayofanyika mashuleni, ni namna tu ya Wakuu wa Shule wanavyotelekeza Waraka huu na Waheshimiwa Wabunge mnapofanya ziara kwenye shule mnaweza mkathibisha hayo. Lakini sisi kama Mawaziri au watu wa Wizara ya Elimu tunapita kwenye mashule tunaendelea kuwaambia wananchi na kuwaelimisha juu ya michango mashuleni.

Mheshimiwa Spika, lakini ipo vile vile michango ambayo ilikatazwa na hapa lazima niiseme; michango ya kuandikisha wanafunzi darasa la kwanza ama kidato cha kwanza haipo, barua za utambulisho wa wanafunzi wanaofaulu darasa la saba kwenda Sekondari, barua zote za wanafunzi kuitwa kuijunga na shule za Sekondari au Vyuo na fomu za kuijunga na kidato cha kwanza katika shule zisizo za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kwa pamoja, kwa

sababu hili suala ni kubwa na Waheshimiwa Wabunge wote mtakapokuwa mnakwenda huko, tupeane tu taarifa, ukinipigia simu hatu mimi kwa shule husika, huwa nakuja mara moja na naweza kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu Bodi za Shule kwamba, labda zinakaa muda mrefu, upo utaratibu na Waraka kwamba, miaka mitatu mitatu Bodi ile ina-expire inachaguliwa Bodi nyingine. Sasa baadhi ya wajumbe wanakuwa ni wajumbe ambao kidogo wanaweza wakaisaidia shule, kwa hiyo unakuta Mwalimu Mkuu au jamii inamrudisha mtu kwa wakati mwininge au mara tatu, lakini kikomo angalau ni mara tatu, lakini mara ya pili anaruhusisha kuwa mjambe wa Bodi tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna lile swali moja lile la watoto wanaofukuzwa shule.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, watoto wanaofukuzwa kwa sababu ya michango, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, Halmashauri husika katika Wilaya husika yenye we ama Kata ama shule na jamii kwa ujumla, ndiyo wanaojua pale kwamba huyu mtoto anayefukuzwa hana michango kabisa aidha, ni yatima au ana uwezo, lakini tulishapiga marufuku kwamba, watoto wasifukuzwe shule kwa sababu ya michango, kwa sababu michango inabidi Kamati ya Wazazi ikae ili Mwenyekiti wa Shule au Mwenyekiti wa Bodi awatangazie wazazi michango hii na jinsi inavyoweza kutolewa utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa nyongeza ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ameelezea michango inayohusiana na kibali kinachotolewa na Wizara ya Elimu. Lakini katika maeneo yetu kuna michango ya ujenzi wa miundombinu ya elimu ambayo huwa inapitishwa na vikao mbalimbali vyta Serikali za Vijiji au *Ward C*; michango ile ikishapitishwa na *Ward C* inakuwa ni jukumu la wazazi kuchangia kwa mujibu wa makubaliano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, michango hii anayozungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri ni michango ile ambayo inahusisha vitendea kazi katika shule, lakini michango ya maendeleo kwa ajili ya miundombinu ya elimu, inapopitishwa na vikao halali inakuwa ni lazima kila mwananchi mwenye uwezo wa kuchangia achangie kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, vile vile Halmashauri fulani fulani huwa zinatunga *bylaws* zao (Sheria ndogo) kwa ajili ya michango. Sasa zikiwa na *by laws* hizo ni lazima kuchangia. Nilitaka niweke sawa haya mambo mawili yaeleweke ili isionekane kwamba kuna michango haramu na michango isiyo halali. Michango hii mingine ya maendeleo ambayo imepitia utaratibu wa vikao hivi, ni halali.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, imebainika kwamba, kuna baadhi ya viongozi wa kisiasa wakiwemo Wabunge mfano, Mbunge wa Singida Mashariki, amehamasisha wananchi wake wakatae kuchangia michango yote ya maendeleo katika Jimbo lake. Kuliachia jambo hili kuendelea ni kuwashawishi na Majimbo mengine waige mfano huo mbaya. Je, Serikali inatoa kauli gani kukemea vitendo kama hivi ambavyo vinadumaza maendeleo ya nchi yetu? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa haji hapa ni kweli kabisa, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hata Mheshimiwa David Silinde na yeye huko Mbozi, hata angekuwepo hapa ningemwambia hilo na yeye alishawahidi kupiga marufuku wananchi wake wa Tunduma pale wakawa hawakuchangia michango.

Mheshimiwa Makamu wa Rais alipofanya ziara mwaka juzi ililetu matatizo kidogo hata kwenye mkutano wa hadhara. Lakini tulikwenda tukafanya ziara pale, tukawaelimisha wananchi wa Tunduma na wakachangia. Sasa hivi angalau wamejenga hata madarasa sita kwa Sekondari na wototo wao wamekuwa *enrolled* pale.

Mheshimiwa Spika, hili la Mheshimiwa Mbunge wa Singida na Wabunge wengine ambao kwa kweli wanahamasisha wananchi wasitoe michango, Serikali inalilaani kabisa, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukuvi ipo michango ambayo ni halali kabisa *RCCama Ward Cama DCC*, wanakaa kwenye vikao vyao halali, wanapitisha kwamba michango hii itakuwa ni halali.

Mheshimiwa Spika, michango hiyo ni kama ulinzi wa shule kwa mfano, kujenga uzio au vyoo, ziara za kimasomo, chakula cha mchana cha wanafunzi, kulipia ankara za maji au umeme na mitihani ya masomo kama *mock* na kadhalika kwa *form two* na *form four* miundombinu kama alivyosema Mheshimiwa Lukuvi, ni michango halali, vikao vinakuwa vimekaa vya kisheria ngazi ya Kata, ngazi za Wilaya hata ngazi ya Mkoa wanapitisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaokataza wananchi michango, suala hili kwa kweli kama Serikali hatuwezi kulinyamazia, lazima tuhamasishane na Waheshimiwa Wabunge wote mnanisikia humu kwamba, tuendelee kuwaelimisha wananchi juu ya michango hii. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsanteni. Naomba tuendelee limekuwa na mchango mkubwa hili swalii, sasa twende Wizara ya Ujenzi Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa niaba yake Mheshimiwa Mwenyekiti mwengine wa Chama cha *NCCR Mageuzi, Engineer Mbatia*.

Na. 424

### Barabara za Lami Wilayani Hai

**MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE)** aliuliza:-

Mbali na barabara kuu itokayo Dar es Salaam

kwenda Nairobi kupitia Moshi na Arusha ambayo hukatiza Jimboni Hai:-

(a) Je, ni barabara ngapi za urefu gani zimejengwa kwa kiwango cha lami katika Jimbo la Hai kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita?

(b) Je, ni vigezo gani vyta kiuchumi, kitaalam, kimazingira na kisiasa hutumika kuchagua Wilaya zinazojengewa barabara kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia kilomita 35,000 ambazo ni barabara kuu na za Mikoa na madaraja 4,880 katika nchi nzima. Kwa mantiki hiyo, Wizara yangu haihusiki na barabara za Majimbo au barabara za Wilaya (*District Roads*). Aidha, ukiacha barabara kuu itokayo Dar es Salaam kwenda Nairobi, Jimbo la Hai lina barabara za Mkoa zenye jumla ya kilomita 40, zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ambazo ni Kwasadala – Kware – Lemira, kilomita 15; Kilimanjaro *Machine Tools* – Machame, kilomita 15; Bomang’ombe – Sanya Juu, kilomita 10.

Mheshimiwa Spika, kati ya ya hizo barabara zenye urefu wa kilomita 25 ni za lamo ambazo ni Kilimanjaro *Machine Tools* – Machame na Bomang’ombe kwenda Sanya Juu. Aidha, barabara ya Wilaya ya Kwasadala – Masama kilomita 12.5, inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2010. Hadi sasa jumla ya kilomita saba zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, vigezo zinavyotumika katika

kuchagua barabara za kujengwa kwa kiwango cha lami ni pamoja na uwepo wa fedha, idadi ya magari yanayotumia barabara kwa siku, uwepo wa huduma za jamii kama vile hospitali kubwa, umuhimu katika kuunganisha eneo husika na maeneo mengine na idadi ya watu pamoja na shughuli na fursa za uzalishaji zilizopo pamoja na Sheria Na. 13 ya mwaka 2007. Aidha, lengo ni kuendeleza barabara kuu na za Mikoa yote, hatua kwa hatua jinsi uwezo unavyoruhusu.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa barabara alizouliza Mheshimiwa Mbewe inayotoka Moshi Mjini kwenda Arusha ijulikanayo kama *The Great North Road* toka Cairo, Misri mpaka *Cape Town* Afrika ya Kusini ni barabara ya tangu wakati wa Mkoloni na barabara ya Kilimanjaro *Machine Tools* – Machame Kilomita 15 imejengwa mwaka 1952. Je, Serikali imewekeza kwa kiasi gani kwa kuwa barabara hizi nyingine ziko mlimani, kuhakikisha mifereji ya kuondoa maji barabarani na kufanya *routine maintenance* kwenye barabara hizi za kihistoria katika nchi yetu? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara hizi zinatumika na magari makubwa ambayo *axle load* yake inaharibu barabara na kuitisha mizigo mikubwa. Je, Serikali imejipanga namna gani kuwekeza zaidi kwenye reli ya kwenda Kaskazini, reli ya katilili mizigo mikubwa ipitishwe kwenye njia ya reli badala ya kuzunguka kwenye barabara hizi ambazo zinagharimu Taifa hili fedha nyingi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikupongeze Mbatia kwa swali zuri na kuwakumbusha Watanzania kwamba, mipango ambayo tunayo sasa hivi tumeweka Mfuko wa Barabara, kazi yake kubwa ni kufanya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiyo *routine maintenance* anayozungumzia Mheshimiwa Mbatia ndiyo kazi ya ile fedha, kwa hiyo fedha za Mfuko wa Barabara

zitahakikisha barabara hizi ambazo tumezitengeneza kwa kiwango cha lami zinaendelea kuwa katika hali nzuri, kwa hiyo, tutazitengeneza mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, suala la *axle load*, kwa maana ya *standard* ya barabara ili ziweze kudumu kwa muda mrefu, ushauri wake kwamba, tuwekeze zaidi kwenye reli ni ushauri mzuri na tumeuchukua. Sasa hivi ndiyo tumeamua kwamba, tuanze kwanza kuimarisha reli ya kat, iweze kuchukua mizigo mingi zaidi kuliko hii mizigo yote kwenda kwenye barabara hii ya kat.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili barabara hizi ziweze kudumu, lazima tuwekeze zaidi kwenye reli na tutachukua pia upande wa Kaskazini kutoka Tanga kwenda Moshi ili mizigo iweze kusafirishwa kwa reli. Kwa hiyo, Serikali itawekeza zaidi kwenye reli kusudi barabara zetu ziweze kudumu.

**SPIKA:** Ahsante. Sikumwona mtu mwingine, hamwezi kusimama baada, mnatakiwa msimame kabla muonekane, halafu niwaite. Tunaendelea, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana swali linalofuata, kwa niaba yake Mheshimiwa Kapteni Komba.

Na. 425

### Kivuko Katika Mto Ruhuhu

**MHE. JOHN D. KOMBA (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA)**  
aliuliza:-

Kivuko cha Mto Ruhuhu kimeondolewa injini na mamlaka husika, hivyo kivuko kutokekanya kazi:-

(a) Je, ni lini injini hiyo itarudishwa ili kivuko kianze tena kufanya kazi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja kwenye Mto Ruhuhu?

## **NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali namba 90 lilitoulizwa na Mheshimiwa *Captain* John Komba tarehe 8 Februari, 2012, injini ya kivuko cha Mto Ruhuhu iliyokuwa imeazimwa kwenda kufungwa kwenye Kivuko cha Kilombero ilirudishwa na kufungwa kwenye kivuko cha Mto Ruhuhu tarehe 9 Januari, 2012. Injini hiyo ilihamishiwa katika Kivuko cha Kilombero kwa muda kutokana na dharura ya kuharibika kwa injini ya Kivuko cha Kilombero.

Mheshimiwa Spika, aidha injini ya Kivuko cha Ruhuhu iliazimwa wakati kivuko hicho hakifanyi kazi kwa kuwa Kivuko cha Ruhuhu hakifanyi kazi wakati maji yamepungua au maji yamejaa sana. Kwa sababu hii Kivuko hiki hufanya kazi kwa miezi mitatu au minne tu kwa mwaka kati ya mwezi Aprili na Agosti.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kujenga daraja litakalojumuisha bwawa (*Bridge Cam Dam*) kama mradi mmoja katika Mto Ruhuhu ili pamoja na kutumika kama daraja, bwawa litumike kwa shughuli za umwagiliaji katika bonde la Mto Ruhuhu eneo la Lituhi upande wa Mkoa wa Ruvuma na Kipingu kwa upande wa Mkoa wa Njombe.

Serikali inaendelea na maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga daraja bwawa la kumwagilia na tayari hadidu za rejea kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa kufanya usanifu zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utahusisha Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

**MHE. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Upembuzi yakinifu, usanifu ni maneno ambayo yamesikika mara nyingi sana tangu miaka mitano iliyopita katika jambo hili la kuweka daraja katika mto huo. Je, hii lugha itakwisha lini?

Mheshimiwa Spika, namba mbili, hivi kweli Serikali ina huruma na watu wale walioko eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba Mheshimiwa Komba asikate tamaa na maneno ninayosema ya upembuzi yakinifu. Daraja lile ili liweze kudumu kwa muda unaotarajiwa ni vizuri tukafanya kazi hii kwa mpangilio unaotakiwa.

Tufanye usanifu wa kina, halafu tuweze kuitisha kandarasi tuweze kujenga daraja lile na tayari hata Rais ameshasisitiza kwamba, tuanze upembuzi yakinifu haraka iwezekanavyo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kazi hiyo itafanyika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huruma ya Serikali, kwa kweli ipo, kwanza kile kivuko kilikuwa kinachukua tani saba, Serikali ikabidi inunue kivuko kingine kinachochukua mpaka tani 50. Tatizo lililoko pale ni maji. Maji yakipungua kile kivuko hakiwezi kufanya kazi na maji yakizidi pia kile kivuko kwa sababu ni kikubwa hakiwezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa huruma ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayo, ndiyo maana tumeona tugharamie kujenga daraja ambalo litafanya kazi zote, kuitisha magari pamoja na umwagiliaji. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Komba pamoja na wananchi wa kule Mbinga watuvumile, Serikali itatatua tatizo hilo.

**SPIKA:** Ahsante. Sikumwona mtu mwengine kabla ya hapo na tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Abdulsalaam Amer, kwa niaba yake atauliza swali hilo Mheshimiwa Nassir.

Na. 426

### **Kupeleka Umeme Katika Vijiji**

**MHE. YUSUPH A. NASSIR (K.n.y. MHE. ABDULSALAAM S. AMER)** aliuliza:-

Je, Serikali itapeleka lini umeme katika Vijiji vya Zoumbe, Lumbe, Kipekenya, Ulaya Mbuyuni, Ulaya Kibaoni, Nakala na Mhenda?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulsalaam Seleman Amer, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Vijiji vya Zoumbe, Lumbe, Kipekenya, Ulaya Mbuyuni, Ulaya Kibaoni, Makala na Mhenda bado havijapatiwa umeme. Hata hivyo, Serikali kuititia Shirika la Umeme inatarajia kufanya tathmini kwenye vijiji hivi katika mwaka wa fedha 2013/2014 ili kuanisha kiasi cha fedha kinachohitajika.

Mheshimiwa Spika, tathmini hii ikikamilika itaiwezesha Serikali kutafuta fedha za utekelezaji kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ukiwemo Mfuko wa Nishati Vijijini kwa ajili ya kuvipeleka umeme vijiji hivyo.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa ratiba iliyotolewa na REA ya mchanganuo wa miradi katika Jimbo hili la Mikumi haikutaja vijiji husika, je, Mheshimiwa Waziri anatuambiaje kuhusiana na utaratibu mzima wa kupata fedha ili miradi ya umeme kwenye vijiji hivi iweze kutimia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge katika swali hili havimo

katika *REA phase II*, lakini awamu hii ya pili ya miradi ya *REA* siyo ndiyo mwisho wa miradi ya *REA*. Sasa hivi tuko katika mchakato wa kuandaa awamu ya tatu, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika awamu ya tatu vijiji hivi vitakuwemo.

Mheshimiwa Spika, aidha, nipende kutambulisha na niwaeleze wananchi wa Jimbo la Mikumi kwamba baadhi ya vijiji ambavyo vimo ni pamoja na Kijiji cha Malolo, Wazaganza na vijiji vingine ambavyo vitapatiwa umeme katika awamu hii.

**MHE. DKT. PUDENSIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mazingira ya Mikumi yanafanana kabisa na mazingira ya Wilaya mpya ya Mlele. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata ya Ilunde, Nsekwa, Mwese, Katuma na Mpanda Ndogo?

**SPIKA:** Aah Mheshimiwa! Haya hebu jaribu kujibu, swali jipya hilo, jibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, katika miradi ya *REA phase II*, Wilaya karibu zote zimepatiwa vijiji vichache vichache. Naomba tuwasiliane baada ya hapa, tuweze kuona hivi alivyovitaja kama vimo katika orodha hii.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Serikali imetekeleza vilivyo ahadi ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete ya kupeleka umeme Mjini Namanyere, lakini njiani kote umeme haujasambaa, umepita na kudondoka nyumba mbili au tatu, lakini sasa wananchi wanaauliza ni lini umeme huu utaenea katika maeneo yote ya vijiji kwa sababu wanauhitaji, wanauona unapita na kudondoka katika nyumba mbili, tatu kuondoka? Naomba majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba

umeme ulipokwenda katika Wilaya ya Namanyere na Nkasi, umepita katika baadhi ya maeneo na baadhi ya maeneo bado. Niseme tu hili litakuwa ni zoezi la kudumu, kwa sababu hata kama tutasema tunapeleka umeme vijijiini, haiwezekani tukapeleka vijiji vyote kwa mara moja, kwa sababu makazi yatakuwa yanaongezeka na watu wanaongezeka, kwa hiyo, ni jambo linaloendelea, siyo kwamba litakoma mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kusambaza umeme kadri tunavyopata fedha, lakini kadri ya maombi ya wananchi, hata Dar es Salaam yenyewe, Dodoma na Mikoa mingine yote, si kweli kwamba wananchi wote katika Mikoa hiyo mijini wana umeme. Kwa hiyo, usambazaji utakwenda kadri ambavyo tunapata fedha na kadri ambavyo wananchi wanahitaji.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa John Chiligati!

Na. 427

### **Utafiti wa Madini ya Urani Manyoni**

**MHE. KAPT. JOHN Z.CHILIGATI** aliuliza:-

Kampuni ya *URANEX* imeanza utafiti wa Madini ya Urani kwenye Vijiji mbalimbali Wilayani Manyoni na kuwapa wananchi hofu kubwa kuhusu zoezi hilo:-

- (a) Je, Serikali itachukua hatua gani kuwaondolea wananchi hofu walijonayo kuhusu usalama wao na hatma ya mashamba yao endapo yatachukuliwa na mwekezaji huyo?
- (b) Je, hadi sasa utafiti huo umeonesha matokeo gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kapteni John Chiligati, Mbunge wa Manyoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sera ya Madini ya mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 zinatumika katika kusimamia shughuli za utafutaji wa Madini ya Urani nchini. Kanuni maalum (*The Mining (Radioactive Minerals) Regulations, 2010*) zimetungwa chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kwa ajili hiyo.

Kanuni na Sheria zote zilizotungwa na zinazoendelea kutungwa zinahusiana na usimamizi wa Madini hayo ya Urani na zinalenga kuzingatia Miongozo, Taratibu za Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomu (*IAEA*) za Usimamizi wa Madini hayo na zinahakikisha kuwa uchimbaji (*exposing of uranium are on the surface*) hauleti madhara au athari kwa watu na mazingira.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Manyoni, wasiwe na hofu yoyote kuhusu utafiti wa Madini ya Urani unaoendelea kufanywa na *URANEX*, kwani kampuni hii inafanya shughuli zake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni nilizoziainisha.

Kampuni hiyo inaendelea na utafiti wa kimaabara wenyе nia ya kutaka kuanza uchimbaji wa Urani katika eneo hilo. Ikiwa *URANEX* itahitaji sehemu ya ardhi ya wananchi, wenyе ardhi katika eneo hilo watahusishwa na watapata fidia stahiki pamoja na kuhamishwa na kujengewa makazi mapya kwa gharama ya kampuni hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa Kampuni ya *URANEX* imegundua takribani Ratili milioni 29 za mashapo ya urani katika eneo la Manyoni. Pamoja na kwamba kiwango hicho cha mashapo kinatosha kuanzisha uchimbaji, Kampuni

hiyo inaendelea kufanya utafiti wa kimaabara na ubora wa kutenganisha urani katika mashapo hayo yenyewe udongo wa mfinyanzi kwa wingi. Mara zoezi hilo lltakapokamiliika na ufanisi wa kampuni hiyo itaanza taratibu za kuanza uchimbaji wa madini hayo.

**MHE. KAPT. JOHN Z.CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa kuna Asasi za Kiraia (*NGOs*) zinapita katika maeneo ya Wilaya ya Manyoni na ya Bahi, zikisambaza upotofu na chuki kwa wananchi dhidi ya shughuli hii ya madini haya. Je, Serikali kwanza inajua harakati za Wanaharakati hao na kama inajua, inatoa tamko gani kukomesha harakati hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba na sisi tunatambua kwamba, kuna harakati mbalimbali za wanaharakati kueleza ama kupotosha wananchi kuhusiana na uchimbaji wa urani, lakini kama nilivyoeleza kwenye swali la msingi kwamba, shughuli hizi za uchimbaji wa urani zinafanywa kwa taratibu zote za Kimataifa zinazosimamia uchimbaji wa urani, chini ya Shirika la Nguvu za Atomi la Dunia.

Wanaharakati hawa wanafanya pia shughuli hizi pengine kwa maslahi fulani kutoka kwa hawa wanaowafadhili kufanya shughuli hizo.

Waheshimiwa Wabunge, ningependa tu niseme kwamba, madini ya urani ni madini ya kimkakati. Kwa hiyo, dunia, Mataifa makubwa pia yanayatazama madini haya kwamba, yanazalishwa wapi, yanakwenda wapi na yanatumikaje. Kwa hiyo, wale walioyapata, ambao hawakuyapata pia hawafurahii kuona yameshikiliwa na makampuni ya nchi ambazo pengine wanasigana kisiasa za kidunia.

Kwa hiyo, shughuli za wanaharakati wetu pia lazima watambue anayepiga ngoma hiyo anamaanisha nini na sisi tusidandie tu kucheza ngoma ambayo mpigaji hatujui anamaanisha nini. Kwa hiyo, niseme tu Serikali tunasimamia na tunazingatia taratibu zote za uchimbaji wa urani.

Mheshimiwa Spika, madini haya yapo kila siku tunaishi nayo na hatujapata taarifa ya kuambiwa kwamba, kuna madhara yametokea katika eneo la Bahi ama Manyoni, ama maeneo ya Mkusu ambako tuna shughuli hizi za urani, lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kusimamia kuhakikisha Sheria hazivunjwi na taratibu zote zinazingatiwa.

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mradi wa urani pia tumebahatika na sisi Wilaya ya Namtumbo tuna mradi wa Mkusu na taratibu za utoaji wa vibali vyta mazingira umeshakamilika, Wizara ya Nishati na Madini mmeshatoa Leseni, lakini sasa hivi mpo katika majadiliano ya Mkataba (*MDAs*). Sasa je, ni lini mtamaliza majadiliano hayo ili mradi huo uweze kuanza na watu wa Namtumbo waweze kuona manufaa ya mradi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, muda umekwenda.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tumekamilisha zoezi la kutoa Leseni na katika eneo la mkataba, kuna maeneo ambayo tulikuwa hatukubaliani nayo kama Serikali kwa maslahi ya nchi hasa kwenye maeneo ya kodi (*withholding tax*) katika *interest na service*, Serikali tumeshatoa msimamo wetu jana na tume shapeleka taarifa hiyo kwa kampuni inayohusika.

Sasa *offer* iko mezani, *either* wanaichukua au wanaiacha, lakini sisi kama Serikali tumeshaweka msimamo wetu na *position* yetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge,

nikuombe tu kwa maslahi ya wananchi wa Namtumbo, kuangalia upande wa pili wa ile kampuni kama ile *position* yetu wataichukua au wataiacha. Ahsante.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Swali langu ni kwamba, wakati wa uhamisho wa umiliki wa mradi huu kutoka kwenye Kampuni *MANTRAS* inasemekana Serikali ilipoteza kiwango kikubwa sana cha kodi, je, hatua gani imefikia kupitia *TRA* kuweza kuzipata fedha hizi?

**SPIKA:** Unadhani umeelewa, sisi hatujaelewa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba *MANTRA Tanzania Limited*, ndiyo iliyouza hisa zake kwa kampuni ya *MANTRA* ya Australia na Kampuni ya *MANTRA* ya Australia iliuza kwa Kampuni ya Kirusi ya *ARMZ* kwa *one billion dollar* na Serikali ilidai kuwa imesitahili kupata malipo ya *capital gain tax*.

Mheshimiwa Spika, sasa kesi ile iko Mahakamani na inasimamiwa na *TRA* na siyo Wizara ya Nishati na Madini kwa sababu ni kesi inayohusiana na mambo ya kodi ambayo kimsingi *TRA* ndiyo yeye *mandate* ya kusimamia.

Kwa hiyo, nisingeweza kutoa *details* kwa sasa kwa sababu shauri hili liko Mahakamani na linaendelea huko kwa mujibu wa taratibu za Sheria za Kodi.

**SPIKA:** Muda umekwenda, twende Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha atauliza swali hilo, kwa niaba yake Afande mwingine Mheshimiwa Ester Bulaya atauliza swali hilo.

**Mgogoro Kati ya Kambi ya Bavuai na  
Wananchi wa Mpendae**

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. MARYAM SALUM  
MSABAHA) aliuliza:-**

Kumekuwepo na mgogoro wasiku nyingi kati ya Kambi ya JKT ya Bavuai, Zanzibar na wakazi wa Mpendae walio maeneo ya Kaburi Kikombe na Migombani kwa wananchi kuchukuliwa maeneo yao na mpaka leo hawajapata ufumbuzi:-

(a) Je, Serikali inawaambiaje wakazi wanaoishi katika maeneo yanayopakana na Kambi ya Jeshi?

(b) Serikali haioni kwamba inaingia kwenye migogoro baina ya Wanajeshi na wananchi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Maryam Msabaha kuwa, katika mwaka huu wa fedha 2013/2014, Jeshi la Wananchi wa Tanzania lina mpango wa kupima mipaka ya Kambi ya Bavuai ambayo ina mgogoro na wananchi wa Mpendae.

Iwapo katika upimaji huo wa mipaka itabainika kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania limechukua maeneo ya wananchi, basi wananchi hao watalipwa fidia stahiki, lakini iwapo itabainika kuwa wananchi nao wamechukua maeneo ya Jeshi, basi wananchi hao watatakiwa kuondoka kwenye maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina sababu

yoyote ya kuwa na mgogoro na wananchi wake inayowahudumia. Kama nilivyosema awali, Wizara yangu ina mpango wa kupima maeneo yote ya Kambi ya Bauuai ili kuweka wazi mipaka ya Kambi hiyo na hatimaye kuepuka migogoro hiyo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya mipaka pia ipo na Tanzania Bara na hasa katika Kata ya Kunduchi, Jimbo la Kawe na najua Serikali ilikuwa inashughulikia suala zima la uwekaji mipaka, nataka kujua, wamefikia wapi ili kutatua mgogoro wa Kata ya Kunduchi.

Mheshimiwa Spika, swalilangu la pili, kwenye Kambi nyangi za Jeshi, zimekuwa zikiongozwa na akinababa, lakini wapo akinamama wanajeshi ambao wanavyeo ambavyo vinafa na wenyewe kuongoza kwenye Kambi hizo. Sasa je, Mheshimiwa Waziri huoni kwamba kuna haja sasa kwenye hivi Vikosi vingine vya Jeshi, akinamama wapate nafasi ya kuongoza?

**SPIKA:** Ili wapime mipaka. Ni swalijipya kabisa, lakini naomba ujibu tu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna maeneo mbalimbali yenye migogoro na kama nilivyosema wakati nilipokuwa nikiwasilisha bajeti ya Wizara yangu, kuna migogoro kama 80 hivi ukiwemo mgogoro wa Kunduchi, lakini kwa taarifa niliyo nayo na bahati nzuri nimezungumza na Mheshimiwa Mbunge wa Kawe, suala hili limefikia katika hatua nzuri sana ya utekelezaji. Tunayo ahadi mimi na yeye baada ya kumaliza Bunge hili Tukufu tupate nafasi sasa ya kwenda kuangalia utekelezaji wa upimaji wa mipaka hiyo katika Kambi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la akinamama, najua kwamba wapo akinamama, wana nafasi nzuri tu ya uongozi

katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Bahati mbaya sana, tunapotafuta kiongozi katika Jeshi, tunatafuta Mwanajeshi ama mwanamke au mwanamume kwa kuzingatia sifa.

Mheshimiwa Spika, sasa pale tutakapoona kwamba mwanamama anazo sifa zinazostahiki hatutakuwa na hiyana hata kidogo ya kumpa nafasi hiyo anayostahiki. Kama mwana baba anazo sifa ya kushika nafasi fulani na yeze hatutamfanya hiyana kwa sababu ati ni mwanamme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumekuwa tukiendelea kutenda haki kwa kadri hali inavyoruhusu. Namhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutekeleza na kuhakikisha kwamba tunawatendea haki wanaume na wanawake katika utumishi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Nini ufumbuzi wa kudumu wa migogoro ya ardhi kati ya JWTZ na wananchi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inachukua hatua tatu ili kuhakikisha kwamba tunapunguza au hatimaye kumaliza kabisa migogoro kati ya wananchi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Hatua ya kwanza, tumeamua kuyapima maeneo ya Jeshi hasa yale yenye migogoro, likiwemo lile eneo la Kambi ya Bauvai na maeneo mengine ili kuainisha mipaka kati ya Jeshi na Wananchi.

Pili, kuwalipa wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa na Jeshi kwa ajili ya shughuli za ulinzi.

Tatu, kuendelea kuwaelimisha wananchi nao waheshimu na wathamini maeneo ambayo yanamilikiwa na Jeshi kwa sababu Jeshi la Wananchi wa Tanzania lipo kwa ajili ya shughuli za ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, najua wananchi wanayatamani sana maeneo ambayo yanamilikiwa na Jeshi kwa ajili ya shughuli za maendeleo, lakini ni kweli vile vile kwamba, Jeshi linahitaji maeneo hayo kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anashughulikia migogoro akumbuke na Kambi ya JKT Msange kule Tabora na yenye wengine iko kwenye mgogoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia niseme kwamba, kwa kuwa migogoro hii mingi inatokana na uhaba wa maeneo yaani ardhi kwenye Kambi ambazo zimekuwa katikati ya miji. Je, kwenye ufumbuzi wa kudumu, kwa nini Mheshimiwa Waziri asiliete Kambi zingine kwenye maeneo ambayo yapo tu kama Iramba kule na eneo lilishakubalika, lipo, halina mgogoro ili kuyaacha maeneo ya mjini ambako ardhi imekuwa kwa matumizi ya binadamu wengine?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nimekubali kwamba Kambi ya JKT pale Msange ina tatizo la mgogoro wa ardhi. Kama nilivyosema, tutafanya kila linalowezekana kushughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, suala la kuhamisha Kambi za Jeshi la Wananchi wa Tanzania kutoka maeneo ya mjini kwenda maeneo ya vijijini, nasema kwamba, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limewekwa katika maeneo haya, hasa katika maeneo ambayo ni nyeti na yana umuhimu sana katika shughuli za ulinzi.

Mheshimiwa Spika, litakuwa ni jambo la ajabu sana, Jeshi unaliondoa katika eneo la mjini kama kwamba hatuna dhima ya kuwalinda wananchi waliko kwenye maeneo ya mjini. Nasema tu, ushauri tumeupokea, lakini ni jambo ambalo tunapaswa kulizingatia, kwa sababu umefanyika utaaliam sana wa kitaalam ili kujua kwa nini Kambi inawekwa kwenye maeneo mahususi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ombi hilo, tatalifanyia kazi na kutoa uamuzi, nadhani kwamba uamuzi huo utakuwa wa busara na wa hekima.

**SPIKA:** Tuendelee na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Donald Max atauliza swali hilo!

Na. 429

### **Kufufua Kiwanda cha Ushirika Geita**

**MHE. DONALD K. MAX** aliuliza:-

Geita ni Mkoa mpya na una kiwanda kimoja cha Ushirika pamoja na maghala kadhaa ya kuhifadhi bidhaa na nafaka:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukabidhi mali hizo za ushirika ili Mkoa mpya wa Geita uweke mikakati ya kufufua kiwanda hicho ili kuongeza ajira kwa wananchi na kuongeza pato la Taifa pamoja na kuwapa moyo wakulima wa zao la pamba ambalo liko katika hali mbaya?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa mpya wa Geita una Viwanda vitatu vya Kuchambua Pamba, vilivyoko Kasamwa, Chato na Masumbe, ambavyo vimelalamikiwa na Vyama Vikuu vya Ushirika vya *Nyanza Cooperative Union (1984) Limited- NCU, Shinyanga Region Cooperative Union (1984) Limited- SHIRECU* na Biharamulo *Cooperative Union (1996) Limited* ambavyo viko katka Mikoa mitatu ya Mwanza, Shinyanga na Kagera.

Mheshimiwa Spika, Jineri (Kiwanda) cha Kasamwa ni

mali ya Wanaushirika wa Geita kuitia *Nyanza Cooperative Union (1984) Limited*. Aidha, Vyama vya Ushirika vya msingi vilivyopo Mkoa wa Geita ni vyama wanachama ndani ya *Nyanza Cooperative Union (1984) Limited*, ambavyo vilichangia, vimewekeza rasilimali zao ikiwa ni pamoja na mitaji na katika shughuli za uzalishaji mali ikiwemo ujenzi wa Kiwanda cha Kasamwa na hivyo Kiwanda cha Kasamwa bado ni mali vya Wanaushirika wa Geita.

Mheshimiwa Spika, mali za kudumu za Vyama Vikuu vya Ushirika zilizoko kwenye eneo la utawala wa Mkoa wa Geita zinaweza kuendelea kuwa za Wanaushirika kwa utaratibu wa Vyama Vikuu vyenye mali za kudumu kuwauzia Wanaushirika walioko katika Mkoa wa Geita Hisa. Aidha, Wanaushirika waliokuwa wanahudumiwa na *Nyanza Cooperative Union (1984) Limited, Shinyanga Region Cooperative Union (1984) Limited- SHIRECU* na *Kagera Cooperative Union-KACU*, pamoja na *Biharamulo Cooperative Union (1996) Limited-BCU* ambao kwa matakwa yao walijitoa kwenye Vyama Vikuu vya Ushirika, kwa mujibu wa Kifungu cha 96 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2003, watalazimika kugawana mali na madeni yaliyopo, hivyo kuanzisha Chama cha Ushirika kipyä kikirithi mali za madeni yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mali za Kiwanda cha Kaswamwa zipo chini ya ushirika, Serikali haiwezi kukabidhi mali hizo za Ushirika kwa uongozi wa Mkoa mpya wa Geita kwani Wanaushirika wenyewe ambao ndio wamiliki lazima washirikishwe kutoa uamuzi kuhusu mali hizo ikiwa ni pamoja na kutafuta mbia mwenza au mwekezaji.

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Hapa swali langu nafikiri halikueleweka vizuri, kwa sababu siyo nia yetu sisi kwamba hii mali ya Wanaushirika ipewe Serikali. Tunachosema ni kwamba, *Nyanza Cooperative Union*, pamoja na *SHIRECU* pamoja na *Biharamulo Cooperative*, hivi Viwanda vyote vya Pamba sasa

hivi, asilimia 90 viko *ICU*, sisi tunavitezama tu, hii ni miaka karibu miaka 15 hivi viwanda havifanyi kazi watu wanang'oa vipuri wanakwenda kuuza kama *scraper*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kujua Serikali inakuja na mkakati gani, tutakaa tunavitezama tu vimekaa. Kwa sababu hivi viwanda ndivyo viliviyowasomesha Babu zetu, Baba zetu na hata sisi. Nataka kujua Serikali inakuja na mkakati gani, hata vile vyta nguo, Tabora *Textile*, Mwanza *Textile*, vyote vimelala. Tunataka kujua Serikali ina mikakati gani? (*Makofu*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tena sawa sawa Waziri wa Viwanda, hata kama ni ya Kilimo lakini ni ya Viwanda.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y.)**

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema kwamba, Vyama Vikuu vikongwe, kama vile Nyanza na Mwanza kile cha *National Cooperative Union*, pamoja na Biharamulo ni vyama vikongwe ambavyo kwa sasa hivi viko *ICU*. Lakini kwa vile anasema kwamba, kuna Kiwanda cha Kuchambua Pamba cha Kasamwa ambacho kipo Geita na halafu suala la kuomba kwamba Chama cha Ushirika kiundwe Geita wakati Kaswamwa iko Geita na Kaswamwa iko chini ya *Nyanza Cooperative Union*.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda hiki cha Kasamwa kilijengwa mwaka 1959 na sasa hivi nacho kinafanya kazi vizuri siyo vibaya sana. Lakini kuundwa ushirika wa Geita kwa sasa hivi itakuwa ni vigumu. Ombi hili limefanywa na Mkuu wa Mkoa ambaye amemwandikia Mrajisi wa Vyama vyta Ushirika ili aweze kuunda Ushirika mpya kwa Geita, ukiachana na Vyama Vikuu hivi kama nilivyosema vyta Nyanza, Mwanza na kule Kagera.

Mheshimiwa Spika, shida ni kwamba, Wanaushirika wa Kasamwa ndiyo wamiliki wakuu, lazima washirikishwe kama kuna kuunda Ushirika mpya na kwa sababu nimesema kwamba Kasamwa yenye ipo chini ya Nyanza. Kuua Nyanza au kuanzishwa kwa Kasamwa ni lazima Wanaushirika

wa Kasamwa ambao ndio wamiliki washirikishwe. Iko sheria ya vyama vya ushirika ambayo inatawala, kwa hiyo kama ni kuuawa kwa Vyama vile Vikuu vitatu na kuanzisha chama kingine kipyta, au kubakiza kile cha Kasamwa ambacho kipo Geita na kina Washirika wa Geita, Sheria iliyopo lazima ichukue mkondo wake.

**SPIKA:** Tatizo la Viwanda vyote vilivyo simama, ndicho tunachotaka kusikia. Naomba nimpe Waziri wa Viwanda na Biashara, pengine.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuongezea majibu ya swali la Mheshimiwa Max, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kwamba hivi sasa baadhi ya Viwanda hasa vya Pamba, vingi havifanyi kazi. Lakini mkakati tunaouchukua sasa hivi, tayari tumekwisheswasiliana na Kampuni moja kubwa tu kutoka Japan, ambayo inaitwa Nitori ambao wao wana nia ya kuwekeza katika eneo la kutengeneza nguo na kuzalisha Pamba yenye.

Mheshimiwa Spika, tayari Kampuni hii imekwisheshatembelea mikoa kadhaa pamoja na Shinyanga. Wamekwishafika maeneo ya Geita, kitu wanachokifanya sasa ni kuzungumza na wahusika wa *Ginnes* hizi ili kuona ni uwezekano gani kama wanaweza kuingia ubia na kufanya kazi kuhakikisha kwamba Viwanda hivi vinafanya kazi. Kwa hiyo Kampuni hiyo ya Nitori tume shakaribisha na tayari imeshaonesha *interest* ya kuendeleza viwanda hivi. (*Makof*)

**SPIKA:** Nadhani Mawaziri wote mnataka mjibu. Haya, Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nataka kutoa taarifa kwamba, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa, tume shasoma mara ya Kwanza Muswada wa Sheria mpya

ya Ushirika. Naomba Waheshimiwa Wabunge waisome, Sheria ile, kwa sababu katika Bunge ijalo tutaipitisha, ndiyo itatoa kasoro zote ambazo Mheshimiwa Max ameuliza zinazotokana na Sheria.

Mheshimiwa Spika, tunajua uko udhaifu mkubwa sana ambao umesababisha vyama hivi vingi vya Ushirika kufilisika, *SHIRECU*, Nyanza na vingine. Kwa hiyo, nawaomba sana marekebisho yote ya Sheria hii mpya ya Ushirika inayokuja tujizatiti vizuri hii ndiyo itakayotoa majibu ya kwamba vyama vya sasa vinaundwa namna gani na mali zake zinakwenda mahali gani.

Mheshimiwa Spika, la pili, juu ya mali zilizokwishauzwa ambazo hazifanyi kazi, tulishawahi kusema hapa, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Serikali imeshafanya tathmini ya mali zote, viwanda na mashirika yote yaliyouzwa, ili kubaini hali yake na namna ya kufanya, yaani *CHC* imekwishapendekeza hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa taarifa hiyo iko Serikalini na wakati wowote Serikali itatoa taarifa baada ya kuipitia, mambo gani yafanyike kulingana na mapendelekezo ya *CHC*, kwa Shirika na Kampuni moja moja iliyokwishauzwa ili viweze kufufuliwa na viweze kufanya kazi. (*Makof*)

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, nataka kutoa ufanuzi tu juu ya Sheria ya Ushirika. Kwamba iwapo wanachama wa Geita wanataka kuunda Chama chao cha Ushirika na kwa sababu kuunda Ushirika ni hiari, uko utaratibu hata kwa sheria ya sasa ambao unawawezesha kutumia mikutano mikuu ya Vyama vya Ushirika ambavyo wanachama wa Geita ni wanachama ili kuweza kufikia maamuzi ya kama wanaweza kuunda ushirika nje ya Nyanza *Cooperative Union* au *SHIRECU*.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile mali za Vyama vile zina matatizo kwa sasa kwa sababu nyingine zimewekezwa, kwa hiyo, hata kama wakiunda ushirika wa Geita sasa,

watapata matatizo ya kupata mgao wa mali za vile vyama, mpaka migogoro inayohusiana na mali hizo itakapokuwa imetatuliwa.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na swali liliobaki la Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, swali hilo litaulizwa na Mheshimiwa John Mnyika, kwa niaba yake Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

Na. 430

**Sera ya Taifa ya Vijana na Mkataba  
wa Vijana wa Afrika**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. JOHN J. MNYIKA)** aliuliza:-

Utekelezaji wa haraka wa Sera ya Taifa na Mkataba wa Vijana wa Afrika ni hatua muhimu katika kuboresha maisha ya vijana na kuchangia katika maendeleo ya nchi:-

(a) Je, ni lini Serikali itawezesha kukamilishwa kwa mchakato wa uundaji wa Baraza la Vijana la Taifa?

(b) Je, ni hatua gani imefikiwa katika kuanzisha Benki ya Vijana Tanzania ili kurahisisha mfumo wa Vijana kupata Mikopo na mitaji ili kuweza kujajiri;

(c) Je, lini Sheria itatungwa ya kuwezesha utekelezaji wa malengo ya msingi ya Sera ya Taifa ya Vijana na Mkataba wa Vijana wa Afrika?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA  
MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Mnyika, lenye sehemu (a) (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mchakato wa uanzishaji wa Baraza la Vijana unaendelea vizuri. Hadi sasa Waraka kwa Baraza la Mawaziri kuomba kutunga Sheria ya kuanzisha Baraza la Vijana umekwishajadiliwa katika ngazi ya Makatibu Wakuu na baadaye kupelekwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa maelekezo zaidi. Mara uamuzi wa Baraza la Mawaziri ukitolewa hatua ya kuandaa Muswada itaendelea.

(b) Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa katika kuanzisha Benki ya Vijana ni kwamba hadi sasa mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi upo katika hatua za mwisho. Mara Mshauri Mwelekezi akipatikana atafanya upembuzi yakinifu na kutoa ushauri wa kitaalam ambao utazingatiwa katika kuanzisha Benki ya Vijana endelevu.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Waraka wa Baraza la Mawaziri wa kuomba kutungwa Sheria ya utekelezaji wa Mkataba wa Vijana wa Afrika unaandalialiwa, pindi utakapokamilika utapelekwa kwenye ngazi za juu za Serikali kwa utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuandaa Muswada wa Sheria.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kujua, kikubwa ambacho tunazingatia hili suala litachukua muda gani yaani tuwe na *timeframe*, isije akawa mpaka wanafikia kuwa wazee huu mchakato na upembuzi haujakamilika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, swali lingine, pamoja na vijana kuwezeshwa na kuweza kupata namna ya kuweza kujikimu, lipo suala la Utaifa kwa Vijana. Zipo jitihada kubwa ambazo zimeoneshwaa na Dkt. Mengi ambaye anamiliki *Radio One* na *Clouds FM* inayomilikiwa na Joseph Kusaga, kuhamasisha Utaifa, uzalendo kwa vijana. Sasa Serikali inatoa tamko gani, kwa vyombo vingine vya habari kuiga mfano huu mzuri wa kuhamasisha vijana kuelewa nini maana ya uzalendo na Utaifa wao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri unaombwa ujibu. Wakizeeka, vijana wengine wanakuja. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema katika mjadala wetu wakati tunawasilisha Bajeti hapa, tulisema kwamba jambo hili limechukua muda mrefu. Lakini tumefanya jitihada, mpaka sasa tayari suala hili limeshajadiliwa katika Kikao cha Makatibu Wakuu na limekwenda kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, muda wowote utakapokuwa umekamilika, sisi tutaleta Muswada huu hapa utungiwe sheria, lakini pia nilishaahidi kwamba mimi mwenyewe ni mdau katika suala hili la vijana toka lilipoanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, nakubaliana na Mheshimiwa Mangungu, namna ambavyo vyombo vyaa habari vinaendelea kuelimisha vijana na suala zima la Utaifa. Nataka kusema kwamba, katika Mkataba huu wa Afrika wa Vijana, unaeleza nchi wanachama wajibu wao kwa vijana, lakini na wajibu wa vijana kuhakikisha kwamba wanatii sheria na kulinda nchi yao na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye na navitaka vyombo vyaa Habari vyote na kuwataka vijana kuona kwamba, wanadumisha amani na kuwa na maadili mema na kujenga utaifa katika Taifa letu la Tanzania. (*Makofii*)

Na. 431

### **Wananchi Kuibiwa kwa Ujazo wa Lumbesa**

**MHE. MCHUNGAJI LUCKSON N. MWANJALE** aliuliza:-

Wananchi wanapouza mazao yao kama vile mahindi, viazi na kadhalika hutakiwa kupima kwenye lumbesa ambaao ni ujazo mara mbili zaidi ya ujazo wa kawaida.

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya wizi huo unaofanywa na wafanyabiashara kwa wananchi?

## NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kusema kwamba, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha wafanyabiashara wanatumia vipimo vilivyo halali wanaponunua mazao kutoka kwa wakulima. Niseme hapa na niwaeleze wafanyabiashara na wakulima wote kuwa, hakuna sheria inayosema kuwa wakulima wanapouza mazao yao eti wanatakiwa kupima kwenye lumbesa. Huu ni udanganyifu na kuwadhulumu wakulima.

Mheshimiwa Spika, nawaagiza wafanyabishara kote nchi, kuacha mara moja mtindo wa kuwalazimisha wakulima kutumia vipimo vya Lumbesa wanapouza mazao yao na vile vile wakulima wasishurutishwe kutumia lumbesa. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wafanyabiashara wote watakaokiuka agizo hili.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Vipimo Na. 20 ya mwaka 1984 ikisomwa pamoja na Tangazo la Serikali na 16 la tarehe 8 Februari, 2008 inaeleza bayana matumizi ya mizani sahihi katika kufanya biashara, vipimo vya Lumbesa ni vipimo batili na haviruhusiwi kisheria kutumika katika kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imefanya marekebisho ya Sheria Mama (*The Weight and Measures Act, 1984*) na kuwa (*Legal and Metrology Act*) kwa lengo la kuongeza usimamizi, udhibiti na adhabu kali dhidi ya wafanyabiashara watakaokiuka sheria hii. Mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria hii yamepelekwa katika Baraza la Mawaziri kwa kuridhia na baadaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa suala hili la lumbesa, limejitokeza hapa katika Bunge lako Tukufu zaidi

ya mara tatu na majibu karibu ni yale yale. Sasa sijajua na zoezi la kudhibiti lumbesa bado haliendelei limekwama, nauliza je, Serikali ina mkakati gani mpya kabisa, ambao kwa kweli utafanya zoezi liweze kufanikiwa?

Mheshimiwa Spika, maagizo hayo wamepewa wafanyabishara, lakini kwa nini Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wasipewe maagizo haya ili waweze kusimamia zoezi hili?

**SPIKA:** Nami naunga mkono suala hilo, ninalo tatizo kubwa kabisa la lumbesa kwangu. Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaomba majibu ya kuridhisha. (*Makoff*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, suala la lumbesa lina wabia wengi, kusema kweli linapaswa likomesha kabisa ili suala hii lidhibitiwe mikoa yote nchini na liishe kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalı lake la kwanza, la kwamba mkakati gani ambao Serikali inafanya ili kukomesha kabisa lumbesa, labda niseme kwamba, sasa hivi kulikuwa na tatizo la sheria iliyokuwepo, ilikuwa inatoa adhabu ndogo sana. Kama mnavyofahamu ilikuwa inatoza Sh. 10,000/= kwa mfanyabiashara yejote ambaye alikuwa anakiuka sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili limekuwa ni tatizo na limetunyima meno sisi watu wa Serikali hasa Wizara katika kutoa adhabu kati. Kwa hiyo, mfanyabiashara akitozwa Sh. 10,000/= alikuwa anaona ni kitu kidogo, hivyo aliendelea kuvunja sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na tatizo hili, ndiyo maana nikasema kwamba, Serikali inabuni au imeanzisha sheria hii mpya ambayo itatoa adhabu kali sana kwa wafanyabiashara ambao watakuwa wanakiuka sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mapendekezo ambayo tumeyapeleka kwenye Baraza la Mawaziri ni

kwamba, kosa la kwanza liwe na adhabu kali, kiasi cha shilingi milioni 100 au miaka mitatu jela au vyote kwa pamoja. Kama utaendelea kufanya kosa, kosa la pili, litakuwa na adhabu kali vile vile ya shilingi milioni 200 pamoja na miaka saba (7) au vyote kwa pamoja. Hiiyo nafikiri itasaidia sana katika kukomesha suala hili la lumbesa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, la kusema kwamba tushirikishe viongozi wengine wa Mkoa na hata Wilaya. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ya kwamba, Sheria hii mpya tayari imeshajaribu kuwaunganisha Wakuu wote wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya ikiwa ni pamoja na Viongozi wengine wa Halmashauri zote, ikiwemo Manispaa na Majiji, Viongozi wa Kata, Vijiji na Vitongozji ili waweze kushirikishwa katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii mpya kutakuwepo na vituo vyta mauzo ya mazao yaani *Trading and Services Centre* vitakavyotumika kwa ajili ya kuwawezesha wakulima wote kupeleka mazao yao katika eneo moja, ambapo zoezi la ukaguzi na uhakiki wa vipimo kwa mujibu wa Sheria litafanyika. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumetumia muda mwingu sana ambao siyo wa maswali.

Napenda kusema kwamba, tunaye Profesa Nderakindo Perpetua Kessy ambaye ni Mbunge wa Bunge wa Afrika ya Mashariki kwa upande wa Tanzania, yuko hapa kututembelea, karibu sana. Nadhani tutapata muda wa kuongea naye. (*Makofii*)

Halafu nina shughuli za kazi. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa *Captain* Mstaafu John Chiligati, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 219. Hivyo basi, Wajumbe wa Kamati ya Maadili wawe tayari kuhudhuria.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**SPIKA:** Mwongozo hauna tatizo utauliza badaye.

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2012/2013 Pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2013/2014 na Makadirio y Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2013/2014**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wafuataao ndiyo wataanza kuchangia hii hoja. Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yusuf Masauni, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Susan Kiwanga, hayupo; Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Khatib Said Haji. Sasa namwita Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mtu wa kwanza kuchangia leo.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu ya Serikali ya mwaka huu, mimi binafsi sina pingamizi na vipaumbele hasa kwa kuwa suala la umeme ni moja katika vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuongeza bajeti kwenye sekta ya umeme kutoka shilingi bilioni elfu moja mia nne na kitu kutoka shilingi mia saba na themanini na kitu hiyo mwaka jana ni jambo ambalo linapaswa kupongezwa. Tukiamini kwamba sekta ya umeme ni muhimu na athari zake sote tunazijua, leo hii kutokuwepo kwa mgawo wa umeme kumesaidia sana kuweza kupunguza *inflation* ambayo ilikuwa inawaathiri sana wananchi wa kawaida katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika eneo la umeme vijijini, nipongeze jitihada za kuongeza bajeti katika eneo hilo

na sasa hivi tumefikia 21% ya wananchi ambao wanapata umeme Tanzania kutoka 10% kwa takribani si zaidi ya miaka 10 toka kuanzishwa kwa Mfuko huu wa *REA*. Kwa hiyo, ni jambo jema sana kuongeza fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo langu kubwa lipo katika masuala mawili makubwa yaani utekelezaji na udhibiti. Inasikitisha sana na inauma sana kwamba sisi Wabunge wa Zanzibar kila siku tukichangia humu katika bajeti maneno ni hayo hayo, kulalamika, kero na mambo ambayo hayaishi.

Mheshimiwa Spika, inatupa mashaka sana hasa kuhusiana na watendaji wa Wizara hii ya Fedha, leo hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepitisha bajeti yale ikitegemea kama ulivyo utaratibu wa *GBS* ama mgao wa fedha za wafadhili kwa 4.5% kama ilivyopangwa. Lakini hivi tunavyozungumza matatizo haya ya kila kukicha mpaka Januari mwaka 2013 *GBS* iliyolipwa ni shilingi milioni 20 peke yake.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, lakini katika eneo linguine, *payee* ambayo miaka iliyopita tumekuwa tukiipgia kelele hapa Bungeni, tumekuwa tukizungumza na tukiahidiwa kwamba hili jambo litapatiwa ufumbuzi, lakini mpaka tunavyozungumza *payee* ya kuanzia mwezi Februari, Machi na Aprili bado haijalipwa na wala haina dalili ya kulipwa. Mheshimiwa Waziri ni lazima atueleze ni kwa nini hii haijalipwa, lakini siyo kutueleza tu bali tunataka *payee* ya miezi mitatu ilipwe na matatizo haya yasijitoneze tena.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunawapa watu midomo tu, watu ambao hawaitakii mema nchi hii, watu ambao hawautakii mema mustakabali wa Muungano wetu kupata visababu vya kuweza kuathiri Muungano wetu kwa mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wetu na mambo ambayo hayaonekani ni kwa nini yanafanya hapa.

Mheshimiwa Spika, kama sheria ipo na utaratibu unaeleweka ni kwa nini sasa watendaji hawa wanakuwa na kiburi kiasi hicho? Itoshe kwamba, fedha hizi zilipwe lakini na

watendaji hawa wachukuliwe hatua ili liwe fundisho kwa wengine ambao wanachangia katika kuzorotesha mustakabali wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka nizungumze katika eneo hili hili la utekelezaji wa bajeti na eneo hili hili ambalo Zanzibar imekuwa ni muathirika mkubwa. Katika utekelezaji wa bajeti hii, ni lazima Serikali iwe na mipango ambayo inatekelezeka na niipongeze Serikali kwa kufanya hivyo, lakini kama hatujasimamia na hatujawajibika, matatizo haya hayatakwisha.

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo la pili lililozungumzwa ni eneo la udhibiti, Tanzania ama nchi yetu inapoteza fedha nyngi sana katika bandari, niipongeze juhudhi ambazo zimechukuliwa mpaka sasa hivi na Serikali kufanya udhibiti wa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, lakini hiyo haitoshi, taarifa ambayo imetolewa na *Tanzania Economic Update* inaonesha kwamba nchi yetu kupitia bandari moja tu ya Dar es Salaam peke yake inapoteza dola za Kimarekani bilioni 1.8 kwa mwaka, ambayo hiyo ni sawa na 7% ya pato la Taifa. Lakini pia inapoteza kodi kupitia *TPA* kwa wastani unaokadirisha dola za Kimarekani milioni 157, ukiachilia mbali athari ambazo zinatokea kwa nchi jirani ambazo zinatumia bandari hii kusafirisha mizigo yake.

Mheshimiwa Spika, hali hii haivumiliki hata kidogo. Haiwezekani leo Serikali inapanga bajeti ya kuwakamua wananchi kulipa kodi, lakini wakati huo huo kuna maeneo ambayo yanavujisha kodi na yanaendelea kuachiwa. Niseme kwamba kuna jitihada zinahitajika kuongezwa katika kuhakikisha kwamba udhibiti wa mapato ya nchi hii katika maeneo mbalimbali unaimarishwa. Eneo moja ambalo linasikitisha na linahitaji kuangaliwa zaidi na zaidi ni kuongeza jitihada ni eneo la bandari.

Mheshimiwa Spika, leo hii utafiti unaonesha kwamba, inachukua takribani siku kumi kwa meli kupanga foleni kutua

mzigo wake bandarini, lakini siku kumi nyingine kwa ajili ya kuupakua mzigo ule mpaka uweze kusafirishwa wakati *International Standards* inahitaji mizigo hii iwe inatolewa kwa muda wa siku mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kana kwamba hiyo haitoshi, nchi yetu ipo katika ushindani wa Jumuia ya Afrika Mashariki, leo hii wenzetu wa Kenya, bandari yao ya Mombasa ambao wameanzisha mfumo mpya ambao unaitwa *National Sing Window* ambao utasaidia kuimarishe na *ku-improve efficiency* katika bandari yao, lakini wao inachukua nusu siku tu kwa meli kufikia bandarini na takribani siku tatu mpaka nne pekee.

Mheshimiwa Spika, sasa tukiangalia tofauti hii ni kubwa mno. Kwa hiyo, nahisi kwamba, suluhisho la matatizo ya ufanisi katika eneo hili la usafirishajili halipo katika uwezo, tuna bandari za kutosha kabisa, leo hii uamuzi wa kujenga bandari Bagamoyo sioni kama una haraka hivyo. Tatizo liliopo ni ufanisi duni uliopo katika bandari zetu, tuna bandari ya Zanzibar, Mtwara, Tanga na kadhalika, hizi zingeweza kabisa kuimarishe na kuwa na uwezo wa kuhimili ufanisi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ni suala la rushwa iliyokithiri katika mifumo ya kodi ya nchi yetu na hasa katika hili eneo la bandari. Inakisiwa kwamba takribani dola la Kimarekani 13,000 hutumika kwa ajili ya rushwa tu. Sasa niseme kwamba, kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba, Wabunge wengi wamechangia wamelizungumzia kwa hisia kali sana hili.

Mheshimiwa Spika, wapo wengine ambao walikuwa kila siku wanazungumzia kwamba suala la rushwa limekuwa ni wimbo wa Taifa, kila siku tumekuwa tukizungumza tu lakini hatua madhubuti bado hazijachukuliwa. Kuna haja ya Serikali kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo zimetengwa zinatumika katika kuhakikisha kwamba ufanisi unapatikana kwa maana ya kuimarishe miundombinu na teknolojia katika bandari, lakini kuhakikisha kwamba suala la rushwa

linafanyiwa kazi ipasavyo na hatua kali zinachukuliwa kwa wale wote ambao wataonekana kwamba wanapokea ama kutoa rushwa.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba, maeneo hayo yakiangaliwa kwa undani zaidi na kupewa msukumo wa kipekee, basi nchi yetu itaweza kuhakikisha kwamba inaimarisha ufanisi na hatimaye kodi inaweza kukusanywa na kutumika inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, jitihada zilizotumika za kuongeza kodi katika baadhi ya maeneo mbalimbali ni jitihada ambazo zinatia moyo ingawa maeneo yamekuwa hayo hayo kila siku. Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali kuwa wabunifu zaidi katika kuona kwamba inaongeza kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, eneo moja la kodi katika maeneo ya mazao, hili kwa kweli si jambo la busara sana, kwa sababu unapoongeza kodi katika maeneo ya mazao, maana yake unapeleka mzigo ule kwa wananchi wa kawaida ambao hatma yake inachangia katika kuongeza ugumu wa maisha, lakini pia kuongeza mfumuko wa bei katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kwamba kwa ujumla bajeti yetu hii haijaka vizuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nashukuru, Mheshimiwa Jenista Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed. Kama hayupo atatengewa baadaye.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi

hii nikipongeze sana Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa ambao umepatikana katika chaguzi ndogo za Kata ambazo zimefanyika muda si mrefu uliopita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ni dalili kwamba, bado Watanzania wana imani na Chama cha Mapinduzi na wana imani na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wale wote walioamua kuchagua Madiwani wa Chama cha Mapinduzi kwa sababu wamechagua chaguo la maendeleo. Nawapongeza sana! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nikupongeze sana wewe mwenyewe, kwa mara ya kwanza Bunge letu limeweka historia. Limeweka historia ya kuunda mfumo mpya wa bajeti ambao ni mfumo wa mashauriano kati ya Bunge ambao ni wawakilishi wa wananchi na Serikali ambayo ni wasimamizi wa shughuli za maendeleo na hatimaye leo tunaona kwamba mfumo huu mpya umeweza kutufikisha mahali pazuri sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni ushahidi wa kutosha kwa Watanzania na wale wote waliokuwa wanabeza kwamba, Bunge hili halipo makini, lakini naomba niseme kwa mara ya kwanza tumewathibitishia kwamba, tupo makini, tumejipanga sawasawa kwa maslahi ya Watanzania zaidi na hii imejidhihirisha kwa kazi tulizozifanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imetufanyia kazi nzuri sana kwa kushirikiana na Serikali na tumeona hapa, naomba niwaambie Watanzania, wakati tunaendelea na bajeti, tuligundua mambo mengi ya kimsingi ambayo Watanzania kuititia Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi walitakiwa wayapate.

Mheshimiwa Spika, tuliomba fedha ziongezwe kwenye bajeti ya Maji zimeongezwa, tuliomba fedha ziongezwe kwenye Mifugo zimeongezwa, tuliomba fedha ziongezwe kwenye bajeti ya Kilimo ili wananchi waweze kupata pembejeo na ruzuku zimeongezwa, tuliomba fedha

ziongezwe kwa ajili ya maendeleo ya akinamama katika nchi ya Tanzania zimeongezwa, tuliomba fedha ziongezwe kwa ajili ya Vijana imeongezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tuliomba fedha ziongezwe kwa ajili ya Miundombinu ya mawasiliano zimeongezwa, tuliomba fedha ziongezwe kwa ajili ya madawa kwa wananchi wa Tanzania zimeongezwa, tumeomba fedha kwa ajili ya umeme vijijiini vikiwemo vijiji vyangu vya Jimbo la Peramiho fedha zimeongezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa haya ni machache, yapo mambo mengi, wananchi wa Jimbo la Peramiho nisubirini, baada ya Bunge hili nitakuja kuwaeleza moja baada ya linguine, nini mmeputa katika bajeti hii shirikishi ya Serikali. Serikali ya Chama cha Mapinduzi iendelee kudumu na iendelee kuwa sikivu kama hivyo nilliyosema na kuwa kwa kufanya hivyo, mnaokoa maisha ya Watanzania wengi na kuwaletea maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nijikite sasa pia katika maeneo kadha wa kadha katika bajeti hii. Eneo la kwanza, kipindi hiki ambacho kwa sababu bado tunaendelea na mashauri na Serikali kuhusiana na haya ambayo Serikali imetuletea na Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mtemi Chenge imetuletea, naomba nirudie kusema, Mheshimiwa Chenge atakapokaa na Serikali kodi hii iliyoongezwa kwenye mafuta na hasa *petrol* na *diesel* ikaondolewe na kama siyo kuondolewa yote ikapunguzwe kwa kiasi kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia suala la mfumuko wa bei, *base* ya mfumuko wa bei ni mafuta. Leo tunategemea mafuta kama ni chanzo cha kila kitu, mitambo yote ya kuzalishia mazao, mitambo yote ya viwandani, usafirishaji na usafiri vyote vinategemea mafuta. Kwa kuongeza tozo hiyo, tutakwenda kuwatesa sana wananchi wa Tanzania na hasa wale ambao wako vijijiini. Nashauri sana katika eneo hilo kwa kweli kuna umuhimu wa kwenda kuangalia upya.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ile kodi iliyoongezwa kwenye ngano, hiyo nayo tukaitazame. Hofu yangu akinamama wengi na hasa wafanyabiashara wadogo wadogo wanategemea biashara hizi za bidhaa zinazotokana na unga wa ngano. Akinamama lishe na Mama ntilie wengi sana mpaka vijijini wanategemea unga wa ngano, ndiyo kitega uchumi chao kikubwa. Nadhani tuna umuhimu wa kuangalia pia eneo hilo kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kufuta kodi kwenye huduma ya Bajaji itasaidia, lakini nafikiri kuna umuhimu wa kutazama, tunapofuta hiki tunafanya kitu gani Kingine ili kuweza kuongeza mapato katika kodi zetu? Tulishaunda Tume ambayo ilifanya uchunguzi wa kiasi cha kutosha kupitia Bunge lako kuangalia vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, niungane mkono na Wabunge waliosema, hivi kweli Serikali mmeshachukua karibu yale mawazo yote ya vyanzo vyote vyta mapato ambavyo vinaweza kuongeza angalau kufidia huko tunakoshauri tuondoe kuwakandamiza Watanzania kwenye kulipa kodi?

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu wamezungumza kuhusu suala la uvuvi katika maji marefu. Hivi tunapata kigugumizi gani kusimamia mapato yanayotokana na uvuvi ndani ya bahari? Naomba tuone namna gani tunaweza kufanya, bahari kuu uvuvi haramu unaendelea, nchi nydingine zinajitajirisha kwa kiasi kikubwa, tungeweza kupata mapato ya kutosha na hizi kodi mbili au tatu ambazo tumeziongeza, tunafikiri zitawaumiza wananchi, tungeweza kuachana nazo tukategemea uvuvi kutoka bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kipindi hiki cha mashauriano kwa sababu hajajitokeza kwenye Serikali. Hebu tuone tunawakamataje wale wavuvi kwenye bahari kuu waongeze mapato kwenye Serikali yetu ili tuweze kuendelea mbele.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia kwa ujumla wake suala moja ambalo ni la msingi sana sjui tunalitazama namna

gani. Ongezeko la idadi ya Watanzania kwa mtazamo wangu haliendani sambamba na ongezeko la uchumi katika nchi yetu. Idadi ya Watanzania inaongezeka kwa kasi kubwa, lakini ongezeko la uchumi wa nchi yetu haviendi sambamba.

Mheshimiwa Spika, sasa tukifanya hivyo nafikiri lipo tatizo mahali fulani kwenye mipango yetu. Narudia kusema kwamba, tunapokuja kwenye mipango, ina maana kwenye utaratibu wetu wa kuangalia vipaumbele, nadhani kuna mahali tuna matatizo, kuna mahali hatujakaa salama, iko haja kabisa ya Tume ya Mipango kuona nini kifanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ipo sekta ambayo tumeisahau sana na tunaidharau ambayo ingeweza kuchangia sana kukua kwa uchumi kwa kiasi kikubwa sana. Sekta hii siyo nyingine zaidi ya sekta isiyo rasmi ambayo inaweza kuunganisha wafanyabiashara wadogo wadogo kwa kiasi kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la uchumi na maendeleo ya uchumi, haliwezi kuacha kuendana sambamba na suala la ajira katika nchi yoyote. Utengenezaji wa ajira utakwenda sambamba na ongezeko la uchumi. Ukiangalia kwenye bajeti yetu mwaka huu fedha nyingi inakwenda kulipia mishahara, lakini mishahara hiyo ina tija kiasi gani katika kuleta maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania? Wapo watu wanalipwa mishahara hawana kazi wanazozifanya zenyetija kuleta maendeleo kwenye nchi yetu. Sasa nadhani tuitumie sekta hii isiyo rasmi katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma nikagundua kwamba, kwa mfano wenzetu wa Zimbabwe mwaka 1997 kupitia hii sekta isiyo rasmi, uchumi wa nchi yao ulichangiwa na sekta hiyo kwa 40% mpaka 45%, walifanya nini? Kwa sababu unapochukua sekta isiyo rasmi, ina maana kwanza, unakwenda kufanya kazi ya kuhamasisha uchumi mdogo mdogo vijijini. Pili, unakwenda kukuza teknolojia vijijini.

Mheshimiwa Spika, tatu unakwenda kutengeneza

masoko na nne unakwenda kutengeneza mzunguko wa fedha wa kutosha katika maeneo ya vijiji ambapo asilimia kubwa ya Watanzania wako huko na tunajua maendeleo ya nchi za Ulaya yalitokana na viwanda vidogo vidogo na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, sasa kama tutaweza kuweka kipaumbele kwa sekta hii isiyokuwa rasmi ikawakuta vijana huko, kwanza, tutawafanya wasihame kwenda mijini lakini mbili tutawatengenezea viwanda vidogo vidogo kule vijiji. Tukiweka pesa ya kutosha huko tutatengeneza masoko ya kudumu ya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, tatu tutatengeneza mzunguko mzuri wa fedha kule vijiji na hivyo ukuaji wa uchumi utaendana na ukuaji wa idadi ya Watanzania, lakini utakwenda kutatua tatizo la umaskini unaowagusa Watanzania moja kwa moja kule Vijiji. Tunalamika hapa uchumi unakua, lakini umaskini haufanyi haupungui wala hauondoki! Haya ndiyo matatizo ambayo nafikiri tunatakiwa kuyatazama.

Mheshimiwa Spika, tumetenga fedha kwenye Mfuko wa Vijana, sasa Mfuko huu tuwaombe wenzetu wa Serikali wanapoongeza hiyo fedha, tutazame namna ya kukuza teknolojia na ajira vijiji kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, tumetenga fedha za akinamama, nashauri tuzipeleke vijiji tukatatue hilo tatizo la ajira, lakini pia tukatengeneze teknolojia za kukuza uchumi kule ambazo zitasaidia kuondoa umaskini wa Watanzania kule vijiji. Hivyo ukuaji wetu wa uchumi utakwenda sambamba kwa maana ya kipato kuongezeka na hali za Watanzania, umaskini unaondoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri bado tuna kazi ya kutosha ya kujitathmini upya kuangalia mfumo wa vipaumbele vyetu...

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na nawatakia heri Serikali katika kutimiza majukumu hayo. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ajiandae.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa muda huu wa dakika 10 ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu katika bajeti hii kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze na ukurasa wa 64 wa hotuba ya Waziri kuhusiana na suala zima la ukusanyaji wa kodi. Tunalamika kuhusiana na suala zima la misamaha ya kodi. Katika ukurasa huu Waziri anaelezea kwamba, msamaha wa ushuru wa forodha utaendelea kutolewa kwenye vifaa mbalimbali viliviyotumika katika kutoa huduma ya utalii. Moja katika maeneo ambayo hatufanyi vizuri katika nchi yetu katika kukusanya kodi ni sehemu ya utalii.

Mheshimiwa Spika, ni dhambi kubwa kusamehe aina yoyote ya kodi ama ya VAT, ushuru au tozo la aina yoyote katika sekta ya utalii. Hivi sasa katika nchi yetu watalii wengi wanaokuja hapa wanakuwa wameshalipa kila kitu huko nje hata vitanda. Kwa kweli ni lazima Serikali ikae makini na iandae mpango mkakati mpya mwagine wa kuhakikisha wanadhibiti mapato au tozo hizi kutoka katika vyanzo hivi vya utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 71 Mheshimiwa Waziri anazungumzia suala la kuongeza ushuru wa bidhaa wa asilimia 14.5 kwenye huduma zote za simu. Fedha hizi anasema asilimia 2.5 zitatumika kugharamia elimu hapa nchini. Nakubaliana naye na nampongeza, ila nataka nitoe tahadhari na hasa kutokana na uzoefu ambao tumeupata huko nyuma, uzoefu wa fedha za rada.

Mheshimiwa Spika, fedha za rada zilikuwa ni za

Muongano, lakini matokeo yake fedha zile zikabadilishwa nadharia na kupelekwa kuhudumia shule za msingi. Kitu ambacho klijulikana dhahiri kwamba, unapopeleka katika shule za msingi Zanzibar haiwezi kupata pato lake pale kwa sababu elimu ile ya msingi si ya Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka Waziri alifafanue hili na aliweke vizuri, simu tunatumia Watanzania sote, hizi asilimia 2.5 Wazanzibari wao watapata nini? Tunaomba hili liwekwe katika hali nzuri ili ieleteweke mgawanyo wake utakuwaje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la vipaumbele. Tumeona vipaumbele vyetu hasa suala la miundombinu, nakubaliana nacho lakini uwanja wa miundombinu ni mpana. Nataka nichukue mfano mmoja wa kule Kigoma katika eneo la Katosh. Katika mpango, Serikali imesema kwamba pale imekusidia kuweka bandari kavu.

Mheshimiwa Spika, tatizo linalokuja pale ni kwamba, sasa hivi Halmashauri ya Kigoma inawanyanyasa na kuwasumbua wananchi wale wa Katosh. Lile eneo la Katosh kwa ajili ya bandari kavu lilipimwa tangu mwaka 1964, lakini leo hii wamekwenda kuweka mipaka mipya ambayo wanaingia hata katika nyumba ambazo ziko pale kwa muda mrefu. Hili linaleta usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali, pale wanapozungumzia suala la vipaumbele hasa katika maeneo kama haya ya wananchi, hebu wajaribu kuangalia au kuepuka kusababisha mkanganyiko na wananchi kwani hii inaleta shida.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wananchi wa Katosh hawazikani, Mheshimiwa Dkt Chizeba hili analifahamu, atusaidie tuondoe lile tatizo pale Katosh. Mipaka ilikuwepo tangu mwaka 1964 na bado iko, lakini leo wamekwenda kuweka mipaka mipya wanaingia mpaka kwenye maeneo ya wananchi, hii hali ikoje?

Mheshimiwa Spika, bado kuna eneo kubwa ukitoka pale ambalo ni pori tu liko wazi, kwa nini hawa wananchi wanyanyasike sasa hivi wakati ambapo hiyo reli yenye we bado Serikali haijawa nayo. Hiyo bandari yenye we ndiyo hivyo hivyo meli hakuna, leo mnaanza kusumbua wananchi wa Katosho bure! Serikali ione huruma katika hili ili wale wananchi kwa kweli wasisumbuke. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2008 ambayo inampa madaraka Waziri wa Fedha kukopa pamoja na ile Sheria ya *PPP* ya mwaka 2012 zinakinzana. Mkinzano huu wa sheria hizi unasababisha sasa baadhi ya Halmashauri zetu kupata matatizo na sasa hivi umesababisha urasimu kiasi kwamba, ule mtindo wa mwanzo wa Halmashauri zinapotaka kukopa inabidi sasa zirudi tena kwa Waziri wa Fedha. Kwa kweli hapa kunakuwa na urasimu.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni Halmashauri ya Mpanda wameleta maombi yao muda mrefu tu ya kutaka kukopeshwa fedha kwa ajili ya mipango yao ya maendeleo. Halmashauri ya Kilwa walitaka kujenga stendi pale Nangurukuru, mpaka leo hawajapewa majibu.

Mheshimiwa Spika, hebu Mheshimiwa Waziri azioneen huruma hizi Halmashauri zetu, wana mipango mizuri, wameibua mambo yao, wanahitaji kukopa fedha, wao wenye we wanajua namna gani ya kuzilipa. Hebu wasaidieni, hii hali ya kuwazungusha sana inakuwa siyo vizuri. Tumekubali hapa mfumo wa *D by D* tuwaachie waweze kufanya kazi, wanapokuja na matatizo yao wasaidieni kwa haraka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la matumizi makubwa ya Serikali na hapa nataka nzungumzie suala la *TANESCO*. Sasa hivi *TANESCO* haiwezi kuwekeza, hili ni suala ambalo liko wazi kwamba sababu kubwa ya *TANESCO* kushindwa kuwekeza ni mzigo mkubwa wa madeni ilionao ambapo sasa hivi inadaiwa takribani shilingi bilioni mia nne na kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli si rahisi kwa *TANESCO* kuweza kuijendesha au kuwekeza. Tunaiomba Serikali kama ambavyo imefanya kwa *STAMICO* na *ATCL* kwa kuyachukua madeni yao, hebu ichukue madeni ya *TANESCO* ili Shirika hili liweze kuijendesha au kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi *TANESCO* wanapewa takribani shilingi bilioni tano kwa siku kwa ajili ya kununua mafuta mazito ya kuendeshea mitambo. Mnawapa *five billion* kwa siku ambapo kwa mwaka ni takribani 1.9 trillioni. Hizi fedha kwanza tunaouliza zinatoka wapi? Ni fungu gani ambalo liliidhinishwa mkawenza kutoa fedha hizi *everyday* kupeleka *five billion TANESCO*? Tunaomba majibu ya Waziri wakati wa kuhitimisha.

Mheshimiwa Spika, mbali na hivyo ni kwamba, fedha hizi vile vile ni mbali ya zile shillingi billion 27 ambazo mnazitoa kwa ajili ya *capacity charges* na *energy charges*. Jana nilimsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasema kwamba, sasa hivi tunaingia katika mikopo na mkopo alioupata jana wa kujenga *flyovers* anasema ni mkopo poa.

Mheshimiwa Spika, hili neno poa liliwahi kuzungumzwa humu ndani ya Bunge na Mheshimiwa Naibu Waziri mmoja, wakati huo alikuwa *back bencher* na tafsiri yake akaita ni *paralysis of analysis*. Sasa hebu iangalieni *TANESCO* kwa upana wake, ili hii poa mnayoizunguza isiwe ni *paralysis of analysis*. Tunaliomba sana hilo kwenu. (*Makofu*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie thamani ya shilingi. Thamani ya shilingi yetu bado inaendelea kuporomoka siku hadi siku na hii ni kwamba wataalam wa Wizara ya Fedha pamoja na Waziri mwenyewe ama Naibu Mawaziri wenyewe, bado hawajajikita na kuwa makini katika suala zima la kudhibiti mzunguko wa fedha nchini. Nina shaka kwamba hivi sasa nikumuuliza Mheshimiwa Waziri ni fedha ngapi ziko katika mitandao ya simu au mikononi, sidhani kama atakuwa anaweza kupata jibu la haraka. Kwa hiyo, hii tunayoita *money circulation* inaonekana bado udhibiti wake ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa Wizara ije na mpango na mkakati maalum unaoonesha ni namna gani sasa hivi tunadhibiti fedha zetu ili shilingi yetu isiendelee kuperomoka.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine kubwa ni suala zima la *commodity exchange*. Mfumo wa *commodity exchange* una matatizo, uangalieni upya. Hii inasababishwa na suala zima la kuuza bidhaa zetu nje ya nchi. Wanunuzi wakubwa wa bidhaa zetu nje ya nchi ni matajiri wa humu humu ndani, wanwanuna kwa fedha zetu za ndani wanakwenda kuuza nje wao kwa fedha za kigeni. Matokeo yao hawa matajiri wanachokileta hapa ni balskeli, sijui vyandarua, mambo madogo madogo ambayo kwa kweli yanapoingia hapa nchini hayalipishwi ushuru. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa hili suala hebu liangalieni vizuri, tutakapoweza kutoa bidhaa zetu nyingi kuuza wenyewe nje, tutaingiza fedha za kigeni na hapa thamani ya shilingi yetu itaweza kuwa *stable*. Sasa hivi thamani ya shilingi yetu haiko *stable*. Tunaomba hilo Mheshimiwa Waziri wa Fedha alizingatie. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la deni la Taifa. Ukuaji wa deni la Taifa kwa kweli ni wa kasi mno kiasi kwamba sasa hivi unahatarisha hata usalama wetu. Ikiwa leo hii mtoto wangu wa mwisho Manahali mwenye mwaka mmoja anadaiwa shilingi laki tano na ushee kutokana na deni hili la trilioni 23.7...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa hiyo ni kengele ya pili. Naomba nimwite Mheshimiwa Sylvester Mabumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Khatibu Said Haji pia ajiandae.

**MHE: SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini

pia nikupongeze kwa ubunifu ambao umeuleta katika kujadili bajeti ukianzia na bajeti ndogo na sasa bajeti kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kuzoa viti vingi sana nya Udiwani. Huu ni ushindi wa kimbunga kwamba katika viti 22 tumepeata viti 16. Pongezi kubwa kwa Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye hotuba hii. Taifa letu linatekeleza Mpango wa MKUKUTA II wa kuondoa umaskini Tanzania, lakini lengo la MKUKUTA ni kuhakikisha Watanzania hawa wanaondokana na umaskini ifikapo mwaka wa 2025.

Mheshimiwa Spika, hofu yangu ni kwamba, benki hizi ambazo zinakopesha wananchi hapa Tanzania bado zinatoza riba kubwa sana ambazo haziwezi kutusaidia kuondokana na umaskini. Mkopaji anapaswa aliye riba ya asilimia 15 mpaka 18, lakini ye ye akiwekeza fedha zake kwenye benki anapata faida ya asilimia nne au tano. Sasa kwa namna hii benki zinawaibia Watanzania, zinafanya ujambazi mkubwa sana. Naiomba Wizara ya Fedha na Serikali yetu izielekeze benki kushusha riba ili kweli kama tunataka tufikie malengo ya MKUKUTA tuweze kuona manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, nataka nizungumzie pia hotuba ya Waziri anapoelezea nia ya kutoza kodi kwa ile Sheria ya Fedha Na. 147. Hivi karibuni Waheshimiwa Wabunge tulikuwa na semina hapa ya kampuni ya vinywaji, *Tanzania Distillers Company Limited*.

Mheshimiwa Spika, wameeleza mbele yetu kwamba, wao wanalipa kodi Serikalini, ukiziangalia kodi za aina zote zinazofikia kwa mwezi shilingi bilioni 6.9 ambazo ni karibu shilingi bilioni saba (7). Hata hivyo Serikali yetu haizilindi kampuni hizi kwani zinapata changamoto sana. Kwa mfano, kampuni hizi zinapopeleka bidhaa zao nchi jirani ya Kenya, kule wanakumbana na vikwazo nya jinsi ya kupata soko.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa Serikali yetu ilinde kampuni hizi kwani kama kampuni inalipa takribani shilingi bilioni saba (7) kwa mwezi, ni kwa nini Serikali inashindwa kulinda kampuni kama hizi ili ziweze kuendelea kuchangia zaidi pengine ya shilingi bilioni saba (7)?

Mheshimiwa Spika, wanaeleza kwamba wanapopeleka bidhaa kule Kenya, kule Serikali imeweka utaratibu inawaambia sijui chupa za ujazo wa mililita 205 hazitakiwi wakati Watanzania ndizo ambazo wanatengeneza, lakini bidhaa za Kenya zina soko Tanzania. Sasa kwa nini bidhaa kama hizo kutoka nchi ya nje hapa kwetu hazizuiliwi ili kulinda kampuni zetu ziweze kuendelea kulipa kodi nzuri?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, uliunda Tume ya kuishauri Serikali vyanzo vipyta vya mapato, cha ajabu ni kwamba kwenye pendekezo la Mheshimiwa Waziri amejikita kwenye maeneo yale yale, kuongeza ushuru kwenye mafuta, vinywaji, sigara, ambavyo ni *traditional*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini Mheshimiwa Waziri anataka kuumiza watu wetu? Unapoongeza kodi kwenye mafuta hata ile anayosema kwamba mfumuko wa bei utashuka, hauwezi kushuka kwa sababu kuna kitu kinaitwa *cost pool inflation* ambayo inalazimishwa kutokana na ghamama za usafiri. Unapandisha kodi ya dizeli, *petrol/halafu unasema unataka kuwa na inflation ya single digit* ya asilimia sita (6%) unaipata wapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nadhani Serikali ikae chini ishirikiane na Kamati yako, mapendekezo ambayo yaliangaliwa na Tume yako uliyoiunda, basi Serikali iyatumie. Haiwezekani kila siku kodi iongezwe kwenye mambo yale yale ya vinywaji na nini, Watanzania wakiokoka inakuwaje? Utapata kodi wapi? Siku zote tunaambiwa sigara zina madhara katika afya zetu, je wakiacha kuvuta sigara Taifa litakwenda kweli? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali sasa ikae na ofisi yako ya Bunge, iangalie na iweze kuangalia vyanzo vingine na siyo hivi ya kila siku ambavyo ni *traditional*.

Mheshimiwa Spika, vile vile kila anayesimama hapa anaisifu *TRA*, mimi nataka kutofautiana kidogo, *TRA* wanachezea akili zetu, tunasema wanakusanya mapato kupindukia, siyo kweli. Leo hii baadhi ya maafisa walio wengi ndiyo wanawasha hasira kwa Watanzania kuichukia CCM, baada ya mwaka mmoja au miwili unamkuta amelimbikiza mali nydingi sana. Amepata wapi na ana mshahara upi? Naomba Tume iundwe kuwachunguza wote ambaao wana mali nydingi watwambie wamezipataje? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna maafisa wengi sana wa *TRA* ambaao siyo waadilifu. Halafu sielewi, *TRA* toka ilipoundwa, watu wameanza kazi pale mpaka hii leo wanazeeka *as if* hakuna sehemu nydingine ya kuwapeleka. Kwa nini Serikali haiwahamishi hawa? Haiwezekani ikawa wewe kwa kuwa ndiyo umesomea mambo ya *finance* ukae pale *TRA* siku zote. Hapana! Naomba Serikali iliangular hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hawa wanakiwashia chama chetu hasira dhidi ya wananchi kwa sababu wamejilimbikizia mali nydingi sana. Harufu ya umaskini hawaijui hawa. Mtanzania hata mkate wa shilingi 100 anashindwa kuununua, lakini unamkuta mtu anasema kwanza ye ye hawezi kula mkate bila siagi, ni jeuri gani hiyo?

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu deni la Taifa. Kwanza niipongeze Serikali yetu kwa kujenga imani na matumaini makubwa kwa nchi wahisani na mashirika yanayotusaidia. Ombi langu hapo ni kwamba, misaada hii tunayoipata basi itumike kutatua kero halisi za Watanzania hasa katika sekta ya elimu, maji, miundombinu ya reli, barabara na bandari.

Mheshimiwa Spika, kama tunapata misaada na mikopo hii. Mikopo hii lazima itumike kwa tija, misaada hii lazima iwe na tija, Tanzania leo hii kusini mwa jangwa la

Sahara ndiyo nchi inayopokea misaada mingi sana ukilinganisha na nchi majirani, lakini ndiyo iliyokuwa nyuma kimaendeleo kwa nini?

Mheshimiwa Spika, madeni haya tunayoyapata yawe na tija hata kama yatakuwa ni makubwa kiasi gani? Tunapowaonesha nini tumetumia misaada na mikopo hiyo, basi naamini wananchi hawatakuwa na maswali wala hofu na namna Serikali yetu inavyotenda. Lakini kama misaada na mikopo tunayoipata haina tija, huwezi kuona utekelezaji wake, basi nina hakika tutakuwa na kazi sana mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, nataka pia nizungumze kuhusu makusanyo ya mapato yasiyokuwa ya kodi, ukusanyaji wake hauridhishi. Ametwambia ali-target kukusanya bilioni 644.6, lakini mwisho mpaka alipotoa taarifa hili aliweza kukusanya bilioni 357 ambayo ni chini ya lengo lao. Sababu alizozieleza hapa ni kwamba, uwezo wa mdogo wa kukusanya kodi, sijui vifaa duni, baadhi ya mashirika na wakala hawachangii sawasawa. Sasa analiambia Bunge ili limsaidie kufanya kazi hizi?

Mheshimiwa Spika, nadhani yeye alikuwa anapaswa kutuambia hapa kwamba, kwa sababu wamekusanya kidogo, Serikali imejipanga kufanya hivi, kuwashughulikia ipasavyo hawa ambao wamesababisha isifikie lengo lake. Kwa sababu sisi si kazi yetu hapa Wabunge kwenda kujenga uwezo wa wataalam kukusanya mapato haya yasiyokuwa ya kodi. Lakini pia si kazi ya Wabunge kutoa vifaa ili kujenga mifumo imara, ni kazi ya Serikali. Atwambie amejipanga viyi kufanya mambo hayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini anapotwambia amekusanya kidogo kwa sababu imekuwa hivi, mimi kidogo, mtani wangu namheshimu sana, basi wasaidizi wake wamsaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwamba, wanapandisha kodi ya

magari yanayozidi miaka kumi na huku tunaamini kwamba Tanzania ni nchi maskini na hili jambo halina ubishi.

Mheshimiwa Spika, ni Watanzania wangapi wataweza ku-afford magari mapya? Naomba Serikali ifikirie upya jambo hili jamanii! Humu Wabunge tumepewaa pesa, tulio wengi tulinunua magari *used*, hakuna Mbunge aliyenunua gari ya kiwandani na gari leo hii siyo anasa. Naishauri Serikali yangu ifikirie sana uamuzi huu kwa sababu hatutaweza kumudu.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE: SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba na Mheshimiwa John Paul Lwanji ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na pia kwa dhamira ya dhati kabisa nikupongeze kwa kuunda Kamati ya Bajeti kwa sababu itachangia kuhakikisha Bunge linakuwa imara na kuisimamia Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia usipoweza kushukuru kwa kidogo, huteweza kushukuru hata ukipewa kikubwa. Mimi kama Mbunge wa Vijana naishukuru Serikali kwa kutenga bilioni tatu kuweka katika Mfuko wa Vijana. Wabunge vijana kilikuwa ni kilio chetu, huu mwaka wa tatu mfululizo kwa sababu Mfuko wa Vijana ulikuwa haupewi fedha za kutosha. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini niweke angalizo tu, kutenga fedha ni jambo lingine na usimamizi wa fedha na kuhakikisha zinawafikia walengwa ni jambo lingine. Sasa niiombe Serikali yangu, isipokuwa makini, tutazijutia fedha hizi kupotea kama

ambavyo zilipotea fedha za mabilioni ya JK kwa kutokwenda kwa walengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa Mifuko hii ya Vijana tunajua kabisa itakwenda kusimamiwa kwenye *leve/ya* Halmashauri na kwenye Halmashauri kumekuwa na urasimu mkubwa sana. Watu wengine wanawaweka huko watoto wa wajomba zao na wa shangazi zao ambao hawana utaalami wowote na ambao hawana biashara zozote na kuwapa hizo fedha na mwisho wa siku fedha hazirudi, hazizunguki na wala haziwasaaidii vijana wengi. Kwa hiyo, ninachokiomba kuwe na usimamizi wa kutosha katika fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kuzungumzia suala nzima la ongezeko la tozo ya petrol. Nilichangia kwenye Wizara ya Uchukuzi, nikazungumzia ongezeko la nauli na nikatetea sana kwamba nauli inapoongezeka wanaoumia ni wananchi wa kawaida. Leo tunakwenda kuungeza tozo ya petroli, Mheshimiwa Jenista Mhagama amezungumzia pale. Watakaoendelea kuumia ni wananchi hawa wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, wamiliki wa vyombo vyaya usafiri wataongeza tena nauli. Kwa hiyo, hapa tunazalisha ongezeko tena lingine la nauli na kuwaongezea mzigo Watanzania ambao wengi wao wanashindwa kumudu hata milo mitatu kwa siku. Sasa nalomba Serikali iangalile vizuri suala hili.

Mheshimiwa Spika, hali ni ngumu ya maisha tunazungumzia hapa sijui uchumi umepanda, tunazungumzia ongezeko la uchumi, lakini tukiangalia asilia uchumi wa Mtanzania mmoja mmoja bado ni duni, bado Watanzania ni maskini na hasa wanaoishi vijijini. Leo hii tunakwenda kuwaongezea mzigo kwa kupandisha tozo ya *petrol*, kwa kweli hatuatendei haki Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini niipongeze Serikali kwa kuondoa kodi ya bodaboda, lakini naomba waliangalie kwa kina kwa sababu vijana wengi, vijana wenzangu hawamiliki

hizi bodaboda wala hizi pikipiki. Mwisho wa siku anayekwenda kufaidi ni mmiliki na wala siyo mwendeshaji.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kuishauri Serikali iangalie kwa kina, kuboresha suala hili ili wale vijana wenyewe waweze kunufaika na kuondolewa kwa hii tozo ya bodaboda. (*Makofj*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia wenzangu wamezungumzia suala nzima la magari na mimi naungana nao. Ni kweli kwamba, siyo Watanzania wote wana uwezo wa kununua magari mapya. Hapa tunazungumzia Watanzania hawa ambaao ni wafanyakazi wanaopata mishahara midogo, anadunduliza kipato chake, anajinyima, aweze kupata usafiri utakaomwezesha kuwahi ofisini, leo hii tunaweka kikwazo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia hapa na mimi nikiwa mmojawapo sikuwa na uwezo wa kununua gari jipya mbali na kupata mkopo. Hatuwatendei haki wafanyakazi ambaao na wenyewe wanataka kutoka kwenye kutembea kwa mguu waweze kumiliki magari, hawatakuwa na uwezo wa kununua gari jipya.

Mheshimiwa Spika, tunaona urasimu uliokuwepo bandarini pale, lakini tunaendelea kuwaongeza mzigo wafanyakazi, huku tunawapunguzia kodi na huku tunaendelea kuwaongeza kodi kwa mgongo mwingine. Naomba Serikali pia iliangalie hiki kwa kina.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kuongeza bajeti trillioni 18, sina tatizo nalo. Pia niipongeze kwa kuongeza fedha kwenye baadhi ya Wizara. Lakini naiomba sana Serikali, kuongeza fedha ni jambo lingine na kuhakikisha fedha hizi zinakwenda katika miradi na lenyewe ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi tuliongeza fedha katika Wizara ya Uchukuzi, lakini Wabunge watakubaliana na mimi je, hizo fedha zilitoka? Mwaka jana tuliongeza fedha

kwenye bajeti ya umeme, lakini hizo fedha hazikutoka. Sasa si vyema Wabunge tukaendelea kuimba wimbo ule ule kila mwaka, tukapewa majibu yale yale na utekelezaji ule ule, hatutakuwa tunawatendea haki Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na fedha za maendeleo kutegemea wahisani na Mheshimiwa Chenge alisema kama kuna wahisani ambao tunaona wanatu-*let down* tuangalie vyanzo vingine, tuangalie wadau wengine wa maendeleo. Wengine hao wanataka kutumia mgongo huu wa kuahidi kutupa hela, lakini hawatupi na kuhakikisha mambo hayaendi, mwisho Serikali yetu iendelee kuchukiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali kama kila siku tunategemea watu ambao hawatupi fedha kwa muda unaotakiwa, tuanze sasa na sisi kama Taifa kuona uwezekano wa asilimia 80 ya bajeti ya nchi itokane na vyanzo vyetu wenyewe. Hili linawezekana kama tutahakikisha tunaminya mianya ya watu kukwepa kodi. Majirani zetu wa Kenya leo hii asilimia 80 ya bajeti yao ni fedha zao za ndani. Siyo wahisani wote wanatupenda na wengine kama mnavyojua hawapendi kuendelea kuona Tanzania hii yenye neema inaendelea kuwa na amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Serikali yangu iangalie suala hili kwa kina. Mambo ya kuwa tunaendelea kutenga fedha, halafu tunapata majibu yale yale, ooh, wahisani hawaajaleta, sisi Wabunge humu ndani tumechoka. Kusanyeni kodi, zibenii mianya ya rushwa, tuhakikishe tunaongeza mapato na tuwe na uwezo wa kuhakikisha bajeti tunayotenga, tunaitenga kwa fedha zetu wenyewe za ndani.

Mheshimiwa Spika, siyo kila siku tunataja *figure* trilioni 18, kumi na ngapi, fedha za nje kiasi Fulani, halafu haziji, hatulitendei haki Taifa hili. Uwezo wa kukusanya mapato tunao. Wale wote ambao wanakwepa kodi wafikishwe kwenye vyombo vyanya na tuminye mianya yote ambayo inatoa mianya ya watu kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze mradi wa maji wa Bunda. Leo hii ukienda hospitali ya *DDH* utakutana na akinamama wodini wana maji kwenye ndoo za lita 20 na 10, hospitali! Mradi huu umeanza muda mrefu na kutokamilika kwa mradi huu kunawachonganisha Wabunge na wananchi. Wananchi wa Bunda wamechoka kunywa maji machafu na wenyewe ni Watanzania, wanahitaji maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, hapa nilisema pia, kuna baadhi ya Wakandarasi hawazitendei haki *tender* ambazo wanapewa na mpaka tunashangaa kwa nini wanaendelea kupewa. Mkandarasi anakwenda *site* baada ya kuona viongozi wa kisiasa, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, sasa tujue wanapewa pesa au hawapewi au wanashindwa kutimiza majukumu yao. Tunaomba sana, wananchi wa Bunda wanaomba mradi wa maji ule ukamilike. Tuliambiwa ungekamilika mwaka jana mwezi Julai, lakini mpaka leo hata asilimia 30 ya mradi haujakamilika. Imechimbwa mitaro mpaka imetitia tena. Mabomba yanarundikwa kule wakisikia labda Mbunge anakwenda au Waziri anakwenda, lakini hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, tunaomba mradi wa maji ukamilike haraka, *operation* zinakwama kwa kukosa maji, akinamama wanakwenda hospitali wakiwa wamebeba maji kwa sababu hospitalini hakuna huduma ya maji, wananchi wa Bunda wamechoka wanataka maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Khatib Said Haji na Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Paul Lwanji na Mheshimiwa Riziki Omar Juma wajiandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante nami kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja mionganoni mwa wanaochangia hotuba hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, nami naomba nianze kwa kutoa pongezi kubwa sana kwa Chama cha Wananchi (*CUF*) kushinda uchaguzi wa Jimbo la Chambani, Pemba na kuwashinda CCM na washirika wao akiwemo *ADC*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia mimi siyo mchoyo, nawapongeza CCM kwa ushindi wa viti vyta Udiwani ambavyo wameendelea kuchukua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Chama changu cha wananchi (*CUF*) kiliniteua kuwa mshiriki wa uchaguzi wa Udiwani katika Kata ya Handeni ambako tuligalagazwa na CCM katika uchaguzi ule.

Mheshimiwa Spika, lakini nimejifunza jambo kwamba, si lazima ushinde hata ukishindwa Mpinzani makini hutoa mkono kwa ahsante kwa aliyekushinda. Lakini katika moja nililojifunza kule Muheza ilipofika saa sita mchana, nilikutana na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Tarime Nyambari Chacha Nyangwine akaniambia kwa kheri, naondoka zangu. Nikamwuliza unakwenda wapi na uchaguzi unaendelea. Akaniambia CCM tumeshashinda, tayari tumeshinda Mheshimiwa Mbunge, mimi nafunga machungwa, naondoka Muheza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichojifunza pale ni kwamba, tutaiangalia hii teknolojia mnayoitumia wenzenzu wa CCM ya kuweza kujua mmeshinda kabla hata uchaguzi haujamalizika.

**SPIKA:** Wewe hujui Maji Marefu yupo kule! (*Kicheko*)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Sasa nianze mchango wangu kwa kusema kwamba, nimeridhika sana na usikivu angalau ambao umeanza kuoneshwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika maeneo haya nitakayoyataja. Nimeridhika kwa kuondoa kodi ya bodaboda kwa vijana wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali leo kwa

kusikiliza kilio cha Wabunge cha kuondoa mtindo wa *direct release* katika bandari zetu. Jambo hili katika bajeti ya Wizara ya Fedha mwaka uliopita akiwa Waziri Mkulo nililisema hapa, Serikali inapoteza mabilioni ya shilingi kwa kuruhusu mtindo wa kuamini wafanyabiashara wakubwa kwa mtindo wa kutoa mizigo bila kukaguliwa bandarini.

Mheshimiwa Spika, nililisema hili nikijua, kwa sababu Mheshimiwa Waziri anakaa karibu sana na Rais, lakini sisi tunakaa karibu sana na wananchi. Tunajua wananchi wanazungumza nini na tulijua kuna matatizo gani kuruhusu kuendelea kutumika kwa mtindo ule wa *direct release*. Lakini mwaka jana yalipuuzwa kwa sababu labda waliokuwa wakitetea jambo lile tulionekana ni Wapinzani.

Mheshimiwa Spika, naomba wenzetu, wakati tunapoleta mawazo yetu ya maana ya kusaidia nchi hili katika ukusanyaji hasa wa kodi wayasikilize na wayatekeleze. Wapinzani wapuuizi, wapuuzeni, lakini Wapinzani makini wasikilizeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili lingesikilizwa mwaka jana, leo tungeokoa mabilioni ya shilingi za Watanzania ambazo zilikuwa zikipotea kwa mtindo huu *direct release*. Tunaposema, nasema tena, tunaposema msichukulie kila Mpinzani analosema halina maana, angalieni na mwangalie kwa uzito muone mambo yenye maana myachukue.

Mheshimiwa Spika, alikuwepo mwimbaji mmoja maarufu, muasisi wa Taarabu kule Zanzibar sasa hivi ni marehemu, alikuwa anaitwa Siti binti Saad, huyu mama alikuwa mbaya wa sura sana, lakini alikuwa na sauti nzuri ajabu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika kumponda wapinzani wake waliwahi kumtolea mashairi yaliyosema hivi. Nataka wewe uyasikilize, ni mazuri, walimwambia; Siti binti Saad umekuwa mtu lini, ultoka kwenu na kaniki mbili chini, kama siyo hiyo sauti wewe ungekula nini? Siti binti Sad aliwajibu; si hoja

uzuri wa sura jamali, utukufu wa kabilia na wingi wa mali, hasara ya mtu kukosa akili. Kwa hiyo, wanayoyasema wenye akili yafuateni na myazingatie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa hilo na naamini hakuna haja ya kuwapandishia Watanzania kodi ya mafuta kwa sababu pato litakalopatikana kwa ukwepaji mkubwa wa kodi ulitokana na njia hii, unatosha kufidia pengo hilo. Mabilioni ya shilingi yaliyokuwa yanakwepwa na matajiri wakubwa kwa mtindo huo wa utoaji wa mizigo inatosha kufidia pengo hilo.

Mheshimiwa Spika, hakuna haja ya kuongezea kodi ya mafuta wala kodi ya simu kwa watumiaji wa kawaida, hiyo fedha itafidiwa na hapo. Msituulize hapa, hata huyo kipofu ukimkabidhi mkia wa paka hakuulizi makalio yake yako wapi? Atajua tu na ni kipofu. seuze wewe mwenye macho, unauliza makalio ya paka yako wapi wakati mkia umeushika, kodi ipo haijakusanywa. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme na si hapo tu, kuna kilio kikubwa sana cha wananchi wetu hasa wa vijiji, wanatozwa kodi ya mkaa gunia moja sh. 8,000, gunia analokwenda kuliiza mjini sh. 25,000 anatozwa sh. 8,000. Ukipiga hesabu mwananchi huyo kama atapeleka magunia 30 kwa mwezi, analipa kodi 480,000/= akienda kwa mwaka ni milioni 5,700,000/=. Mwenye lori lile hafikii kulipia Serikali kodi hiyo analipa mtu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, leo mzee wangu ametoka kule Tanga Vyera, Monga, Kichalikani anapofika na gunia lake la mkaa analipishwa fedha hiyo. Kwa kweli tunawanyonya na tunawaumiza wananchi wetu. Tuangalieni hizo kodi zinazokandamiza watu wetu, mtu anayeilipa Serikali 5,700,000/= hata akiumwa anapokwenda hospitali anaambiwa anunue hata kidonge cha *panadol*, hii siyo haki, tuangalieni.

Mheshimiwa Spika, nitakwenda moja kwa moja kwenye kero za Muungano. Nampongeza Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, jana aligusia suala la kero za Muungano. Kumekuwa na vikao vya Waziri Mkuu na Makamu wa Rais wa Zanzibar kila mwaka kujadili kero za Muungano na moja kati ya kero hiyo na napenda kuisema sana ni Watanzania kutoka Visiwani, wanapoingia na magari yao kwa ajili ya matumizi yao Tanzania Bara. Kumekuwa na usumbufu na hali isiyokuwa ya kawaida na hili ukilizungumza unaambwiwa limo katika kero ya Muungano. Sisi hatutaki methali hii ya kero ya Muungano, inayowaumiza Wananchi, hicho siyo kitu cha kujivunia. Wenzetu wamesema na sisi tunasema, hapa nina fomu hii ya *TRA* ambayo imebatizwa jina la *C32 (Custom Regulation 136 Section Two)*, ambayo hii inawaruhusu watu wote wanaotoka katika *East and Central Africa*, nchi za *COMESA*, zote kuingia na magari yao hapa wakatumia kwa mtindo na kuna sehemu tu hapa unapigwiwa muhuri wa kuingia na muhuri wa kutoka pasipo na vikwazo vyovyote.

Kwa Zanzibar au kwa Watanzania wanaotoka Zanzibar, haliwi hilo na nimekuwa nikifuatilia jambo hili, mara ya mwisho nimeletewa jibu hili. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, niliuliza swali hili katika moja ya vikao na Kamishna wa *TRA*, akasema jambo hilo hajui kama liko kama Mzanzibari anapoingia na gari lake pale Dar es Salaam kutaka kutumia mwenyewe anakutana na kikwazo hicho. Nataka nisome leo jibu ambalo nimeletewa *officially* na Watanzania waliskie, mwone namna gani ambavyo yanatumika mambo mengine katika kuzorotesha hata huo Muungano wenyewe na kwa hili kama tunafikia hapa, basi hakuna ubaya watu kuchukia Muungano, kwa sababu kero za Muungano zimezidi.

Mheshimiwa Spika, jibu nililoletewa ni hili linasema: "Mtu yejote anayetoka nje ya Tanzania kwa ajili ya kufanya makazi ya muda ndani ya nchi wakiwemo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, *SADC*, anaruhusiwa kuingiza gari kwa ajili ya matumizi yake wakati akiwa nchini kwa masharti yafuatayo: Anatakiwa kulipa ada ya Dola 20 za Kimarekani na kutumia gari hilo kwenye barabara za Tanzania. Niruke

19 JUNI, 2013

kwa sababu ni mengi, lakini naenda kwa mtu anayetoka Zanzibar sasa. Mtu anayeingiza gari lake kutoka Zanzibar hatakiwi kuacha taarifa zilizotajwa hapo juu, badala yake mtu huyo anaagiza gari ambalo lina namba ya usajili wa Zanzibar kuweka dhamana benki au fedha taslimu ambazo ni sawa na tofauti ya kiasi ambacho atatakiwa aliye."

Mheshimiwa Spika, hii *paragraph* ni ndefu lakini kifungu cha mwisho kinasema: "Hata hivyo, suala la kuwezesha magari yaliyosajiliwa Zanzibar kuweza kutumika Bara, lipo katika orodha ya kero za Muungano na linatafutiwa ufumbuzi wa kudumu. Toka sijafika kwenye Bunge hili, miaka 20 kero hii inatafutiwa ufumbuzi! Hii ni fedheha, kumchukua Waziri Mkuu wa Nchi, Makamu wa Rais wa Zanzibar, wakakaa kujadili eti suala dogo la kero kwa sababu ya gari kutoka Zanzibar kutumika Bara. Sisi ni Watanzania, leo hili kila Mtanzania anadaiwa shillingi 500,000 hapa hawapo Warundi wala Wanyarwanda; kwa nini?

**SPIKA:** Kengele ya pili hii. Hiyo *document* uliyosoma inatoka wapi?

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Inatoka kwa Wizara ya Fedha, majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

**SPIKA:** Inatoka ndani?

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Haitoki hapa ndani inatoka huko kwenye Kamati yangu?

**SPIKA:** Sawa ni Bunge hilo. Haya ahsante nadhani wamesikia. Mheshimiwa Saleh Pamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Lwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Barwany ajiandae na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, napenda

nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Fedha, Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kutuletea bajeti hii ambayo inatupa mwelekeo wa kule ambako tunaelekeea.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka kulizungumzia, nataka nikupongeze wewe binafsi, umeacha *legacy* kubwa sana kwa kuleta utaratibu huu wa *Budget Cycle* mpya. Haipo katika maeneo yetu, sisi na Uganda na Rwanda ndiyo ambao tunayo *Budget Cycle* ya aina hii.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto, lazima tukubali kwamba, katika jambo jipya lolote unaloliletu, lazima litakuwa na changamoto. Tunaiomba Serikali kwa yale ambayo yamejitokeza katika kipindi hiki, ambayo ni changamoto katika utayarishaji wa bajeti, wachukue kama changamoto za kuweza kuzifanyia kazi. Hakuna jambo jipya ambalo litaanza bila ya kuwa na changamoto mbalimbali, lakini nakupongeza sana, umefanya kazi nzuri sana kwa nchi yetu na jina lako litabaki katika historia; hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, kwa hiyo, lazima ni-*declare interest* kwamba, niko katika Kamati ile. Napenda pia nikupongeze sana kwa kuanzisha Kamati hii ya *Budget Scrutiny*, kwa sababu inasaidiana na Serikali. Kamati hii imekuwepo katika kuiongoza Serikali kwenye maeneo ambayo imeshindwa kuyaona. Kamati ya Bajeti imefanikiwa sana katika kuongeza bajeti ya karibu shilingi bilioni 513. Fedha za maji shilingi bilioni 184.5 hazikuwepo, fedha za umeme shilingi bilioni 153 hazikuwepo, fedha za mabehewa hazikuwepo, lakini katika ushirikiano uliokuwepo kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali, kwa kukaa pamoja kwa sababu wote tunafanya kazi moja, fedha hizo zimepatikana na sasa nina uhakika kabisa fedha hizo zitawezwa kwenda kuwalettea Wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Pangani, tutapata Miradi mpya ya Maji katika maeneo ya Kigurusimba, Mikocheni, Mzambarauni, Masaika, Stahaku,

acha miradi mingine ambayo inaendelea. Tutapata mradi mkubwa wa umeme wa karibu shilingi milioni 800 kutokana na fedha hizi ambazo zimeongezwa. Napenda nichukue nafasi hii, kuishukuru sana Serikali kwa hatua hii ambayo wameichukua. Suala la kutenga bajeti ni moja, suala la kuwa na miradi ni suala mojawapo, lakini suala la usimamizi na utekelezaji wa miradi ni suala lingine. Ninaiomba Serikali kwamba, katika fedha hizi ambazo zimetengwa kwa ajili ya maendeleo na kwa ajili ya miradi mbalimbali ziletwe, zipelekwe na zilindwe. Kulindwa maana yake fedha za miradi ziwe *ring-fenced*, zisiende katika matumizi mengine ambayo yanajitokeza; hapo ndipo tutaweza kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, naomba niende haraka haraka kwenye Sera ya Mapato. Katika Sera ya Mapato na katika Bajeti ya Waziri wa Fedha, mara nyangi tumekuwa tukienda katika maeneo yaleyale; sigara, vinywaji, *juice*, vinywaji vikali, mvinyo na kadhalika na *pay as you earn*. Sasa lazima tufike mahali tuondokane na maeneo kama hayo. Lazima tuwe na miradi mikubwa, tuachane na kutoza kodi kwenye maeneo ambayo ni *traditional*. Sasa tunafanya nini? Kuna maeneo ambayo lazima tuyafanyie kazi na tuyawekee mkakati, maeneo ambayo tunaita *mega projects*, miradi mikubwa mikubwa ambayo *stimulate* uchumi. Kwa mfano, miradi inayohusiana na madini ya *uranium*, madini makubwa, madini ya viwandani kama *nickel*, madini kama Chuma cha Liganga na Mchuchuma, mambo kama gesi, maeneo ya mafuta haya ni maeneo ambayo Serikali lazima iweke mkakati maalum na iweke vivutio maalum ili kuweza kuhakikisha kwamba, maeneo haya yanachangia na yatachangia katika uchumi.

Nitatoa mfano, nchi ya Mozambique ilikuwa na matatizo lakini waliamua kuingia katika mradi mmoja mkubwa kabisa na Kampuni ya Japani inaitwa Mitsubishi. Waliamua wakajenga kiwanda cha kuyeyusha *aluminium*. Huu ni mradi mkubwa, ndiyo miradi ambayo tunaita *mega projects*, miradi ambayo inafufua uchumi kwa haraka. Huu mradi unaitwa *Mozambique Aluminium*, ulipojengwa mwaka 2000 pale Msumbiji matokeo yake yalikuwa nini?

Matokeo yake ni kwamba, walitoa ajira ya watu 3,000 mara moja. Waliweza kutumia umeme megawati zaidi ya 50 pale Kiwandani na vilevile Pato la Taifa la Mozambique, uchumi wa Mozambique ulikua kwa asilimia tano mara moja. Kwa hiyo, haya ni maeneo ambayo lazima Serikali yetu iyafanyie kazi. Maeneo ya viwanda vikubwa, maeneo ya viwanda mkakati, hayo naiomba Serikali na nimeona miradi mingi iliyomo humu nayo inatuelekeza huko; kwa upande wa Serikali nasema hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie suala la Miradi ya *Public Private Sector (PPP)*. Miradi hii tusikae nayo kwenye madawati. Fedha zipo nje, kwa hiyo, lazima twende nje kutafuta fedha za kusukuma Miradi ya *PPP*. Twende Uchina, Marekani, Ulaya, twende na Marekani ya Kusini ili tuweze kuhakikisha Miradi hii yote nayo inapata wawekezaji, tusikae nayo peke yetu kwa sababu huko ndiko ambako kuna fedha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka nizungumzie masuala mawili muhimu sana. Suala la kwanza ni la nidhamu ya matumizi. Serikali tutapitisha bajeti ya shilingi trilioni 18.2. Serikali inayo madaraka ya kubadilisha vifungu hapa na pale, lakini ndani ya Serikali wana utaratibu wa kusema kwamba, wanayo *Action Plan*. Kwa hiyo, *as long as* wao hawatabadilisha, ile *figure* haitabadilika, wanaweza wakatumia fedha hizo. Tunacholomba Serikali ni kwamba, lazima waufuate ule mkakati wao wa *Action Plan*. Kwa sababu ukizitoa fedha katika fungu moja ukazitumia zikazidi, maana yake ni kwamba, maeneo mengine yaliyoko katika Mpango Mkakati wako hayatafanyiwa kazi. Kwa hiyo, tunahitaji nidhamu ya matumizi kuhakikisha kwamba, fedha zinatumika katika maeneo yale tu ambayo yamepangwa, maeneo mengine ambayo hayajapangwa, basi fedha hizo zisubiri bajeti nytingine.

Pamoja na kwamba, Waziri wa Fedha anayo madaraka ndani ya vifungu vyake vyaa bajeti kwa kuyabadilisha hapa na pale, lakini tunafikiri kwamba, mahali ambapo tunatakiwa tuendeleee, lazima tuhakikishe

tunakuwa na *discipline*, tunakuwa na *financial discipline* kuhakikisha kwamba, fedha iliyopangwa ndiyo ileile inayotumika hata ndani ya kifungu hicho hicho haizidi na hapo ndipo ambapo tutaweza kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizingumzia ambalo nalionna ni la msingi kabisa na hotuba zote mbili zimelizingumzia, Hotuba ya Waziri wa Fedha pamoja na Hotuba ya Waziri wa Mipango, ambalo sijaona mkakati wa Serikali wa kuweza kulitekeleza. Haya yote tunayozungumzia ...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naona kengele ya pili.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, asilimia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma na Mheshimiwa Devotha Likokola ajiandae.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bajeti hii. Nachukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuwasilisha bajeti nzuri na yenye mwelekeo. Wakati anahitimisha labda nimnukuu alisema: "Mheshimiwa Spika, yote niliyoyasema yanawezekana iwapo kila mmoja wetu na Wananchi kwa ujumla, tutatimiza wajibu wetu kila mmoja kwa nafasi yake kwa kushiriki na kuwajibika kikamilifu katika kutekeleza sera na mipango tuliojiwekea."

Mheshimiwa Spika, maneno haya ni muhimu na ni mazito na sisi kwa upande wetu Wabunge, nadhani tumeshiriki na tumetoa michango yetu toka mwezi wa Machi kwenye Kamati, tumeuja hapa miezi yote hii tumekaa hapa nadhani tumetoa michango ambayo itaisaidia Serikali kusimamia mapato hayo

yatakayokusanya na matumizi yake. Tuna tatizo hilo la uwajibikaji, lakini sisi tunamrudishia tena Waziri asimamie nyumba yake hiyo, hayo mapato yatakapopatikana yaweze kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, tatizo tunalo nchi hii la rushwa, kitu kidogo, vitu kama hivi na tatizo hili limekithiri miaka nenda rudi. Fedha zinakusanya lakini katika matumizi, *CAG* na vyombo vingine vinatoa taarifa mbaya kwamba matumizi hayasimamiwi vizuri. Sasa ningeliomba safari hii basi tufanye kweli, tusimamie fedha hizi za umma ziweze kutufanya kazi ambazo tumefanya.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Liberia, Mama Ellen Sirleaf Johnson, nadhani aliposhika madaraka alipofika tu mara ya kwanza aliangalia Wizara ya Fedha, alikuta uozo. Kitu alichokifanya, aliwaondoa wote pale, akakodisha watu kutoka nje wakashika hiyo Wizara ili Serikali iweze kuwa na mapato ya kutosha pamoja na nidhamu ya matumizi, alifanya hivyo. Sasa miaka ijayo, nafikiri haya ni mawazo yangu, tusione aibu basi kwa sababu tutakuwa tumeshindwa tusione aibu ya kuweza ku-*outsource* au tupate wataalamu katika Wizara hii kutoka nje ili waweze kusimamia maana sisi hatuwezi. Utaratibu huu inavyoonekana kwa sisi ndugu, jamaa, marafiki na nini, tunaoneana aibu. Mheshimiwa Keissy hapa alisema kwamba, wanyongwe, hata tukiwanyonga haiwezekani shughuli itakwenda hivyo. Mimi naona suala hapa ni la utaalamu, ni la usimamizi wa kina kuhakikisha kwamba, fedha za umma zinatumika kama zilivyolengwa na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Marehemu Meresi Zenawi, aliyekuwa Rais wa Ethiopia; Nchi ya Ethiopia inategemea sana pilipili kama zao kuu la biashara, linapeleka nchi za Kiarabu na nini, lakini mwaka mmoja walipata shida wafanyabiashara walihoji sana zao hili wakanunua kwa wingi wakahodhi wakaficha, sasa uchumi wa nchi ukawa unalegalega kwa sababu zao hili ni muhimu kwao, walichofanya, walifanya operesheni maalum kabisa.

Operesheni maalum ya makusudi, wakaingia katika maduka yao wakakuta wafanyabiashara kadhaa wengi wamehodhi zao hili. Kwa hiyo, alichofanya yule alikuwa ni Mwanajeshi, alituma maaskari wake wakaenda wakakamatwa wale watu waliokuwa wamehodhi na bidhaa zao zikawekwa nje pale, kilichofuata ziliwekwa nguzo kila nyumba kwa huyo mtu, akafungwa pale basi wakala shaba wote na nidhamu ilirudi. Sisi mambo hayo sidhani kama tunaweza tukayafanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kitu muhimu tunachoweza kufanya, tuone kama mama yule wa Liberia alivyofanya, kama Wizara ya Fedha haitengamai basi tuombe msaada watu hawa waje watusaidie twende na Wizara nyingine kama inaonekana pale pameimarika twende na Wizara nyingine, basi tuwaweke watu weupe hawa watusaidie, maana inaonekana bila ya hao watu weupe hatuwezi kuendelea mbele, hatuwezi kusonga mbele katika mipango yetu. Kwa hiyo, ninashauri kwamba, Wizara isimamie mapato hayo.

Mwaka jana tumeambiwa kwamba, fedha za wahisani nyingi hazikuletwa na ni kisingizio wanasema unajua fedha za kigeni hazikuja, lakini ukweli wenyewe ni kwamba, taarifa hatupeleki kwa wakati maana hizi fedha kila *quoter lazima ziwe na taarifa*. Tumeambiwa kwamba, baadhi ya maeneo taarifa hazikukamilika, sasa watatoaje fedha hawa watu kama taarifa hazikukamilika; hawawezi. Kama taarifa hakuna na hii imanzia kule juu katika taarifa hizi mpaka chini, mpaka hata kwenye Halmashauri na kwenye Serikali za Vijiji, taarifa za fedha na mapato hatusomi na hatupeleki kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa hizi fedha; kwa mfano, bajeti hii inasema kwamba, takribani shilingi trilioni nne tunatarajia kutoka kwa washirika wa maendeleo na wanaita *development partners*; sasa *development partners* hata mimi nashindwa kuelewa hili neon. Hivi huyo *development partner* atakuwa na uhusiano gani na mtu maskini?

Mheshimiwa Spika, sisi tukubali tu kuwa walete wahisani. Wahisani wanatusaidia, lakini kama hatufuati masharti yao tutafanyaje? Inabidi tufuate masharti waliyotuwekea ili waweze kutoa hela. Mimi nilikuwa ninashauri Kamati yako hii ya Bajeti ipewe fursa kwa makusudi kabisa ya kutembelea Mabunge ya hizo nchi za wahisani. Juzi ametusomea Waziri wa Fedha hapa kuwa ni nchi 19 zimetusaidia na taasisi tisa za Kimataifa. Kama pesa zinasuasua, Kamati ya Bajeti haiwezi ikaishurutisha Serikali kuwa nendeni mkawaulize au mkafanye hivi. Kamati hii ya Bajeti ipewe fursa ya kwenda kwenye Taasisi au Mabunge ya nchi zinazohusika za wahisani wazungumze na wenzao jamani kuna tatizo gani kwa nini fedha hizi haziji kwa wakati. Kama wataambiwa tatizo liko kwenu basi na huku nako wafuatilie.

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza kwa kuunda Kamati hiyo, imetuonesha njia hapa kwa muda mfupi. Utaratibu huo uendelee, ninadhani itumike vizuri waende sambamba na Wizara hii, lakini kila mmoja a-*play role* yake. Sasa kama Wajerumani walihidi; hivi kweli mmewekeana sahihi na kila kitu na ikatangazwa, mbona Japani pamoja na matatizo yao yote waliyoyapata ya mwaka 2011, lakini hawakusitisha misaada kwa sababu *they honor their contract*. Wajibu wao sasa kama zinasuasua basi hii Kamati ya Bajeti iruhusiwe itembelee hizo nchi, izungumze na wahisani kuwa nchi yenu imeweka mkataba na nchi yetu, lakini tunashindwa kuelewa ni kwa nini fedha haziji. Ninadhani hilo linaweza likatupa njia ya kuweza kupata hizi fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, niliomba Watendaji pamoja na kuwa wanahitajika kubanwa, lakini Serikali nayo ije na mkakati wa kuweza kuwalipa Watumishi wa Serikali vizuri, kulingana na hali ya maisha ilivyo, labda hii nayo itasaidia hawa watu wasiweze kuangalia mianya mingine ya kutuibia. Kama unampa mtu jukumu la kusimamia fedha za Wananchi au hela za Serikali halafu mshahara wake ni mdogo, lazima atatafuta njia zingine. Kwa hiyo, ninawaomba kwa makusudi kabisa kuwa, bajeti ijayo

tuangalie pamoja na kuwa tunaongeza kidogokidogo, lakini maeneo ambayo tunaona ni muhimu, basi waweze kupata malipo ya kutosha kwa ajili ya maisha yao na kwa ajili ya kuwaweka katika hali ya kuwafanya wasiwe na tamaa.

Vipaumbele sita vya Kitaifa vilivyowekwa ninaviona ni vingi, tupunguze tubaki na vipaumbele vitatu. Nchi ya Sweden, miaka ya 1950 ilijiwekea vipaumbele vitatu; elimu, halafu ikajiwekea *control* ...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante ya pili. Tukienda kuwaliza wale *Donors* sisi Bunge tutakuwa tunaingilia kazi ya *Executive*. Wabunge wa Bajeti watakwenda kujfunza katika nchi ambazo zimefanikiwa vizuri zaidi. Sisi hatutafanya kazi ya *Executive*, watafanya wenyewe. Mheshimiwa Riziki Omar Juma!

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa spika, ninaomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenijalia uwezo wa kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu, kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nachukua nafasi hii kukupongeza wewe, kwa kazi nzuri unayofanya katika Kiti chako hicho katika kusimamia Bunge hili. (*Makofii*)

Ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, pamoja na timu yake ya wataalamu, kwa kujitahidi kufanya kazi ambayo tumewatuma. Ninaomba niseme kuwa, bado wanahitaji kufanya kazi ya ziada kwa kutumia wataalamu wao ambao wanao ili tuweze kujikwamua hapa tulipo.

Ninaomba nianze na hoja ya utafiti. Utafiti katika bajeti hii umetengewa fedha ndogo sana. Nchi yoyote haiwezi kwenda bila kuwa na utafiti wa kina na ndiyo maana leo hii tunakuwa tukiongea humu ndani kila siku tunatafuta

wapi ambapo tumejikwaa, lakini hatupajui, kumbe hatufanyi utafiti wa kina ili kuweza kufikia malengo yetu ambayo tumejipangia. Nchi yoyote bila utafiti hatuwezi kufika mahala na ndiyo maana leo hii kilimo chetu kinaonekana kila siku ni kilimo ambacho hakina tija, kwa sababu watafiti hatuwezi kuwatatumia ipasavyo, kutokana na fedha ndogo ambayo tunawapangia. Nchi za wenzetu ukienda jinsi wanavyozalisha utashangaa, ukiliona pera linakuvutia, ukiona embe unatamani kula, ukiliona chungwa utalipenda.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na kwamba, wataalamu wao wanafanya utafiti wa kina na kuweza kufanya kilimo chao kwa utaalamu wa kutosha. Leo sisi wataalamu ninadhani tunao, lakini labda hatuwatumii ipasavyo, hatuna mbegu bora, hatuna mbolea bora na Wananchi haziwafikii kwa wakati. Kwa hiyo, tunafika mahala tunabakia tunagwaya hapahapa, kilimo chetu hakina tija na mwisho wa siku tunafikia mahala Wananchi wetu wanaomba omnia chakula, kwa sababu hakuna chakula cha kutosha. Kila siku tunaomba chakula cha njaa, ni tatizo, ni kutokana na suala la utafiti. Ninamwombwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aangalie kwa kina suala hili la kuwatengea fedha za kutosha sehemu ya utafiti ili tuweze kufanya utafiti wa kina, mambo mengi hatuwezi kuyafanya bila ya kuwa na utafiti wa kutosha. (*Makofii*)

Ninaomba niente kwenye suala la kipaumbele; kipaumbele ni jambo muhimu sana na la msingi na kama hatujaamua tuweke kiipaumbele gani hasa ili tuweze kufika, tutakuwa na shida nydingi sana kila siku. Tuna fedha nydingi, ukitazama bajeti iliyotengwa safari hii ni triliioni 18, kama fedha hizi tungeziweka katika mgao mahususi tukalenga kipaumbele gani hasa tunataka tukifanyie kazi, basi tunaweza kufanikiwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu. Kwa mfano, mwaka huu tungetenga fedha nydingi tukazipeleka kwenye elimu na kwenye afya, sehemu nydingine tukapeleka fedha kidogo; kwanza, tukubali kufunga mkanda, tukubali kujikita katika sehemu fulani tuweze kuzalisha vizuri, basi tusingekuwa na tatizo. Kwa

mfano, katika suala la elimu tuna tatizo la madawati, tuna tatizo la vifaa, tuna tatizo la maabara, tuna tatizo la vifaa vya maabara, walimu wanadai wana madeni yasiyokwisha, maandamano yasiyokwisha, hebu tujikite katika kitu fulani ili tujikwamuke hapa tulipo, mwaka ujao tufanye jambo lingine.

Unajua sisi Waislam, tukifunga Ramadhani tunapika muhogo, njugu, tambi, sijui mkate, sijui nini, mwisho wa siku vyote huwilii hivyo, kila mahali unatia mkono kidogo. Sasa na sisi bajeti yetu tunaitumia kama futari, hatuwezi kufika mahala, tuchukue fungu kubwa tulielekeze mahala. Wenzetu China mwaka 1964 waliamua wakasema kuwa Wachina wote wavae viatu, viwanda vikaagizwa, vikapewa uwezo, vikawezeshwa, suala la kuvalaa viatu likatekelezwa. Wachina wote wakapewa viatu wakavaa na wakapewa taaluma ya umuhimu wa kuvalaa viatu na sisi Watanzania tukiamua tukajikita kwa kusema jambo fulani lazima lifanywe, tutaweza kulifanya, tutaweza kabisa hebu tuamue.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kutia mkono kila mahala tukasema tutafika, hatufiki, tutajenga barabara kilomita moja, tutakwenda afya tumkomboe mzazi mmoja, tutakwenda elimu tulipe madeni walimu wawili wengine wanabaki, tutaendelea na mizozo na migogoro isiyokwisha. Tuchukue fungu tufanye jambo tuamue! Watanzania tuwaambie tunataka kujikita katika elimu, mengine yote kwanza tunaweka pembedni, tutaweka fedha kidogokidogo lakini sasa tunakwenda kwenye afya, ndani ya miaka mitatu tutakwamuka. Ninaamini tutakwamuka hapa tulipo tutaondoka. Tuna miti mingi ambayo imejaa, tuwaelimishe Watanzania wapande miti halafu miti ya mbao ile Halmashauri ipewe kibali wakate miti ile ya mbao tuchonge madawati, tuchonge viti, tuwape wanavijiji *tenderwafanye* hiyo kazi tueneze madawati shuleni, ili tuweze kupiga hatua hapa tulipo isiwe kila siku wanafunzi wetu wanakaa chini. Mtoto akirudi nyumbani suruali imechanika, anapinda magoti wakati wa kuandika, suruali imechanika magotini, imechanika matakoni, hatuwezi kwenda wakati miti ya

mbao tunayo, Wananchi wapo wa kuweza kufanya kazi, lakini uamuzi hatujaamua. Waheshimiwa tutie nia na tuamue, ninaomba tulifanyie kazi hilo.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la kuongeza ushuru kwenye sigara, vinywaji na soda; hili halitusaidii, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni Mchumi na timu aliyonayo ninadhani ni timu ya wataalamu mahususi, hebu tuijulize siku Watanzania wakisema hatuvuti, hatunywi pombe, hatunywi soda, tutatoa wapi hizi fedha zingine? Hatuwezi kutoa na mwisho magazeti huko siku nydingine yanatuambia soda zina sumu, tunatishwa tishwa, kwa hiyo, wengine wanaamua kugoma kunywa soda na wengi wanapata sukari wanajikita sasa hivi wanasema hapana hakuna kunywa soda tunakunywa maji tu. Kwa hiyo, itafika siku tutashindwa vipaumbele vyta kuongeza ushuru. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, kwa uwezo wako ulio nao, ukae na timu yako ya wataalamu, tutafute vyanzo vyta mapato vingine. Tuna madini ya kutosha, ninashangaa madini yanachukuliwa. Mimi nina nyumba yangu ninakaa unanitoa unaniambia ninatakugawia hapo barazani ukae; inawezekanaje?

Haiwezekani, tuna fedha za kutosha, Watanzania siyo maskini ni matajiri, tuna uvuvi, bahari zimetuzunguka, tunaacha watu samaki wetu wanachukua, vyote hivyo ni vyanzo vyta mapato. Hebu tuvitumie vizuri, wataalamu tunao timu, hiyo hapo mbele, mimi ninahisi ni timu ya wataalamu, ifanye kazi ya ziada tuone namna gani tutapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, suala la kuzuia kuingiza magari yenye umri wa miaka kumi; Watanzania ni maskini, hadi leo Watanzania ni maskini, lakini wote wanapenda kustarehe, hakuna asiyependa kustarehe. Ukiuia kuagiza magari yenye umri huo ni Watanzania wangapi wataweza kununua magari mapya?

Mwenzangu mmoja amesema hapa yeye Mbunge na hakununua gari jipya na siyo yeye tu na wengi humu

ndani siyo wengi walio na magari mapya kabisa kwa sababu uwezo wetu ni mdogo. Kwa hiyo, hili suala tulitafutie ufumbuzi, tutawanyima Watanzania haki yao ya msingi. Gari siku hizi ni kitendea kazi muhimu sana, kinakuharakishia shughuli zako kabisa.

Mheshimiwa Spika, mtu akidunduliza akipata shilingi zake milioni tatu, anakwenda kutafuta kigari kinamsaidia kumharakisha kazini, kinamsaidia kushughulika na harakati zake za kimaendeleo. Kwa hiyo, tusiwaondoe Watanzania katika matumaini ya ulimwengu huu wa kisasa. Ulimwengu huu wa kisasa kila mtu anahitaji gari, anahitaji pikipiki, anahitaji vespa, kwa hiyo, tujitahidi tuliangalie kwa umakini hili suala jamani, ni gumu sana tunawatoa matumaini Watanzania wenzetu hawa ambao wanaishi maisha duni, tuisiwakatishe tamaa. Mheshimiwa Waziri amesema kuwa, magari haya yanababisha ajali, yanachafua mazingira, lakini je, amefanya utafiti kiasi gani na kuona kuwa yanababisha ajali; amefanya utafiti wa kina? Ndiyo pale niliposema kuwa hakuna utafiti.

Nije pia kwenye suala la kuongeza ushuru katika unga wa ngano; anayepata athari siyo mfanyakibashara, hakuna mfanyakibashara anayekubali kupata hasara hata siku moja; mwisho wa siku anayepata hasara ni mimi na wewe. Zaidi, tumwangalie Mtanzania aliye katika hali ya chini kabisa, unga sasa hivi kilo moja ni shilingi 1500, keshokutwa utakuwa 2000, kwa hiyo ni tatizo. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Devotha Likokola, Mheshimiwa Khalfan ajiandae, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Maria Hewa na Mheshimiwa Kigwangala atakuwa wa mwisho asubuhi hii.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ninaungana na Wabunge wenzangu, kumshukuru sana

Mwenyezi Mungu na kushukuru sana kwa ajili ya Bajeti hii. Ninawapongeza Wataalamu wa Wizara ya Fedha na wa Wizara ya Mipango na hasa Idara ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Wabunge wengi wamesema, umejenga historia ya nchi yetu, umeweka Kamati ya Bajeti na inaweza kusaidia sana kuleta bajeti yenyе manufaa kwa nchi yetu. Siyo tu umeleta Kamati ya Bajeti, lakini umefanya kazi kubwa sana kuwasomesha Wabunge katika masuala haya ya bajeti, umewapeleka Wabunge maeneo mbalimbali, umewapa mafunzo ya aina mbalimbali yanayohusiana na bajeti; katika hili tunakupongeza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tukianza na bajeti yetu, kweli bajeti yetu ni nzuri, lakini ina changamoto ni nyngi. Wananchi wetu wengi wanapokaa na kuisikiliza bajeti hii wanajuliza bajeti hii inawaletea matumaini gani? Kwa bajeti ya mwaka huu, ninapenda kuwaambia Wananchi ni bajeti yenyе matumaini makubwa, kinachotakiwa ni Wananchi kujipanga kuangalia vipaumbele vilivyopo na kuweza kushirikiana kutekeleza bajeti hii. Tukitaka bajeti yetu itekelezwe vizuri, bado tuna changamoto kubwa. Tunakusifu umeunda Kamati ya Bajeti, lakini tunataka kuiuliza Serikali ni lini italeta Sheria ya Bajeti, kwa sababu kama tunataka bajeti itumike vizuri, basi tuwe na Sheria ya Bajeti iweze kusimamia utekelezaji wa maazimio yote ambayo yanatolewa kwenye bajeti hiyo? Waziri amekuwa akiahidi mara nyngi kuwa ataleta Sheria ya Bajeti lakini hili bado halijatekelezwa. Tunaomba Sheria ya Bajeti iungane na nia nzuri uliyonayo ili bajeti yetu iwe inayotekelzeza.

Mheshimiwea Spika, tuna Mpango wa Taifa, ninaomba kuiambia Idara ya Mipango kuwa, Mpango huu ni mzuri, lakini ninaomba Wananchi wengi waelezwe huu Mpango, wengi hawaujui; na kama unapangwa bila kushirikisha Wananchi wengi ni ngumu sana Wananchi wakaona maeneo yao ya vipaumbele. Kama Wananchi wengi hawajashiriki katika kuviiuba vipaumbele hivi, bado kutakuwa na mgogoro katika kutekeleza, kwa sababu ni

ngumu sana kutekeleza mpango ambao hujashiriki katika kuupanga. Ninaomba Wananchi waelekezwe Mpango huu wa Bajeti na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Serikali ilianza kutekeleza masuala mazima ya bajeti ya kijinsia, tunaomba katika mpango wadau mbalimbali washirikishwe ili utekelezaji wake uwe na manufaa kwa aina zote za watu walioko nchini. Tuna wanawake wengi sana, tunataka kujua ni namna gani wanawake wa nchi hii wananaufaika na bajeti hii; ni kwa asilimia ngapi vijana wa nchi hii wananaufaika na bajeti hii; na ni kwa kiasi gani wazee wa nchi hii wananaufaika na bajeti hii? Tukiweza kujua kwa takwimu ni rahisi kila mmoja kuiona bajeti hii ni bajeti ambayo inaweza kuwasaidia watu wengi.

Mheshimiwa Spika, tuna kundi kubwa la walemvu, ni vizuri tukaainisha ni kwa namna gani walemvu katika nchi hii wananaufaika na bajeti hii. Tusipoainisha haya makundi maalumu, bado kutakuwa na manug'uniko makubwa katika jamii yetu. Ninajaribu kuangalia katika suala zima la mapato ya nchi yetu, suala la mapato ni nyeti na ninaomba maadam umeshaunda Kamati ya Bajeti, ni vizuri Kamati hii ikajikita katika kuangalia mapato, maana bila mapato tutagawana nini? Tutakaa hapa tunagombana mapato hayaonekani, kila mtu ananung'unika hakuna mapato, hakuna mapato.

Mheshimiwa Spika, Mussa alikuwa anawapeleka Wana wa Israel, walipofika Bahari ya Shamu wale Wana wa Israeli walikuwa wanalamika, Mussa mwenyewe alikuwa analia, lakini alimlilia Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu akamwuliza Mussa kwa nini unalia akasema sielewi cha kufanya. Mwenyezi Mungu, alimwuliza Mussa una nini mkononi? Tumia ulichonacho, fimbo uliyonayo mkononi, piga maji yatagawanyika na Wana wa Israeli watapita. Mimi ninaomba kuuliza Tanzania tuna nini mkononi? Lazima tujiulize Watanzania tuna nini mkononi? Tanzania hii ina watu milioni 44.9; kweli nchi hii tumeshindwa kutumia watu hawa tupate maendeleo?

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina vijana karibu inafikia asilimia 60, kweli tumeshindwa kuwatumia vijana hawa ili tupate maendeleo? Kuna wanawake mahiri kweli wameshindwa kutumika? Kuna wazee, watu wenye uzoefu, wataalam wazuri, kweli tunashindwa kuwatumia na nchi yetu ikapata maendeleo? Tuangalie tulichonacho mkononi.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina ardhi, nchi hii ina madini mbona hatuoni mchango wa madini katika Pato la Taifa. Lazima tutumie tulichonacho, madini yako wapi jamani; ni lazima tutumie madini yetu.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nyingi sana bajeti zao inaongoza kwa vile walivyonavyo. Nchi ya Botswana tunaambiwa madini waliyonayo yanasaidia kuongoza ile nchi; kwa nini isiwe Tanzania? Tunaambiwa Botswana wana idadi ndogo tu ya ng'ombe, lakini inasaidia kukuza uchumi wa nchi ile, kwa nini isiwe Tanzania ina ng'ombe kila mahali?

Mheshimiwa Spika, mimi naona ajabu, tuna bahari, tuna mito, tuna maziwa, tuna gesi, jamani hivyo vitu Mwenyezi Mungu ameleta kwa ajili ya Watanzania. Tukiendelea na mchezo wa kuingia mikataba isiyokuwa na tija kwa Watanzania, Mwenyezi Mungu atatuangalia kwa jicho bayaa na mimi ninaogopa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie kuwa, kuna Wawekezaji Wakubwa, kuna *Private Sector* ambayo inatakiwa ikue katika nchi yetu, lakini je, tunawawezesha vipi? Wafanyabiashara wetu hatuwapi motisha, hatuwapi mitaji, hatuwapi elimu; kwa nini? *Private Sector* isipokua nchi haikui. Kwa hivyo, ni lazima tuikuze *Private Sector* yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie pia makampuni yanayofanya vizuri nchi hii. Ninashangaa Kitabu cha Bajeti cha Waziri wa Fedha, anakazana kuwasifu wafadhili tu, ina maana nchi hii hakuna watu wanaofanya vizuri, hamna makampuni yanayolipa kodi vizuri, mbona hamyaleti hapa tukayasifu, kwa nini tuna mambo ya kuangalia watu wa nje tu? Hii ni aibu kwa nchi yetu. Lazima

tuseme katika nchi yetu makampuni haya yanafanya vizuri, yanalipa kodi vizuri na ni lazima tuyatambue kwa sababu ndiyo yatakayojenga uchumi endelevu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala zima la *Big Results Now*. Nina ombi moja tu kwa Serikali, kama wanataka *Big Results Now* iende vizuri, wenzetu wa Malyasia walianza kusomesha makundi ya watoto, walitoa vijana wakawapeleka kusoma nchi mbalimbali na kwa wingi, siyo hapa tunaambiwa sijui *scholarship* nane, mbili, mia, mia tano, elfu, ndiyo vijana wakirudi wakielewa yale mambo wataweza kujenga uchumi endelevu.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma, Barabara ya Namtumbo - Tunduru ishughulikiwe kwa mpango wa dharura. Ile barabara ina hatari, watu wanapata tabu, tangu Uhuru mpaka sasa ile barabara ni ya hatari na ni barabara inayoshangaza. Siku moja nilikuwa naongea na Mtaalam mmoja wa Wizara, akaniuliza hivi ni kweli ile barabara haina lami mpaka leo! Nikamwambia ni kweli; akasema hapo Serikali haijawatendea haki. *Big Results Now* kuna mtaalam anaitwa Dkt. Gwajima, yupo Wizara ya Afya, yule mama ana uwezo mkubwa na ni Daktari wa Wilaya Mkoa wa Singida, mchukueni yule anaweza kuleta *Big Results Now*, mpelekeni kule yule mama anaweza akafanya mambo makubwa na mapinduzi. Ameshafanya kwenye Wizara ya Afya, mchukueni kwenye *Big Results Now* na Idara ya Mipango ili aweze kusaidia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.  
*(Makofii)*

**SPIKA:** Yaani aende akajenge barabara? Mimi nilifikiri akasimamie afya siyo akajenge barabara, itakuwa tatizo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Salum Khalfan, Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa niweze kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze na ushauri mdogo tu kwa Viongozi, Wabunge pamoja na Watanzania kwa ujumla. Uchumi imara kote Duniani hauwezi kupatikana kama nchi hiyo au Wananchi wake hawatakuwa na amani, utulivu, ambao utawafanya pamoja kuzingatia ni namna gani nchi yao inaweza kuipeleka katika ustawi wa uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, na kama nchi hizo hazitakuwa na utawala wa sheria ili Wananchi wapate haki zao stahiki na kama nchi hizo hazitakuwa na Utawala Bora kwa maana kwamba, Serikali itashughulikia kutoa huduma za jamii kama vile afya, elimu na mambo mengine, bado nchi hiyo itakuwa ndoto kwenda katika ustawi. Vilevile kama nchi haitakuwa na demokrasia ya kweli, Wananchi wakapata Viongozi ambao wanawaona wanafaa, hakutakuwa na ujanjaujanja katika kuwapata Viongozi ambao wanaweza kushika mamlaka ya dola, migogoro siku zote itakuwa inaendelea katika nchi hizo na amani itakuwa haipo, mwisho wake nchi hiyo bado itakuwa haiwezi kupata maendeleo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala zima la bajeti, ni kwa namna gani tunasema tumekuja katika Bunge hili kuja kupidisha Bajeti ya Serikali. Bajeti ipo kwa mujibu wa sheria, tupo hapa kupidisha bajeti kwa mujibu wa sheria, hatukuja hapa kama kitengo cha kisiasa, hapana. Tuna wataalam wetu ambao tayari wanatushauri juu ya suala zima la kupidisha bajeti na sisi kama Wabunge, tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba, tunaisimamia Serikali kutekeleza wajibu wake katika kuifanya bajeti yetu ifikie malengo yake.

Mheshimiwa Spika, lakini hapa jambo la kusikitisha ni kwamba, tunapitisha bajeti leo, baada ya mwaka mmoja, mwaka wa Serikali unapoanza, Bajeti ya Serikali inashindwa kufikia malengo yake. Tunapewa sababu mbalimbali hapa; wahisani wameshindwa kutoa pesa kwa wakati, makusanyo ya Serikali yamekuwa madogo, lakini

uhalali wa kisheria wa kuwepo bajeti hii ukoje? Serikali inapaswa kuwajibika kwa Wabunge kama tunavyowajibika katika kuwasimamia. Pale tunapofikia mahali kwamba bajeti imeshindwa kufikia malengo, sisi kama Wabunge tuna wajibu gani kwa Serikali hiyo?

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa hapa kwamba, bajeti ya 2012/2013 katika Wizara mbalimbali haikufikia malengo yake. Tunaambiwa kuna asilimia 35, asilimia 40, Wizara zilikosa pesa, Halmashauri zetu hazikufikia malengo ya bajeti, hili ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, hata kama hapa tutaambiwa tuna trilioni 23 katika bajeti hii, mwisho wa mwaka tutaambiwa kwamba, pesa ambazo zimekwenda katika Wizara na Halmashauri mbalimbali ni asilimia 40 au 50 tu. Hatuwezi kufikia maendeleo yetu kama tunavyotarajia.

Mheshimiwa Spika, pia kuna jambo ambalo lipo muda mrefu bado halijafanyiwa kazi la kuhamisha mafungu ya fedha kutoka Wizara moja kwenda katika Wizara nyingine bila idhini ya Bunge. Nimesema hapa kwamba, hii bajeti ipo kwa mujibu wa sheria, Bunge ndiyo limeidhinisha kwamba kiasi hiki cha pesa kinakwenda katika eneo fulani, lakini kuna usoefu uliopo sasa kwamba, tunaweza tukahamisha mafungu ya pesa bila Bunge hili kuwa na taarifa. Inaonekana kama hili Bunge ni *rubber stamp* tu; kwamba, tunakuja ili ioneokane bajeti hii imepitishwa na Bunge, lakini mwisho wa siku Bunge hili bado halipati taarifa juu ya mabadiliko ya kibajeti ambayo yanafanywa na Serikali. Hili linaweza likatuletea tatizo.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa hapa tumeongeza eneo fulani fedha, tunakuwa tuna namba kubwa lakini matokeo yake fedha hizi hazifiki katika miradi mbalimbali ambayo tunaitarajia.

Mheshimiwa Spika, sisi tunakuwa mabingwa wa mikakati, ambayo imeshindwa. Tuna mikakati hapa zaidi ya mitano, sita, tangu tunapata Uhuru, lakini mikakati hiyo

yote siyo endelevu. Siyo mikakati ambayo tayari inatupa matumaini, Watanzania wamechoka na mipango hii.

Mheshimiwa Spika, leo tunasema mipango yote ipo kwa mujibu wa Sera, lakini imebadilika, leo tuna mipango ipo kwa mujibu wa awamu siyo Sera za Chama, Sera za Nchi, Sera za Kitaifa. Mipango yote inakwenda kwa mujibu wa awamu zinazokaa madarakani.

Awamu ya Mkapa tulikuwa na *Mtwara Corridor*, hakuna maelezo ya Serikali juu ya *Mtwara Corridor* yako wapi leo, *Mtwara Corridor* imekwenda wapi? Utaratibu wake uliridhiwa na Bunge alipoondoka Mkapa katika mamlaka na Mawaziri wake, habari ya *Mtwara Corridor* haipo, leo tunakuja na mpango mwingine huu ambaao tayari tunao. Mimi naamini kabisa mpango huu baada ya Awamu hili ya Nne kuondoka atakayeku na Serikali mpya atakuja na mpango wake. Hatuna Mpango Maalum wa Kisera wa Kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, hatuwezi kufikia Malengo ya Maendeleo kama bado hatujawa makini, ni lazima tuwe na Sera za Kitaifa, ambazo awamu yoyote ambayo itakuja madarakani itakuja kuendeleza pale awamu nyingine ilipoachia. Tuna uzoefu kwamba, kila awamu inayokuja tayari inakuja na mpango mpya ambaao bado hauwezi kutuletea maendeleo. Tunasema tuna mipango isiyo endelevu na sisi ni mabingwa wa mikakati iliyoshindwa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo eneo la watu wenye ulemavu. Bado Serikali inatoa ruzuku kwa makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu katika Taifa letu, lakini bado ruzuku hiyo haitoshi, ni ruzuku ndogo kabisa, haiwezi kuendesha vyama vya watu wenye ulemavu. *Ceiling* ambayo inatolewa ni ile ile zaidi ya miaka kumi, mahitaji leo yameongezeka, walemovu wameongezeka, wapo wengi katika Taifa hili. Tunaitaka Serikali ihakikishe inaongeza ruzuku katika maeneo ya makundi ya watu wenye ulemavu ili tuweze kufikia malengo yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la *formula* ya mgawanyo wa rasilimali katika Taifa letu bado ni utata na ndiyo manung' uniko mengi yapo ndani ya Taifa hili. Watu katika maeneo wanalamika, wanapiga kelele, huku maendeleo hayapo, huku wamependelewa, kwa sababu hakuna *formula* maalum ambayo tayari inaelekeza kwamba mgawo wa rasilimali katika Taifa letu ukoje.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Lindi Mjini, nimezungumza mara kadhaa na Waziri wa Fedha, ni namna gani sasa Manispaa ya Lindi imetoka katika Halmashauri ya Mji. Tulikuwa tunapata *ceiling* ya milioni nane kabla hatujawa na Halmashauri, tumeongezewa Kata tano kutoka Halmashauri ya Wilaya katika Majimbo ya Mchinga na Mtama, lakini bado tunaendelea kupata *ceiling* ile ile ya Halmashauri ya Mji, baada ya kuwa ndani ya Manispaa ya Mji wa Lindi, tumeongezewa Kata tano zingine, bado Serikali imekuwa kiziwi, imekuwa kipofu juu ya hoja za Wananchi wa Lindi kwamba tayari Halmashauri ile imekuja kisiasa tu, haikuwa na maana kwamba imeletwa Manispaa kwa ajili ya maendeleo ya watu wake.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ihakikishe mgawo wa bajeti uende sambamba. Mliahidi hapa katika llani ya Uchaguzi ya CCM kwamba, mtahakikisha mnatoa kipaumbele katika maeneo ambayo bado yapo nyuma kimaendeleo. Mlichukua kura nyngi kwa hoja hiyo, lakini yote yale leo mmesahau kwamba mliahidi nini na ndiyo haya matatizo ambayo leo yanajitokeza katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, bado kuna migogoro mingi, watu wamefikia mahali hawaiamini Serikali kwa kauli zake. Hivyo, hayo ndiyo mambo ya kuzingatia katika kuona kwamba ni namna gani tunaweza tukajenga uchumi imara ambao Wananchi watashirikishwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia suala la thamani ya bidhaa za kilimo. Bado inaonekana kabisa kwamba, kilimo hakioneshi kwamba kinawenza kikatoa mchango mkubwa wa maendeleo katika Taifa letu. Tunaendelea

kuuza mazao yetu ya kilimo ghafi katika masoko ya nje, badala ya mazao hayo kuyafanya *process*. Tuna viwanda vya korosho kadhaa katika Mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi, lakini bado viwanda vile vimesimama tunaendelea kuuza korosho ghafi katika masoko ya nje. Tunanyima watu ajira, hivyo ni wakati mwafaka tulitegemea kauli ije na ufumbuzi wa tatizo ni namna gani sasa korosho, pamba, kahawa na vitu vingine ambavyo vinatokana na kilimo vinafanyiwa *process* ili viwe na thamani katika kuboresha uchumi ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, kama hatujawa makini, hatujazingatia maendeleo ambayo yamepatikana katika nchi mbalimbali huko yameanzia wapi. Walikaa hapo, wakakaa pamoja, wakaona tatizo letu la msingi ni nini. Tatizo ni elimu, ni afya, ni kilimo ni namna gani tunakwenda katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya nchi. Tunakurupuka tu leo katika kujenga uchumi wetu, hatuna uhakika tunakwenda katika jambo gani na tunajiandaa kwa lipi.

Mheshimiwa Spika, tuna uhaba wa chakula katika nchi; nchi ina ardhi nzuri, ina mito, ina mabonde na ina watu wenye uwemo wa kufanya kazi, lakini unashangaa Watanzania leo wanalia na njaa na wanasema Taifa lao lina njaa. Kuna nini hapa? Hatujawa na mpango madhubuti, hatujawa na mpango imara, hatujawa na mpango endelevu, ambao unaweza kuwaondoa Watanzania katika umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, tunalazimika sasa tuwe na mjadala wa kitaifa katika nchi hii, hatuwezi kuwaachia watu wachache wafanye mipango ambayo imeshindwa kuleta maendeleo. Zaidi ya miaka hamsini leo, tumeachia kundi moja ambalo limeshindwa kuleta maendeleo katika Taifa letu. Wakati umefika sasa kama Taifa tukae pamoja, tutumie wataalam wetu, tuone tunatokaje katika umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wamechoka, Watanzania wana maisha magumu, Watanzania wanahitaji maendeleo. Nchi jirani zinazotuzunguka zimepiga hatua kubwa ya maendeleo sasa, sisi tunabaki nyuma kwa lipi?

Mheshimiwa Spika, Msumbiji tu hapa wamepiga hatua kubwa, tumewasaidia kudai uhuru, wale wana miaka thelathini tu tangu Uhuru wao lakini leo wanaishi vizuri katika ustawi wa Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hilo, nataka tukae tuone ni namna gani... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Christina Ishengoma, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mheshimiwa Mangungu, huenda na Mheshimiwa Masoud Abdallah anaweza akafikiwa.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuongea katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongozi kwako kwa kazi nzuri unayoifanya humu Bungeni kwa kuendesha vikao vizuri. Napenda pia kuwapa pongozi Mawaziri wanaohusika na bajeti hii na watu wote ambao wamehusika kuchambua na kutekeleza bajeti hii kuanzia huko kwenye Kata mpaka hapa tulipofikia Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu kupandisha ushuru wa *petrol* pamoja na *diesel* na mafuta ya taa. Naomba sana iangaliwe kwa undani, ingawa tumpunguza ushuru kwa vitu vingine na kodi, lakini hii itaweza kuathiri mambo mengi hasa tukipandisha mafuta ya *petrol* na *diesel*; itapandisha bei ya usafiri, itapandisha

bei ya bidhaa mbalimbali, itapandisha bei ya vyakula. Kwa hiyo, naomba sana hili jambo liangaliwe kwa undani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mafuta ya taa, tunajua kuwa Wananchi wengi na hasa wa vijijini, wanatumia sana mafuta ya taa. Ningombwa sana nalo liangaliwe vizuri, tusiathiri na kuleta mgongano kwa Wananchi wetu ambao tunawapenda sana.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ninaomba kuliongelea tena ni kuongeza ushuru wa bidhaa hasa zinazotokana na juisi. Tunajua kuwa, Tanzania sasa hivi tuna matatizo ya utapiamlo na upande wa vitaminini ni matatizo. Akina mama hasa wajawazito, wanapata matatizo ya *anaemia*, upungufu wa damu kwa watoto. Kwa hiyo, ninaomba kwa sababu haya matunda yanazalishwa nchini kwetu, yaslongezwe ushuru wowote, ushuru wote utolewe. Juisi ni nzuri na hasa kwa manufaa ya akina mama wajawazito na watoto wadogo. Ninaomba ushuru utolewe kabisa, ifanane na maji ambayo tumesema yanayozalishwa katika viwanda hayatakuwa na ushuru wowote. Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa uchambuzi wa bajeti hii. Tangu tumeanza mpaka tulipo, imeweza kushirikisha watu wengi, imeweza kushirikisha Wabunge vizuri sana, tumeweza kuichambua na tumeweza hata kuongeza fedha kwa Wizara zingine kama Maji, Kilimo na Maendeleo ya Akina Mama na vitu vingine vyote ambavyo tumezikilizwa na Kamati ya Bajeti na Wizara. Naishukuru sana na ninaipongeza sana Kamati ya Bajeti, kwa kazi nzuri iliyoifanya kwa kuweza kuongezea fedha kwa Wizara mbalimbali ambazo tumeomba fedha na kukubali kuongezwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naomba kuliongelea ni kuhusu fedha, ni kweli tumeongea kwenye bajeti na fedha zimetengwa. Fedha zinazoenda kwenye Halmashauri na kwenye mikoa ingawa siyo nyingi sana, lakini

naomba sana ziende kwa wakati ziweze kufanya kazi huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wengi zaidi ya asilimia 70 wanaishi vijijini na wanapenda kuona maendeleo huko vijijini. Naomba hizo fedha zipelekwe kwa wakati, ziweze kufanya kazi ilivyo na zote kama zilivyotengwa zipelekwe hivyo hivyo bila ya kupunguza au nini. Naamini Serikali yetu sikivu inaweza, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaweza. Nitashukuru kama fedha zote zitapelekwa kama zilivyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaloomba kuliongelea ni vipaumbele. Vipaumbele vya Taifa ni vizuri sana. Naishukuru Serikali kwa kuweka hivi vipaumbele. Vipaumbele hivi vikitiliwa maanani, naamini Watanzania wote wataweza kuona manufaa ya nchi yao na jinsi inavyowapenda. Nikianza na ukusanyaji wa mapato; kama kweli tutasimamia ukusanyaji wa mapato, pato letu litawenza kuongezeka na Wananchi wataweza kufaidi uchumi wao. Jambo muhimu ninaloliomba ni kuwa, tumeanza kukusanya mapato kwa kutumia *electronic hasa receipt*.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wengi hawana elimu ya kudai risiti mara wanaponunua bidhaa. Hii inarudisha nyuma pato letu. Kwa hiyo, naomba elimu itolewe kupitia kwenye vyombo vya habari, kupitia kwenye vyombo vyo vyote vinavyohusika na kupitia mahali popote pale, kusudi Wananchi waweze kudai risiti mara wanaponunua bidhaa zao kama nchi zingine zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru ulinipeleka Canada, nilijiona mimi mwenyewe hata chakula unachokula unatoa kodi inahesabiwa kwa pato. Kwa hiyo, wao wapo makini sana kutoa risiti zao. Naomba sana Wananchi wadai hizo risiti.

Mheshimiwa Spika, kwa kipaumbele cha kilimo, kama nilivyosema kuwa asilimia 70 ya Wananchi wanaka huko vijijini na wanategemea kilimo. Jambo ninaloomba,

fedha zilizotengwa kwa pembejeo zipelekwe kwa wakati kusudi kwa kutumia Wagani, Wananchi waweze kufaidi kilimo chao. Kitu kingine ninachoomba, kufuatana na mipango mbalimbali ya KILIMO KWANZA, SAGCOT, *Smart Partnership, Big Results Now*, zikisimamiwa vizuri, naamini Wananchi wetu wataweza kuona matunda ya kilimo na wataweza kufaidi matunda hayo pamoja na pato lao la kaya na nchi yetu litaweza kupanda.

Mheshimiwa Spika, kwa jambo hili la kilimo, naomba sana tuwatumie Wataalam wetu wa SUA pamoja na wataalam wengine na watafiti wengine, kusudi tuweze kuleta mabadiliko kwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni elimu hasa rasilimali watu kwa upande wa sayansi. Nyote ni mashahidi kuwa, wanafunzi wa siku hizi hawapendi sana kusoma masomo ya sayansi. Nashauri kuwa, mpango au utaratibu wa wataalam au walimu kupita mashulenii kushawishi wanafunzi kuanzia hasa *Form Two* kuanza kuchukua masomo ya sayansi, naomba uangaliwe. Kwa sababu wakishawishika, wataweza kuchukua hayo mafunzo ya sayansi na tutaweza kupata rasilimali watu hasa kwa upande wa sayansi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nishati hasa nishati ya vijijini, nashukuru sana, hivi ninavyoongea Wananchi wengi na Wabunge wengi wamefurahi, hela zimetengwa na zimeongezwa, kwa hiyo, Wananchi wengi kwenye majimbo yetu wataweza kupata umeme. Hata kwangu kule Morogoro, naamini wataweza kupata umeme na hivi ninavyoongea hata huko Ismani kwa siku hizi tatu watapata umeme. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwa kuliona suala hili la umeme. Pia kutohana na umeme, Wananchi wengi hasa wanawake wataweza nao kufaidi kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vyaa usindikaji na namna hii, tutaweza kukuza pato la Mwananchi na pia la nchi yetu.

Kwa upande wa miundombinu, barabara tunaziona zinazidi kupendeza. Kwa upande wa reli, kwa upande wa

19 JUNI, 2013

viwanja nya ndege, hayo yote ni mambo mazuri ya Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Tunawashukuru Viongozi wetu wa Awamu ya Nne.

Kuhusu maji; maji safi na salama; ni muhimu sana kwa Wananchi. Sote tunajua kuwa Wananchi huko vijijini wana matatizo sana ya maji, lakini kama hivi tumeomba fedha tumeongezewa; tunashukuru sana kuona Wananchi wengi watapata maji na watazidi kupata maji safi na salama. Akina mama waliokuwa wanapoteza muda wao saa 24 kutafuta maji, wataweza kufanya miradi mingine ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea kuhusu mambo ya uchambuzi wa bajeti, nimeshaongea kuwa nashukuru sana mpango ulikuwa mzuri. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuchangia hayo machache na ninaamini hata vijana wataweza kujiajiri kwa sababu umeme utakuwa vijijini, maji yatakuwa vijijini na wataalam wengine wote watakuwa vijijini. Kwa hiyo, wataweza kujiajiri huko vijijini hawatapata muda wa kuja mjini kuranda randa hovyo hovyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu katika suala zima la bajeti ya kipindi hiki, bajeti ambayo tumeianza na mabadiliko tofauti na tulivyokuwa tukizijadili bajeti za miaka iliyopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia kwa jinsi ulivyokuwa jasiri, kwa kuunda Kamati ya Bajeti ambayo inaongozwa na Kiongozi mahiri kabisa, Mheshimiwa Mtemi Chenge, ambaye huwa anaongea kwa uhakika kwa kile

kinachotoka kinywani mwake akiwa anasaidiwa na Kamati yake hiyo ya Bajeti. Nakupongeza kabisa. (*Makofi*)

Pamoja na hayo, mfumo wetu huu tuliouanzisha kwa sasa wa kuanza bajeti mwezi wa nne na kumaliza mwezi wa sita, ninaamini tunaweza tukatoka mahala tulipo, kwa sababu Wizara tunapozijadili mwanzo kwa kuwa na *ceiling* fulani baadaye mwishoni kunakuja kujitokeza fedha ambayo inakuwa ni kama vile albaki, ilikuwa ni 16 lakini tumekwenda mpaka 18. Hilo peke yake sasa inatupa mwanga wa kujua wapi vipaumbele vyetu ambavyo tunesuguana humu kabla na kuvipa pesa, ambayo nadhani inauweka unafuu wa Wananchi wetu kujua Wabunge wamejadili nini kinagusa kero zao katika utaratibu huu mpya tuliouanzisha. Ninaomba udumu kwa kweli, nadhani unatupeleka mahala pazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijazungumza mengi niliyonayo, naomba nianze na ushuru ndani ya mafuta. Mimi naweza nikasema *okay* mmeona kuna utaalam ndani wa kuongeza ushuru kwenye mafuta ya *petrol*, dizeli na nini. Ombi langu futeni kuongeza ushuru kwenye mafuta ya taa. Naomba kabisa kwa sababu haya mafuta ndiyo wanayotumia akina mama, bado vijiji wanapoenda kujifungua, wanunua wenyewe. Kwa nini tufiche! (*Makofi*)

Sasa yanapopanda, yaani tunajiweka mahali pabaya. Msidhani kwamba huu umeme tunaouzungumza umeme vijiji utakwenda kwa mwaka huu au mwaka kesho ndiyo tunamaliza shida za kuweka umeme kwenye vijiji vyetu. Hapana, naomba hilo ni ombi rasmi nalileta kwako Mheshimiwa Waziri ufute ili akina mama waendelee kununua mafuta hayo kwa matatizo mbalimbali huko vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kitu ambacho huwa kinanichanganya kuhusu uzalishaji wa mali zetu viwandani. Viwanda vya nchini mwetu. Tunalalamika hatuna viwanda vya kutosha. Tunazalisha mali kutokana na viwanda vyetu, lakini tunaagiza vitu kutoka nje kwa maana ya kufidia uzalishaji wetu tulionao pungufu. Nchi zetu jirani zina

viwanda vya kutuzidi sisi, lakini wenzetu wanazalisha na bado wanaagiza vitu vingi kutoka huko nje na wanakuja kuuza kwa bei ya chini. Sisi ambaao tunaagiza pamoja nao tunashindwa kuvinunua, badala yake tunakwenda kununua kwa nchi jirani na kuuza tena kwa bei nafuu.

Sasa mimi huwa najiuliza ni nini; kama si sisi tuna ushuru wa hali juu tusiotaka kujifunza hata kwa majirani zetu wanatoza ushuru wa namna gani ili twende sambamba nao, Watanzania wasishawishike kwenda kununua vifaa kwa nchi jirani. Tufanye utafiti wa kuona tutoze ushuru namna gani wa vifaa hivi na majirani zetu vifaa vyao viro chini kiasi cha kwamba, tunakimbilia kununua huko hata simu. Simu za mikononi hivi wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wanakwenda kununua Kenya. Wanapeleka fedha zetu Kenya wanakuja kutuuzia humu tena kwa bei ya chini kidogo ukillinganisha na za kwetu humu. Simu inayonunuliwa kwa shilingi 70,000 tunauza kwa laki na nusu. Hapo huwa kuna nini? Hatutaki kujifunza kuona tunaishije na ushuru wa vifaa vyetu hivi ambavyo tunaagiza kutoka nje na wale wenzetu wanatusababisha tunavinunua tunavileta. Tucheki ushuru wetu ukoje? Tupate majibu jamani. (*Makofii*)

Lingine ambalo ninapenda kuliongelea ni suala hili la bodaboda. Jamani watu wa bodaboda tusiwakatishe tamaa. Tusiwakatishe kabisa tamaa kwamba bodaboda ni za matajiri. Sijui tufanye nini? Mtulie hivyo hivyo kabisa, msije mkaongeza, wale wanaosema ni za matajiri inawezekana wapo kweli matajiri ndiyo wanawapa hawa watoto hizo bodaboda. Isije ikawa kigezo sasa cha kusema zile ni za matajiri. Wamo pia wenye bodaboda zao ambaao wanaishi nazo wamo kabisa.

Tatizo labda ni ule uchambuzi tu wangapi ambaao wana bodaboda za matajiri. Wengine ambaao ni bodaboda za kwao, lakini msimamo ubaki pale pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la ugawanyaji wa rasilimali hapa nchini. Rasilimali za maendeleo, rasilimali watu

na ujuzi. Jamani Kanda ya Ziwa tuna Mikoa yapata sita, lakini hatuna Chuo Kikuu cha Umma. Miaka 50 ya Uhuru, tunazidiwa na Morogoro wana vyuo viwili vya Serikali, sisi hata kimoja ndani ya Kanda. Tunalia walau tupate hata kiwanda cha *cement* nacho hakuna kimeanzishwa kwingine. Barabara sisi mpaka tumekuwa wa mwisho kuwekewa lami; jamani hivi tuna makosa gani Kanda ya Ziwa? Kila kitu sisi wa mwisho. Tunayo ardhi ya kutosha kupata na sisi Chuo Kikuu cha Serikali. Wasingekuwa Wakatoliki hawa tungekuwa wageni wa nani? Ndiyo waliotujengea huko na bado wameendelea kufika huko Mtwara, wako Tabora, sijui wako wapi. Hawa ni *private*. (*Makof!*)

Sisi cha Serikali kiko wapi Kanda ya Ziwa? Haa jamani, mnataka nishangae Kisukuma! Jamani tunaomba Kanda ya Ziwa na sisi mtufikirie na walipa kodi wako huko. Kodi zetu zinakwenda wapi? Mnatuona sisi hatutaki maendeleo. Tunaomba, mmezungumzia hili, kipindi kijacho tunaomba bajeti ijayo mtukumbuke katika hili. Ardhi tunayo, Butiama kule, mimi sizungumzii wapi kijengwe, lakini tunataka Kanda ya Ziwa na sisi ni walipa kodi kule. (*Makof!*)

Mwisho, nasema Mheshimiwa Waziri, wewe ndiye Waziri wa Fedha, sasa nakukumbusha tena na nilikwambia wakati fulani kuleta taarifa ya uendelezaji wa miradi. Fedha zetu zinapotoka zinafanya kazi gani *quarterly* au kwa muda wa miezi sita. Nadhani tukupe miezi sita, labda tutakwenda vizuri ili tuwe tunajua fedha zinakotoka miradi imeteklezwa kwa kipindi hicho. Hiyo ndiyo pekee tena Watanzania tutaishi nao */ive* kujua tumetaja hapa kitu halafu kimeteklezwa. Hiyo ndiyo pekee tutaendana na nchi hii kujua hapa tumetamka fedha itoke, je, imetoka na kama imetoka imekwenda wapi. Tuwe */ive* na Wananchi. Tunataja miradi iliyoko huko katika maeneo yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite msemaji mwingine; Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla!

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, nitumie fursa hii, kumpongeza sana na kumkaribisha Bungeni kaka yangu mpendwa, Dkt. Dalay Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, ambaye alichaguliwa kwa kura halali na Wananchi wa Igunga. Jimbo ambalo aliniachia kulilea toka aliponyang'anywa Ubunge wake na Mahakama. (Makof)

Nitumie fursa hii kumpongeza sana na kumkaribisha Bungeni, rafiki yangu Mheshimiwa Aeshi Hilary, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, naye tena kwa kurejeshewa Ubunge wake na Mahakama. Naamini Watanzania watakubaliana na mimi kwamba, Mahakama sasa inatenda haki. (Makof)

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo za awali, sasa naomba nijelekeze kwenye kuchangia hoja hii ya Bajeti Kuu ya Serikali iliyoko mbele yetu. Ninaomba niweke kumbukumbu sahihi kwamba, sitaunga mkono hoja hii kwa sababu ambazo nitazisema. Kubwa zaidi, ikiwa ni kwamba, bajeti hii haitoi majawabu ya muda mrefu ya changamoto ambazo zinalikabili Taifa letu. Changamoto hizi ni pamoja na ajira kwa vijana, njaa na uhakika wa chakula, uharibifu wa mazingira, maradhi, lakini pia changamoto kubwa ya mfumko wa bei kwenye bidhaa mbalimbali.

Pamoja na kutokujibu changamoto hizi ambazo zinalikabili Taifa kwa sasa, Bajeti hii ni wazi kabisa iko *pro-inflationary*, kwa sababu inaongeza kiwango cha kodi kwenye baadhi ya bidhaa ambazo kwa kiasi kikubwa zinawagusa watu wa chini. Nitatoa mfano kwenye kodi ya huduma ya simu ambayo ni mawasiliano muhimu sana katika uzalishaji, pia katika maisha ya kila siku ya Wananchi. Vilevile kodi kwenye mafuta kwa maana *fuel in general*, ambapo katika hali ya kawaida ukiongeza tu kodi kwenye mafuta, maana yake unaongeza ghamama za usafiri na ghamama za uzalishaji kwenye viwanda na hivyo bei za bidhaa mbalimbali kwenye soko zitapanda. Ninaomba nitoe ushauri, wenzetu wa Wizara ya Fedha wajifikirie kwa

mara nyingine tena, waweze kufanya marekebisho ambayo yataondoa taswira ya *inflation* kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nilisema sitaunga mkono hoja hii mpaka itakapotoa majawabu ya changamoto zinazolikabili Taifa, ikiwa ni pamoja na ukweli kwamba, bajeti hii haioni mbali sana, iko *myopic in nature*. Inaangalia kwa karibu tu, kwa mwaka mmoja tu, haingalii mbali zaidi kwa kuwa hajielekezi kuwekeza kwenye sekta ambazo zinawagusa watu wengi. Pia kwa kuwa hajielekezi kuwekeza kwenye sekta ambazo zitakuza ajira ya watu wengi zaidi; na pia kwa hajielekezi kwenye sekta ambayo itapunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi na kuja kwetu, ili kuweza ku-*stabilise balance of payment accounts* na hatimaye kupunguza mfumko wa bei na mwisho wa siku kukuza uchumi. Bajeti hii haielekezi ni namna gani tutakuza uzalishaji katika nchi yetu katika muda mfupi na katika muda mrefu na badala yake ni bajeti ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa muda wa mwaka mmoja tu, mwisho.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu tungetaraja bajeti ya karne hii iwekeze zaidi kwa watu; kwanza, kwa kupunguza zaidi kodi. Kwa wale Wataalam wa Uchumi wanafahamu zile *reganomics, taxnomics* na hata *kigwanomics*, ambazo zimekuwa *named* baada ya jina langu, ambapo bajeti za aina hiyo zinalenga zaidi kwenye kuwekeza kwa watu zaidi kuliko kwenye kuuacha uchumi wa soko huria ujiendeshe kama unavyoenda, kwa kufuata *force* za *demand* na *supply*, bila kuangalia ni namna gani tutawekeza kwenye sekta ambazo zitadurufu uchumi wetu kwa haraka zaidi, ili kupunguza umaskini na kuongeza ajira kwa Wananchi. Kwa mfano, kuwekeza kwenye viwanda, kupunguza *regulation* kwenye sekta mbalimbali hususan kwenye *private sector*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuongeza *tax base*, kupunguza *tax* kwa ujumla na kupunguza kodi kwa ujumla wake, lakini kuongeza wigo wa kodi kama ilivyofanya mwaka huu kwa kiasi fulani kidogo, lakini pia kuhakikisha kuna *tax equity*, usawa kwenye kodi. Kwa mfano, leo hii

mtu wa chini mwenye kioski, anatozwa kodi kubwa sana ukilinganisha na mtu ambaye amewekeza kwenye sekta ya madini ama ya gesi au ya mafuta; jambo ambalo halikubaliki kwa kuwa haliweki usawa. Ndio maana nasema bajeti ya karne hii katika zama ambapo uchumi wetu ni wa mchanganyiko, ambapo kuna ubepari umeingia kwenye ujamaa, ni lazima tutafute na tuweke misingi ya kuweka usawa kwenye kodi yetu, lakini pia usawa kwenye mgawanyo wa mapato yanayotokana na kodi wanayotozwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii haitoi *Long Term Vision* ya kukua kwa uchumi wetu na ndiyo maana nimesema siiungi mkono. Ninaomba pia niseme kwamba, leo hii tuna fursa nydingi za kuweza kukuza uchumi wetu, ikiwa ni pamoja na kuwekeza kwenye maeneo maalum ya kukuza ajira kwa vijana, hususan wale ambao wanajilajiri kwenye sekta za kilimo na mifugo, ili waweze kuzalisha ajira nydingi zaidi na pia waweze kupunguza *importation* ya *goods*. Leo hii nguo zilizojaa kule kwenye maduka ya Kanda ya Ziwa zinatokea Kampala, madawa ya pembejeo hizi za kilimo yanatokea Nairobi; wakati huo sisi wenyewe tuna fursa ya kuweza *ku-attract* hivi viwanda vikaja kuzalishia hapa kwetu vika-supply kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kutoa mchango wangu kwa kuongelea jambo la amani na jinsi ambavyo linaweza likasaidia kuwa chachu ya kukuza Uchumi wa Taifa letu. Tunaichezea amani, Viongozi wa Kisiasa wanasimama majukwaani, wanatoa kauli mbalimbali ambazo zinahatarisha amani, wanaachwa.

Mheshimiwa Spika, katika hali ambapo nchi yetu amani imekuwa *so vulnerable*, Kiongozi wa Kisiasa anasimama na kusema kwamba, yeye amewaona waliolipua bomu kwenye mukutano wa hadhara. Inatia mashaka alilaona wakati gani, kwa sababu ninavyofahamu, Kiongozi ukiwa kwenye Mkutano unakuwa mbele, unakuwa jukwaa kuu na bomu halikupigwa jukwaa kuu lilipigwa kwa nyuma. Sasa mtu ambaye anasema

aliwaona wanaolipua mabomu, aliwaona wakati gani; alitumia kifaa gani; na kwa nini asiisaide Polisi kuweza kudumisha amani? Badala yake anatoa kauli tata ambayo itatia mashaka na wasiwasi mkubwa kwa Wananchi, jambo ambalo sidhani kama ni busara na ni la hekima kwa Kiongozi wa Kisiasa ambaye ana dhamana kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, sisi Viongozi ni *charismatic*. Tunaaminiwa na Wananchi na kauli zetu zina madhara makubwa sana kwa Wananchi; aidha, madhara *positive* ama madhara hasi. Naomba sana sisi Viongozi wa Kisiasa tuchunge ndimi zetu, tutoe kauli ambazo zitajenga na kudumisha amani, ili uchumi uweze kusonga mbele tuweze kufaidisha Wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siasa ya karne hii haiwezi hata kidogo kuwa ni siasa ya vurugu, kuwa ni siasa ya mapambano, kuwa ni siasa ya mapinduzi ya maandamano, ya vurugu, ya namna yoyote ile ambayo siyo ya amani. Siasa ya leo hii ni uchumi. Tunajadili bajeti hapa, lakini sina hakika kama ndugu zangu Wana-Arusha, wanapata fursa ya kusikiliza namna ambavyo tunajadili bajeti ambayo itawakomboa wao kiuchumi. Wapo katika hali ya mabomu, wapo katika hali ya mashaka, kazihaziendi kule Arusha; tunaomba sana sisi Viongozi wa Kisiasa, tujichunge tuliongoze Taifa hili, tuweze kudumisha amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika enzi ya uhai wake aliojaliwa na Mungu, aliwahi kuandika Kitabu kilichoitwa kwa jina la "Tanzania Itajengwa na Wenye Moyo".

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema wale wenye moyo ambao walitamkwa na Mwasisi wa Taifa hili, wewe ni mmojawapo. Kwa kipindi chote ambacho nimeingia katika Bunge hili, nilikuwa ni mionganoni mwa Wabunge ambao

walikuwa wanapinga mfumo ule ambao tulikuwa tunaenda nao kibajeti. Hii ilikuwa ni changamoto kubwa, lakini niseme tu kwamba, wewe ni mwanamke wa shoka, umeweza kulisimamia hili na tumeweza kufanikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tukirudi katika bajeti ambayo imewasilishwa hapa na Waziri wa Mipango pamoja na Mahusiano na Uratibu na Waziri wa Fedha, niseme tu kwamba, mfumo wa bajeti bado una matatizo; kwanza, huu utaratibu wa kutoa vipaumbele. Serikali kwenye kutunga bajeti, kila Halmashauri, kila Mkoa wanapewa *ceiling*, wao ndiyo ambao wanajua ni vitu gani vina umuhimu kwa wakati huo, lakini inapokuja huku kwenye kuweka bajeti tayari inazuiwa wanasema kwamba, katika hili sisi tumeweka *ceiling* hii.

Mheshimiwa Spika, mnaweza mkawa mmetupangla sisi kutupa matrekt 100, lakini mahitaji yetu siyo matrekt 100. Sasa naomba Serikali, ikubaliane na matakwa ya Wataalam kutoka kwenye ngazi za Halmashauri na Mikoa, kwa vipaumbele ambavyo wanaviainisha kwa ajili ya maendeleo ya maeneo wanayoyaongoza. Hii itasaidia kukuza na kuharakisha maendeleo katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi kwa mfano, kwenye Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mahusiano kuhusu hali ya uchumi, ameainisha hapa kwamba, kuna mtawanyiko katika eneo la Mkoa wa Lindi ni 1/14; ndiyo eneo ambalo lina mtawanyiko mdogo kuliko maeneo mengine yote. Sasa hivi mmeshawahi kujiuliza ni *factor* zipi zinazosababisha watu wengi wasipende kuishi katika Mkoa wa Lindi? Sababu, hakuna miundombinu ya kutosha. Tunapohitaji mahitaji ya zahanati, vituo vyaya na shule, tunaambiwa kwamba, pesa tulizozitenga safari hii ni kwa ajili ya kukuza kilimo; sisi tumekuwa tukilima kabla hata hii nchi haijawahi kuitwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa hapa ni kuhusiana na *inflation*. Hii *inflation*, mimi ninaitafsiri

siyo mfumko wa bei, Tanzania kuna bei ya mfumko; kwa maana kwamba, bidhaa zinapandishwa bei kiasi ambacho hazihimiliki. Serikali kila mwaka inapanga kutoa *exemption* kwa ajili ya bidhaa za chakula kuagiza nchini, lakini usimamizi wake unakuwa ni duni na hafifu. Mfano mzuri, mwaka jana ambapo tulitoa vibali vya kuagiza sukari kutoka nje ni kampuni moja tu ya *Mohamed Enterprises*, ilikubali kuuza bei ambayo ilitamkwa na Serikali ya shilingi 1,700, wengine wote sukari ilifikia mpaka shilingi 3,500. Tunatoa misamaha ya kodi hii kumnufaisha nani? Sasa hili ni eneo ambalo lazima tuliangalie kwa umakini na tuangalie ni jinsi gani ambavyo tunaweza kuweka mfumo mzuri wa kudhibiti mianya hii ya uvujaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la mapato, Serikali imezungumzia jinsi ambavyo imeweza kukabiliana na udhibiti wa uagizaji bidhaa na ukiukwaji wa kodi. Jambo moja ambalo najiuliza; wakati tunadai uhuru wa nchi hii, jambo kubwa ambalo liliwahamasisha Wananchi walieleza kuhusu umuhimu wa kutokulipa kodi, tukipata uhuru wetu hatutalipa kodi. Sasa leo hii tumeshakuwa huru, tunahitaji Wananchi washiriki kwenye kulipa kodi, ili tujenge uchumi wetu. Kwenye bidhaa zinazoagizwa nje, jambo la msingi ambalo naionba Serikali ifanye utafiti, wafanyabiashara hawajajenga utamaduni wa kuwa wakweli kulipa kodi kama walivyo wafanyabiashara wa nchi nyingi nyingine Duniani; mmeshawahi kutafiti? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, bei ya bidhaa zinazoingia hapa nchini zinatozwa ushuru kwa kutokulingana na thamani halisi ya ununuzi. Sisi tunafuata viwango vya kimataifa, tunanunu vitu Asia huko, ambavyo *quality* yake haiwezi kuwa ina ushindani katika *World Market*, ambapo na sisi ndiyo tumetumia kama *base* yetu. Kwa hiyo, naomba tuweke kodi ambazo ziko *reasonable* ili Wananchi wengi na wafanyabiashara wengi, waweze kushiriki na kukubali kulipa kodi bila shuruti.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa. Mwaka jana na mwaka juzi, bajeti yetu tumekuwa tunalenga kulipa madeni

ya ndani, lakini bado wadai wengi, wazabuni wengi, wanadai katika Idara mbalimbali za Serikali. Sijui ni sababu zipo zinazosababisha pesa zinatengwa, lakini bado madeni yanaendelea kuwepo. Hebu Serikali ichukue jitihada za makusudi kuweza kufanya tathmini ya watu ambao wanadai kwa zabuni walizotoa, tuweze kujua uhalisia.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilzungumzie, naipongeza sana Benki ya *Stanbic*, kwa jinsi ambavyo imeweza kuisaidia Serikali, kwenye ile *syndicate loan* ambayo walifanya, ambapo tumeweza ku-*raise 600,000,000 dollars* zitakazosaidia kukuza sekta nyengine, hasa umeme na barabara. Nilisoma gazeti moja wiki mbili au tatu zilizopita, nimeona kwamba, Serikali imefanikiwa kuweza kushawishi kupata *sovereign bond* za bilioni mbili. Naomba tu nii-*caution* Serikali, *sovereign bonds* zina matatizo yake; matatizo ambayo nchi kama Ugiriki, Hispania na Ureno wanayapata, yanatokana na hili. Kwa hiyo, tusikope pesa, tusiende tuka-*raise funds* huko nje kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Tuwekeze katika miundombinu na tuwekeze katika maeneo ambayo yatakuwa na ustawi katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, katika sekta muhimu za Afya, Elimu, Jeshi, Polisi, lazima tuweke umuhimu sasa wa kuwalipa mishahara ambayo inakidhi. Malalamiko katika sekta hizi muhimu yamekuwa mengi na ninaona tunaweza tukaumiza uchumi wetu kama tusipoyazingatia na kuyaweka vizuri. Katika hili kumekuwa na malalamiko makubwa sana, hasa katika eneo ambalo ninaliwakilisha pale Kilwa; Walimu na Watumishi wa Afya, wanakopeshwa mikopo katika taasisi hizi za kifedha kwa *interest* kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninajuliza ni kwa nini *NMB* ambapo ndipo mishahara yao inapitia, isifanye kazi ya kuwakopesha watumishi hawa? Mtaji wa Serikali uliokuwepo ni kwa ajili ya kitu gani? Lazima tuangalie namna, kwa kuwa wale wanatumia mfumo huohuo wa *ku-deduct* pesa zao kila wanapolipwa mishahara kwa mwezi.

Wanakopeshwa katika *rate* ya zaidi ya asilimia 30, hii ni hatari, tuwaokoe watumishi na tuweze kuwapa nafasi nzuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, mapato yanayotokana na rasilimali za nchi yetu. Nimemsikia Mheshimiwa Rais, amezungumza siyo chini ya mara mbili na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, aliwahi kulizungumzia hili; ni lini Serikali itakuwa tayari kuanzisha *sovereign fund* au *heritage fund* kwa ajili ya mapato yanayotokana na gesi, *uranium*, pamoja na makaa ya mawe? Kwa sababu, pesa hizi hatuwezi kuingiza kama ni matumizi ya kawaida, lazima itumike kwa ajili ya kuendeleza Wananchi wetu na tuweze kuokoa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunavyo viwanda vya korosho na hilli tunalielewa, tunaltaka sasa Serikali itusaidie. Tumekuwa na matatizo ya korosho, mwaka huu mmeona matatizo sehemu mbalimbali. Viwanda ambavyo wameshindwa kuviendeleza, basi Serikali ivirudishe ili tupate wawekezaji wengine au Serikali yenye we iwekeze. Vilevile wale ambao wamepewa vile viwanda na wanao uwezo wa kuviendesha, kwa nini Serikali inachelewa kutoa idhini ya hawa watu kukopesheka, kuwa na mitaji ya kuendesha hivi viwanda? Kuna tatizo kubwa sana la viwanda kutokuwa na mitaji ya kutosha kuweza kuijendesha na vilevile mitaji ya kuweza kununua korosho kutoka kwa wakulima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa asubuhi hii, naona huyo alikuwa Msemaji wetu wa mwisho, naona dakika zimeisha. Tutakaporudi jioni, watakaochangia ni Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mheshimiwa Capt. Chiligati, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Koka, Mheshimiwa Diana

19 JUNI, 2013

Mwatuka, Mheshimiwa Martha Umbula, Mheshimiwa Charles John Mwijage na Mheshimiwa Kayombo. Ndiyo hao na wengine watatajwa mchana.

Mimi sina matangazo mengine, naomba tusitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilitfungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya hoja iliyoko mbele yetu na kwa mujibu wa utaratibu na kwa mujibu wa taarifa niliyoipokea kutoka kwa Mheshimiwa Spika, wafuatao walishatajwa kuwa wachangiaji wa mwanzo. Kwa hiyo, nitaanza kuwaita hawa ambao Mheshimiwa Spika alishawaandaa kuchangia hotuba hii kwa jioni. Ilikuwa tuanze na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, naona hayuko ndani ya Ukumbi wa Bunge, basi nitamwita Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan ajiandae na Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati ajiandae.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia uzima na afya njema hadi na mimi nachangia bajeti hii ya mwaka 2013/2014 na nikiwa mtu wa kwanza kwa jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka niikumbushe Serikali kwamba, nchi ya Rwanda ambayo ilikuwa katika machafuko makubwa na vita vyatengenezewa kwa wenyewe, bajeti ya maendeleo mwaka huu ni asilimia 50 na sisi ndipo hapo tulipo, tumepitwa na nchi ndogo kama ya Rwanda ambayo ilikuwa katika machafuko. Tunajifunza nini? Kazi kwetu sisi kama Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze sasa kuchangia. Kwangu mimi nilikuwa najiuliza uko wapi mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwenye Sekta ya Uvuvi? Mwaka huu wa 2013/2014 Serikali imedhamiria na imepanga kuanzisha mashamba, vitalu na vituo saba vya kufuga samaki. Cha kushangaza, sehemu ambayo imetengwa katika kufuga samaki hao ni shilingi 217 milioni; najiuliza hivi ni kweli shilingi milioni 217 zinaweza kutosha kiasi gani kuweza kufuga samaki katika vitalu hivyo au ni kutania Tania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri hili aliangalie kwa makini sana. Huwezi kufuga samaki, ukaanzisha tatizo hili kubwa katika hali ya kuwakomboa wavuvi ambaو wengi ni maskini ukapeleka shilingi milioni 217, ni kuwatania. Wavuvi ni masikni, lichukue, liangalie na andaa mazingira mengine ya kutafuta fedha ili uboreshe nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Tanzania kama nchi kubwa, Vietnam wenzetu wana mashamba ya kufuga samaki zaidi ya 100; najiuliza hivi sisi kama tunakwenda mara nyingi huko nje na tunapata elimu ya kutosha; ni kwa nini basi Mheshimiwa Waziri asiandae mazingira ya kufikia angalau mashamba 50? Hili namwambia Mheshimiwa Waziri, aliangalie kwa mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 ukuaji wa uchumi katika Sekta ya Uvuvi ilikuwa na asilimia tano, lakini mwaka 2012 ukuaji wa uchumi ilikuwa na asilimia 2.9 tu, tumeshuka. Hili ni jambo moja kubwa, tunapoweza kushuka katika sekta hii ambayo ni muhimu, basi kuna haja ya kuangalia ni mipango gani iliyoweza kushusha asilimia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende kwenye utalii. Tanzania ni nchi ya pili Duniani kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii ikitanguliwa na Brazil. Kwa mujibu wa *World Economic Forum*, mwaka 2011 Tanzania tulikuwa kwenye nafasi ya 110, mwaka 2012 tulikuwa kwenye nafasi ya 109, lakini wenzetu Kenya mwaka 2011 walikuwa kwenye nafasi

ya 103, mwaka 2012 wenzetu Kenya walikuwa kwenye nafasi ya 99 kwa kuingiza wageni wengi na kuingiza fedha nyingi kwa ajili ya utalii. Mimi najuliza tatizo nini kwetu; hivi bado hatujifunzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi, fedha za kutangazia utalii hazitolewi, kuna malalamiko makubwa kwenye Balozi zetu hata pale ambapo wao tunawaambia waandae mazingira ya *Economic Diplomacy* watafanya nini wakati fedha hatuwapi? Mabalozi wetu nchi za nje wanalalamika sana kwamba hatuwapatii fedha hata za kufanya makongamano na warsha. Inakuwaje leo unasema tunapanga mpango wa kuweza kuendeleza utalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo, lakini siyo hilo tu, sisi hatuna ndege, wenzetu Kenya wana *Kenya Airways* mpaka Ulaya wanakwenda na kurudi, wanavutia. Ingawa hiyo sisi hatuna ni tatizo; tumejifunza nini kwetu? Tunapiga kelele siku zote, lakini Serikali bado naona haijachukua hatua madhubuti za kuweza kuiimarisha sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, hata zile fedha ambazo tuna maeneo, tuna watalii, hatuna udhibiti wa fedha. La kushangaza sana, jambo ambalo mimi silihendi hata kidogo, ukienda kule Millan Italy, watalii wanaoondoka kule tumemuweka Mzungu mmoja ndiyo anayekusanya fedha, watalii wanakuja huku, baadaye anatupa anachotaka yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo, Millan Italy na jina la mzungu mimi nalihofadhi, kwa sababu ninyi Serikali ndiyo mlimuweka nyinyi mnaomjua; shauri yenu, tunapiga kelele siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye kilimo, tulikuwa na kauli nyingi tu Siasa ni Kilimo, Kilimo Utii wa Mgongo, KILIMO KWANZA mwaka huu, lakini mpango wa Serikali wa kuthaminisha mazao ya kilimo uko wapi. Bado siuoni, nilitarajia mtakuja na majibu kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda alivyotuambia Bungeni

hana kwamba, bajeti inayokuja ya Serikali, Bajeti Kuu, itakuwa na mpango wa kufufua viwanda vilivyokufa ili kuboresha maisha ya Watanzania kuthaminisha mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mpango wa kufufua viwanda vilivyokufa haupo na tulimwuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda kwa wakati ule akasema, bajeti hii kuna mpango mahususi ambao ukifika tutaona vile viwanda vyote ambavyo Serikali mlivichukua mkawauzia Vigogo wa Serikali, baadaye utaratibu wa kuingia ubia na baadhi ya mashirika ya kijamii kuweza kuvifufua. Lakini ni aibu tupu, alituambia Mheshimiwa Waziri atawaita wale wote aliowapa viwanda ili wakae pamoja waone namna gani ya kuweza kuboresha. Jamani kilo moja ya korosho safi ni shilingi 20,000, korosho ghafi haziwasaidii Wananchi wa Lindi na Mtwara. Umaskini wa Lindi na Mtwara unachangiwa na Serikali, kwa sababu mlipeana viwanda Vigogo wa Serikali na mmesema mtawaita lakini wapi maskini mnaogopana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikopa dola milioni 20 kutoka nje mwaka 1970 mpaka 1980 kutoka Italia na Japani, tukasema kwamba mnajenga viwanda, lakini mnashindwa kuwaita. Mlituambia mtawaita hamjawaita na naomba mniambie Kiwanda cha Mtwara Mjini, Taasisi ya Fursa kwa Wote ni Kigogo wa Serikali, mtu wa juu kabisa wa Serikali mmeshindwa kumwitwa mnaoneana aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Newala One* mmechukua Vigogo wa Serikali, kiwanda hiki mmepeana wenyewe kwa wenyewe, hamjathubutu kuwaita; militudanganya Bungeni. Masasi ni ninyi wakubwa wa Serikali hamjawaita. Nachingwea nako ndiyo hasa kumeoza. Mtama ndiyo kabisa. Tatizo nini Likombe, Lindi Mjini, Kibaha tatizo nini na kwa nini msiwaite Mheshimiwa? Thamani ya mazao iko wapi, leo uko wapi mpango wa kufufua *SUNGURATEX* umekufa, *MBEYATEX*, *MUTEX*, *KILITEX*, *MWATEX*, *Morogoro Polytex*, vyote vimekufa na mltuambia mna mpango madhubuti wa kwenda kufufua viwanda ili kukuza uchumi na kuwapatia

ajira Wananchi. Uko wapi mpango huo, mimi siuoni naona kizaaza tu mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, katika hili Wananchi wanalamika Serikali imeshindwa kudhibiti bidhaa bandia na bidhaa feki. Bidhaa feki ni nyingi, Wananchi wanaonunua mabati wanalamika, baadhi ya mabati hayana *TBS*, hayana muhuri wa *TBS*; tatizo nini? Nyaya za Umeme zinaharibu nyumba za watu, nyumba zinaungua, ukija kwenye mabati kuna viwanda kibao. Mimi naomba uniambie kuna kiwanda cha Wachina Vingunguti, ndani yake kuna Kiwanda cha Korosho, *Premium Cashew Nuts*, kinajulikana kwa jina la *Dragon Roofing Sheet*; mabati hayana nembo ya *TBS*, yana migongo minne, unaponunua hupewi risiti na Mchina anakwambia wewe nenda beba tu *ching chang*, bei nafuu ninyi mnajua wenyewe mnakaa tu Wananchi nyumba zinavuja shauri yenu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kingine kipo Kurasini kule nyuma ya Chuo cha Diplomasia, nacho ni kwa ajili ya kuunganisha aina ya pikipiki ya T-belta. Ukiingia getini utakuta mtambo wa kutengeneza mabati, vilevile kuna dada wa Kichina nipe risiti, beba tu bei nafuu; jamani, hamjui kweli ninyi au mnatuminyia minyia kibongo mbona hatuelewi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, tatizo kubwa lilitopo hivi sasa ni rushwa. Udhibiti wa fedha za umma haupo na hili ni eneo ambalo liliipigiwa kelele sana. Mwaka 2006 Serikali imepoteza bilioni 2.3, mwaka 2007 tumepoteza bilioni 3.5, 2008 bilioni 3.1, 2009 bilioni 11.1, 2010 bilioni 12.9; bilioni 33. Upotevu wa fedha za umma, ufisadi uliokithiri Tanzania, hiyo bilioni 33 ndiyo eneo hilo; tatizo nini?

Tunaposema hapa jamani ni kwa nini Serikali haichukui hatua kwa wale wote waliobainika na ufisadi huu, tuko katika mchakato jamani. Wale wanyonge wa Mungu, wanaochukua vitu vidogo vidogo tu wanafungwa miaka minne, miaka mitano, wamejaa magerezani tunawasemea

sisi wanyonge mbona hao matajiri wanaoonekana wanachukua mabilioni haya hawafungwi; tatizo nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napata mashaka makubwa sana kwenye eneo hilo. Ikiwa Serikali inaruhusu kuwaachia mafisadi wakubwa, lakini wale wadogo wadogo wanabanwa, hili ni tatizo kubwa. Naiomba Serikali ikae makini, ichukue hatua madhubuti na wale mafisadi wakubwa, mafisadi papa, wachukuliwe hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofii*)

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii. Naungana na wenzangu kupongeza utaratibu ambao umetumika hivi sasa wa bajeti yetu, kupitisha bajeti yetu hii. Zaidi, napongeza pale ambapo kulikuwa na upungufu kwenye baadhi ya Wizara, kwa makusudi kabisa Serikali ilikubali kuongeza fedha na hasa kwenye suala la maji, ni tatizo kubwa sana na lipo karibu nchi nzima. Mimi wa Dar es Salaam nimelifurahia sana, kwa sababu fedha ambazo zimeongezwa, nina hakika Miradi ya Maji katika Jiji la Dar es Salaam itakamilishwa kwa wakati, haitakuwa hadithi tena, kwa sababu tatizo la maji lilikuwa ni kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo tunalo kwenye bajeti hizi kila mwaka ni matumizi ya Serikali. Matumizi ya Serikali yamekuwa makubwa sana na hata baadhi ya fedha za miradi ya maendeleo zinapokuwa hazikupatikana, lakini fedha za matumizi ya kawaida hizo lazima zipatikane, lakini kwenye miradi ya maendeleo huku fedha hazitapatikana, utaambiwa fedha hazijafika na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba sana hebu tujaribu kuangalia matumizi ya Serikali ni jinsi gani tutaweza kuyapunguza, kwa sababu matumizi yamekuwa makubwa sana. Nitoe mfano tu miaka ya 80 wakati wa Mwalimu Nyerere na wakati huo Makatibu Wakuu wa Wizara

walikuwa wanatumia magari madogo haya ya *Saloon*, *Nissan Globatt* na wakati huo kutoka mjini kuja Magomeni unatumia nusu saa, Jangwani barabara ilikuwa mbovu mno, lakini yalitumika magari hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, imejenga barabara takribani nchi nzima kama anavyosema Mheshimiwa Magufuli, unaweza kutoka Mtwara mpaka Bukoba kwa bajaji; lakini sasa ndiyo tumeongeza kutumia magari makubwa ya kifahari, yenye thamani kubwa mno na siyo thamani tu ya kununua, lakini hata kulitengeneza hilo gari.

Fedha ambazo zinatumika kwenye matengenezo ya magari ni nydingi sana, lakini fedha zinazotumika kwenye ununuzi wa mafuta ni nydingi zaidi. Kwa hiyo, tuangalie ni jinsi gani sasa tutaweza kupunguza matumizi kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeamua hapa kwamba sasa magari ya *CC 3000* yatumike, lakini *CC 3000* ndiyo unazungumzia Prado, ni magari hayo hayo ya thamani kubwa, yanatumia mafuta kwa wingi sana. Mimi ningombaa sana, tuangalie uwezekano wa kurudi tena chini, wenzetu Wakenya wameweza wanatumia magari ambayo hayazidi *CC 2000* nafikiri na sisi pia tunaweza kufika huko. Twende taratibu ili tuone ni nani anatumia gari ya *CC 3000* na nani atumie gari la chini ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Waziri atumie gari la *CC 3000*, Mkuu wa Idara naye anatumie gari la *CC 3000*, Rais anatumia *VX*, Mkurugenzi wa Halmashauri naye *VX* hilo hilo; sasa huwezi kutofautisha, imekuwa kama kambale, baba ana masharubu na mtoto ana masharubu na mama ana masharubu. Kwa hiyo, lazima tuone tunakwendaje kwenye hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningeomba kukizungumzia ni suala la mfumko wa bei, mtaani bei ziko juu sana, vitu vina bei kubwa sana na hii inasababishwa na wafanyabiashara kubanwa na wanabanwa kwenye maeneo mengi sana kununua bidhaa hizi. Sasa anapobanwa ye ye huko naye anakuja kuwabana Wananchi, mwisho wa siku anayeumia sana ni Mwananchi wa chini. Mfanyabiashara ye yote anayefanya biashara lazima aende benki akakope. Hebu sasa angalieni riba za kwenye mabenki na hakuna jitihada zozote za Serikali kuweka utaratibu kwamba hivi sasa jamani ukomo wa riba uwe ni kiasi fulani, asilimia fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo unakwenda mahali kwenye mabenki, mikopo mpaka asilimia 24, asilimia 22, sasa mfanyabiashara atachukua mkopo lakini mwisho wa siku anakuja kumwumiza Mwananchi ndiye anayeumia. Kwa hiyo, tuweke utaratibu tu kwamba, jamani mabenki yetu haya sasa asilimia 15 iwe ndiyo mwisho wa riba tusizidi hapo.

Kinyume cha hivyo, tutakwenda kuwaumiza Wananchi wetu, bajeti zitakuja lakini anayeumia sana ni Mwananchi wa chini. Kwa hiyo, tuone ni jinsi gani tunaweza kumsaidia na ni karibuni tu mmesikia mabenki yanavyotangaza faida, benki inatangaza kwa mwaka inapata faida ya zaidi ya bilioni 50 au 60. Sasa jiulize bilioni 50 au 60 anazozipata mwenye benki; ni kwamba, kawaumiza Wananchi, ndiyo maana ye ye anapata faida kubwa kiasi hiki; ni faida kubwa kuliko inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana tuangalie hilo ili mambo yaende vizuri, Wananchi wetu waweze kupata unafuu wa vitu mbalimbali. Siyo hilo tu, kuna suala la matumizi ya fedha hizi za Kitanzania (Shilingi). Maeneo mengi hivi sasa ukienda watu hawakwambii ulipe kwa shilingi wanakwambia ulipe kwa dola na hili limekuwa kubwa sana na ukienda kwenye maduka ya kubadilishia fedha wenye maduka ndiyo wanaopanga fedha wauze kiasi gani siku

hiyo. Hakuna utaratibu maalum ambao umewekwa na Serikali kwamba, shilingi yetu thamani yake ni hii, wenye maduka ya kubadilishia fedha wasizidi kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenye maduka ya kubadilisha fedha anaamua tu leo nibadilishe kwa shilingi ngapi na kesho nibadilishe kwa shilingi ngapi; na faida wanayoiweka wao ni kubwa sana tofauti na nchi nyingine. Kwa hiyo, naomba na hili nalo mliangalie ili kuwarahisishia Wananchi wetu waweze kupata unafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni bidhaa zisizokuwa na viwango. Tumeona ni juzi tu Dar es Salaam lilianguka ghorofa pale na uchunguzi unaendelea, lakini unawenza ukaangalia tu nondo iliyotumika pale ina ubora uliostahili. Twende kwenye simenti ambayo inatumika, nayo ina ubora unaostahili. Siyo hilo tu, kaangalieni na matofali yanayotengenezwa hivi sasa yana ubora au mradi tofali tu, kwa sababu unakwenda kuangalia tofali ni mchanga mtupu.

Nakumbuka zamani Kiwanda cha Saruji Wazo walikuwa wanatengeneza matofali, lakini mfuko mmoja wa simenti wa kilo 50 utatoa matofali yasiyo zidi 25, kati ya 18 mpaka 25. Leo mfuko mmoja huo huo wa simenti unatoa matofali kati ya 40 mpaka 50. Kwa hiyo, tofali unalikuta mchanga na tumekaa tunaachia majumba yanaporomoka. Ninafikiri na huko pia twende tukaangalia ili tuhakikishe Wananchi wetu hawanunui bidhaa ambazo siyo imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo bidhaa hizo za ujenzi tu, yapo mambo mengi; kuna madawa na vyakula ambavyo vinaingizwa. Juzi tulikuwa na watu wa konyagi nao wanaonesha jinsi pombe hizi zinavyoingizwa nchini kinyemela tu, hazina viwango, hazina *TBS*, hazina chochote, lakini zinaingizwa Wananchi wetu wanakunywa na nyingine ni sumu.

Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe tunawalinda wananchi wetu kwenye masuala ya vyakula, vinywaji na dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ulinzi, tumeona ambayo yametokea hivi sasa, nimekuwa nikipigia kelele siku zote juu ya nyumba za Askari. Leo tunavyozungumza, Askari Mtware walikuwa hawakai kwenye nyumba zao, nyumba zao wanazoishi zinachomwa moto, kwa sababu tu ya vurugu ambayo imetokea. Kuondoa tatizo hili, ni lazima tuhakikishe tunajenga nyumba za Askari. Sasa kwenye bajeti inayokuja tuangalie umuhimu wa kujenga nyumba za Maaskari kwenye makambi yao. Tusiruhusu Askari kuishi mtaani kwa sababu anashindwa kufanya kazi yake, kuna uwoga na mambo mbalimbali. Kwa hiyo, tuone jinsi gani tunawasaidia Askari kujenga nyumba kwenye *line*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tumeondoa kodi ya bodaboda, sawa, lakini unapoondoa kodi ya bodaboda, yule mwenye teksi unamweka wapi, kodi yake umepandisha na ndiyo gari ambazo tunazitegemea. Wajawazito watapanda teksi hawawezi kupanda bodaboda, lakini umeondoa kodi ya bodaboda ambapo yeye kwa siku anaingiza Sh.15,000 kwa tajiri na mimi ninazo, tena niseme tu ninazo bodaboda na mmeondoa kodi na mimi nafurahia, lakini mnawaumiza wananchi, wangeweza na wao kuchangia hata kidogo kwenye bajeti hii, lakini mmewaondolea kodi matokeo yake mnaendelea kuwaumiza wenye teksi ambazo ndizo zinazotakiwa na watu wengi wanapopata matatizo. Kwenye bodaboda huwezi kumpakiza mzazi, lakini mmeziondolea bodaboda, mwenye teksi mnazidi kumkandamiza, analipa kodi ya mapato, *road license*, analipa kituo anachoegeshea pale anakatwa na Halmashauri, lakini mwenye bodaboda yuko huru tu na baadhi ya wenye bodaboda hata leseni ya kuendeshea hawana. Mimi naomba hivi sasa kwa sababu bajeti siyo msaaifu, mwaka huu tumefanya hivyo, lakini mwakani tuangalie jinsi gani tunafanya kuweza kutatua tatizo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mfanyabiashara na ninaomba ni-*declare* na huwa naingiza mzigo kwa kontena. Kuna utaratibu ambao unatumika hivi sasa kwamba unapoingiza kontena nchini, unapotaka kwenda kuteremsha ule mzigo, unatoka na lile kontena, ili utoke na kontena unatakiwa uweke *deposit* ya dola na siyo shilingi, wanakwambia ulipe dola 2,000, unaweka dola 2,000 unashusha kontena mzigo wako, siku ya pili unarudisha kontena, ukirudisha unafuata sasa ile dola 2,000 hawakupi, hiyo fedha hurudishiwi, huu ni wizi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Barwany, naomba urudi ulikotoka, unavunja utaratibu.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wizi ambao unafanya na makampuni haya, *Maersk Line, Safmarine, Nyota Tanzania Limited*, wao ndiyo wanafanya hivyo. Sasa hebu fikiria kontena 30 au 50 zinazotoka kwa siku, kila mmoja amelipa dola 2,000 ni shilingi ngapi hizo kwa siku, kwa mwezi ni ngapi na fedha hizo hazirudishwi, ukim dai anakwambia oooh, lete *account number*, aah mimi nina akaunti ya dola ya nini, mimi sina akaunti ya dola, mimi nina akaunti ya shilingi, nirudishieni shilingi basi, kwa sababu nimekupa *deposit* dola 2,000 nirudishie hizo hawataki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushahidi hapa, fedha zimelipwa tangu mwezi Oktoba, 2012, mpaka leo hawataki kurudisha hizo fedha na ni watu wengi wamefanyiwa hivyo, lakini Serikali wanalijua na hawachukui hatua. Watu wachache hao wanazidi kutuumiza, wanaumiza wananchi wetu kwa sababu ukinibana mimi mfanyabiashara na mimi nakwenda kuwabana wananchi, mwisho wa siku tunawaumiza wananchi. Ningeomba sana Serikali iliangalie hili na ichukue hatua zinazostahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, mimi niseme tu naunga mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Azzan. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa John Zefania Chiligati anaafuatiwa na Mheshimiwa Chacha Nyambari Nyariba Nyagwine.

**MHE. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bajeti ilio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme kwamba naunga mkono bajeti hii na nitatoa sababu zangu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya matatizo makubwa tuliyonayo hapa nchini sasa hivi, ni kuongezeka kwa kasi kwa pengo kati ya walionacho na wasinacho, kati ya maskini na matajiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haihitaji kuwa muumini wa itikadi ya ujamaa kama mimi ili kuona athari za tatizo hili ambalo ninalolisema. Ni tatizo likiachwa likaendelea, kama hatua za kibajeti hazichukuliwi kulikabili tatizo hili, litazaa chuki mionganoni mwetu, litazaa uhasama mionganoni mwetu, litazaa mapambano ya kitabaka kati ya makundi haya mawili, jambo ambalo litakuja kuvuruga umoja wetu na amani yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Watanzania wengi hasa wafanyakazi wa kawaida na wakulima kule vijiji, mapato yao ni kidogo, wanashindwa hata kupata milo mitatu kwa siku, baadhi ya wenzetu walionacho, tangu Jumatatu mpaka Jumapili ni sherehe tu, tena za mamilioni, mara harusi, mara *sendof*, mara kipaimara, siku hizi hata mtoto akimaliza chekechea anakwenda darasa la kwanza, vilevile kuna sherehe ya mamilioni, Tanzania hiihii! Sina ugomvi na matajiri, wala kutajirika si jambo baya, ili mradi kama utajiri huo mtu ameupata kwa njia halali, kafanya kazi halali, kafanya biashara halali, ametajirika, si tatizo. Tatizo letu na changamoto yetu, ni kuwasaidia watu hawa wa chini kwa kuwawezesha kuititia Wizara ya Mama Nagu na wenyewe kuinua hali zao za maisha na bajeti ndiyo silaha yenyewe ya

kutufikisha huko. Chama kinachotawala, itikadi yake kubwa ni kusaidia wanyonge, ambao ni wakulima na wafanyakazi, sasa vitendo vyake lazima vionekane kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bajeti ya mwaka huu, imejitahidi kidogo na ndiyo maana naiunga mkono kutazama makundi haya, wakulima na wafanyakazi. Mfanyakazi wa kawaida yule ambaye ni mwaminifu, hali rushwa, hadokoidokoi mali ya tajiri wake, hana mapato huyu, mapato yake ni ule mshahara tu. Sasa mwaka huu kodi ya mshahara imepunguzwa kwa kutoka asilimia 13 kwenda 12, ni ishara nzuri ya huruma lakini mwakani hebu tuangalie vizuri eneo hili, tuwapunguzie mzigo hawa wafanyakazi. Namna moja ya kumuongeza kipato mfanyakazi, ni kupunguza ile kodi kwenye mshahara wake. Mwakani Waziri wa Fedha, hebu shuka fika kwenye 10 hata tisa, ili huyu mfanyakazi tumpe motisha ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima vilevile bajeti hii imewatazama na Serikali imesaidiwa na Waheshimiwa Wabunge kuongeza bajeti kwa mfano ya kilimo, kumsaidia mkulima. Zile fedha zilizowekwa mwanzo, baada ya sisi Wabunge kupiga kelele, Serikali imeongeza shilingi bilioni 21. Ni ishara nzuri, mwakani ongezeni zaidi ili wakulima tuweze kuwasaidia zaidi kuinua kilimo chao, mapata yao, ili pengo kati ya hao matajiri walichonacho na hawa amabao hawana tulipunguze badala ya kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka huu vilevile suala la maji hasa vijiji kule, wakulima vijiji kule, pamoja na fedha za awali, zile shilingi bilioni karibu 760, Serikali imekubali kuongeza zingine za nyongeza, shilingi bilioni 184, ni ishara nzuri kuwakumbuka hawa wakulima vijiji, ndiyo maana bajeti hii naiunga mkono. Kwa hiyo, vijiji vyangu, ile miradi iliyokuwa imekwamakwama kule, Mpapa kule, Chelejeho, Kitinku, Maweni, Ngaiti, kwa bajeti ya mwaka huu watakumbukwa. Kwa hiyo, lazima niiunge mkono bajeti hii, nikiikataa maana yake sitaki hawa wapate maji.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bajeti hii imewakumbuka wakulima vijijini hasa kwenye suala la umeme, Serikali hii, pamoja na fedha za awali ambazo zilikuwa zimepangwa karibu shilingi bilioni 153, imeongeza shilingi billioni zingine 186 ili umeme ufike mpaka vijijini. Ndiyo maana naiunga mkobo bajeti hii, ni ishara nzuri na mwakani Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, tuwakumbuke tena hawa wakulima na wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo lipo, ni kwamba je, hizi fedha ambazo tumeidhinisha, zitafika zote? Maana hapa tunaidhinisha karatasi tu, je zitafika zote. Sasa ili zifike zote, ni lazima makusanyo ya Serikali yawe makubwa, kwa sababu tusipokusanya, hii bajeti itabaki kwenye makaratasi, tatizo letu bado liko katika makusanyo. Tatizo la kwanza, Watanzania tulio wengi, mtazamo wetu kuhusu kodi, bado ni mtazamo hasi, bado ni mtazamo wa kukwepakwepa kodi. Sasa tunataka Serikali ijenge barabara, iboreshe elimu, iboreshe huduma za afya, itafanyaje bila mapato! Tunataka haki, lakini wajibu wetu wa kulipa kodi bado tuko nyuma sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, hebu tuanzishe hasa elimu ya uraia kuhusu wajibu wa raia kwa Serikali yake. Haki zetu tunafundisha sana lakini je wajibu? Kulipa kodi ni sehemu ya wajibu. Mtanzania yuko tayari hata kumsaidia yule ambaye anakwepa kodi. Unafika dukani, anakwambia shati hili ukitaka risiti Sh.20,000, bila risiti Sh.18,000, mwizi huyu. Sasa wewe unafurahi Sh.18,000, lakini amekwepa kodi huyu ambayo ingeongeza huduma za elimu, maji, umeme, haya ni mambo ambayo naomba Serikali tuzidishe elimu ili Watanzania tujue kwamba kulipa kodi ni kuchangia maendeleo yetu wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mapato, kuna baadhi ya vianzio bado Mheshimiwa Waziri hujakusanya vya kutosha. Kwenye sekta ya mawasiliano, mawasiliano ni sekta inayokua kwa asilimia 20, lakini kuchangia kwenye pato la Taifa ili hela na sisi itufikie huku mitaani, imechangia asilimia mbili tu, ndizo fedha ambao zimeingia kwenye pato la Taifa,

asilimia 98 zimekwenda wapi? Hujakusanya Mheshimiwa Waziri. Naomba sana tazama, kama kuna sheria inayokuzuia usikusanye ama taratibu, ama mikataba, tulitazame ili eneo hili litoe mchango stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini, Mheshimwa Waziri hujakusanya ya kutosha, ni ng'ombe ana maziwa mengi, lakini hujakamua yote. Madini kwa mwaka jana ni sekta ambayo imekua karibu kwa asilimia nane, lakini mchango wa madini kwenye pato la Taifa ni asilimia tatu tu. Hujakamua vyta kutosha hapo Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunaomba ukamue ili tupate fedha nyingi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini liko eneo lingine la ardhi, hili ndiyo hujakamua kabisa, kwa sababu huyu ni ng'ombe ana maziwa mengi, hujamkamua kabisa Mheshimwia Waziri. Ardhi kule India, kwa miaka mingi ilikuwa ndiyo chanzo namba moja cha kukusanya mapato ya Serikali ya India, kwa miaka mingi sana. Mpaka ardhi ikawa chini ya Wizara ya Fedha, kwa sababu ilikuwa ndiyo chanzo namba moja kuingiza mapato. Walichofanya India, ardhi yote waliipima, wakamilikisha. Sasa ukishapima ardhi ndiyo umeipa thamani, kwa hiyo, yule unayemmilikisha sasa utatoza kodi, kama ardhi hujapima, hujamilikisha, huwezi ukatoza kodi. Kwa hiyo, wakatoza kodi kwa sababu walipima na yule aliyepata hati miliki alinaitumia hati miliki ile, sasa anakopesheka, anapata mitaji, anapata mikopo, wanazalisha, Serikali inakusanya kodi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwetu, hatujapima ardhi yetu, ndiyo maana hukusanyi chochote katika ardhi, ukiondoa eneo la maji, ardhi sasa ambayo haina maji, ni karibu *squire kilometers* 800,000. Sasa kuzipima hizo lazima kutumia picha za *satellites*. Sasa hivi tunanunua, mwaka juzi tulikuwa tunapima kule Wilaya ya Bariadi na kule Babati, kununua picha ya *satellitesili* upime ile ardhi ni ya ghali, Wilaya mbili tu zilitugharimu karibu mabillioni, je, sasa Wilaya 159 sijui bilioni ngapi! Ndiyo maana mwaka 2010, Bungeni hapa Serikali ilileta wazo na likakubalika, tuwe na kituo chetu

wenyewe cha kupokea picha za *satellites*, badala ya kununuanunua, sisi wenyewe tuwe na kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile wazo lilikubalika, lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hujatoa fedha kwa ajili ya kuanzisha hicho kituo cha kupokea picha za *satellites* na tukasema hicho kituo kijengwe hapa Dodoma (*UDOM*), ili picha za kupima ardhi yetu tuzipokee hapahapa na kile kituo vilevile kitawasaidia wanafunzi wa *UDOM* wanaosomea mambo hayo ya picha za anga, sasa hivi picha hizi tunazinunua nchi za nje. Mwakani Mheshimiwa Waziri, tunaomba zile fedha kwa ajili ya kuweka kituo cha kupokea picha za *satellites*, kijengwe, ni kama shilingi bilioni 15 na si zote zitatolewa kwa mwaka mmoja, unazigawa, kwa sababu kile kituo hakijengwi kwa mwaka mmoja. Kuna baadhi ya vifaa, ukiagiza leo utakipata baada ya miezi tisa. Kwa hiyo, katika miaka miwilii unaweza kabisa kuanzisha kile kituo, tukatenga fedha za kupima ardhi, tukapima ardhi yetu, tukaimilikisha, ili uweze kukusanya mapato ya kodi ya ardhi.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa Namwita Mheshimiwa Chacha Nyambari Nyangwine atafuatiwa na Mheshimiwa Hilda Ngoye.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema kwamba nitaunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100 na vilevile nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mambo mazuri ambayo inayafanya, hata

kama wenzetu hawaoni, lakini inafanya mambo mazuri sana, barabara na vitu vingine vingi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la amani katika nchi yetu. Suala la amani katika nchi yetu liko mikononi mwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na wale wote ambao wanavuruga amani, mimi naomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kabisa kwamba amani inakuwepo katika nchi hii ya Tanzania. Hilo ni jambo la msingi na kila mmoja wetu lazima tulisemee na tulikemee kwa hali na mali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kunisiaidia katika mambo fulani fulani Tarime, hasa katika suala la barabara na umeme. Kuna tatizo kubwa la maji, Serikali kwa sababu imeongeza fedha na juzi nimeona wanazindua mradi wa maji kule Tarime, naomba hizo fedha kwa kweli ziende Tarime, zitatue tatizo la maji, mambo yote yatakuwa ni mazuri hasa upande wa suala la afya na la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Tume ya Bei nchini Tanzania. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango msikilize suala hili, hapa Tanzania hatuna Tume ya Bei na hali hii imepelekea kila mmoja kujiuzia jinsi anavyotaka yeye mwenyewe. Kalamu hii utakuta kwenye duka fulani inauzwa Sh.500, ukitoka duka la jirani inauzwa Sh.2,000, huu ni wizi na hii ndiyo inayoleta matabaka katika nchi yetu. Tunaomba kwa kweli Serikali iamue, maana kupanga ni kuchagua, wale walioondoa Tume ya Bei wakasema kila kitu huria, kwa kweli siyo huria kwa kila kitu, tunaumiza watu maskini, naomba tuanzishe Tume ya Bei ambayo itadhibiti kila kitu katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa tofauti kidogo na wale Wabunge ambao wanasesma kwamba Watanzania wasilipe kodi, nchi yoyote ile haiwezi kuendelea kama mtu halipi kodi. Yeyote anayefanya biashara ali pe kodi, nasisitiza ali pe kodi ndiyo tutaendelea, kwa sababu katika nchi yoyote ile tunazoziona zilizoendelea watu walilipa kodi.

Nenda kwa mfano China, wanalipa kodi ya Serikali, kila mtu anajituma tu kuhakikisha kwamba analipa kodi bila kulazimishwa, lakini sisi hapa mara tunaondoa kodi kwa baadhi ya watu, tuwasamehe kidogo lakini walipe, hapo ndipo wataona uchungu, lakini tunaposema kwamba tunawaondoa kabisa kila kitu burebure, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba kila mmoja alipe kodi, hata kama ikiwezekana, hata kuna baadhi ya madhehebu ambayo yanafanya biashara, ikiwezekana walipe kodi, kwa sababu haiwezekani mtu akaanzisha dhehebu siku moja, ya pili, ya tatu unamwona ametajirika, *TRA mnafanya kazi gani?* Walipe kodi, hapo ndipo tutaweza kujenga nchi na nchi ikaendelea, lakini kama tutakuwa tunasema kwamba tunawaonea watu kulipa kodi, sijui tutarithi nchi ya aina gani ambayo tutaendelea kuiongoza. Naombeni tuhakikishe kabisa kwamba kila mwenye uwezo wa kufanya biashara na anayefanya biashara na alipe kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaenda sambamba na misamaha ya kodi kwa wawekezaji. Mheshimiwa Waziri wawekezaji wanansikia, wawekezaji wanatunyonya, naomba muwawekee sera ya kulipa kodi, hawawezi wakaja wakachuma katika nchi hii, wakaondoka, wakaifanya nchi ya Tanzania kama shamba la bibi, hilo kwa kweli Mheshimiwa Waziri nasema hatutakubaliana nalo. Watu walipe kodi, hiyo itawezekana kama sisi tutakuwa waaminifu na tutakuwa watiifu, hali kadhalika tutadumisha uzalendo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa katika Halmashauri zetu ndilo linaloturudisha nyuma, linalrudisha maendeleo yanchi yetu nyuma. Mimi naamini kabisa fedha zinazokwenda katika Halmashauri zetu, tukizisimamia vizuri na tukajiamini, wale wanaokula rushwa, tukawashikisha adabu, siyo kuwafukuza tu na muwafungulie mashtaka muwafunge, kwa kweli hii Tanzania itaendelea. Sasa kuna kuoneana aibu, mtu akichukua rushwa kwenye Halmashauri, katika manunuzi, tunawaonea aibu. Naombeni tuhakikishe tunapiga vita rushwa kwa hali na mali. Yeyote anayechukua rushwa, kama

mnawaonea huruma sana, basi wanyongwe, itakuwa ni heshima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* inashindwa kukusanya kodi na Mheshimiwa Waziri nakuomba usikilize hapa, maana mnasema kabisa kwamba *TRA* imekusanya kodi lakini ni watu wangapi wanaolipa kodi hapa Tanzania? Tunao Watanzania wangapi? Watanzania tuko milioni 45 halafu leo hii tunasema kwamba tunakusanya shilingi bilioni 500 kwa mwezi. Mimi ninaishauri Serikali ihakkishe kabisa *TRA* inakusanya mapato. Kuna rushwa kuwa sana *TRA*. Kila Mbunge aliyechangia hapa utasikia anasema *TRA* kuna rushwa, ni kwa nini msifanye mabadiliko makubwa sana *TRA*. Hata ikiwezekana kama ni kuivunja muivunje na kuanzisha Kitengo kingine ambacho kitakuwa na watu waadilifu ambao watakuwa tayari kuitetea nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maliasili zile tulizonazo mfano utalii, madini, misitu bahari, mito maziwa, gesi, bandari, hata viwanja vyta ndege na hata ndege zenyewe kama ikiwezekana tununue, itasaidia sana kuinua pato la uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba niulize Waziri anayehusika na Mpango wa Taifa, naomba wataalam wetu watueleze kwa nini uchumi wa nchi yetu unakua lakini Watanzania walio wengi ni maskini? Vilevile Waziri atueleze ni kwa nini nchi yetu ni maskini mpaka sasa hivi, tunataka majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba Waziri anayehusika na Mpango wa Taifa wa Maendeleo atueleze, ni lini Serikali itajenga Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere kule Butiama. Maana toka tumepitisha bajeti ya mwaka 2011 mpaka sasa hivi ni ahadi zinatolewa lakini utekelezaji hakuna. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba kuwambia Watanzania kwamba tuache kulalamika, tufanye kazi. Zamani nilikuwa ninaona Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa

Mikoa wanasisitiza kila mtu afanye kazi. Imeandikwa hata kwenye Biblia na Vitabu Vitakatifu kwamba asiyefanya kazi na asilie lakini kwa sasa hivi tumejenga tabia mbaya ya kila mtu kukaa na kulalamika, hafanyi kazi anafikiri kwamba Serikali itamfanya kazi. Kwa hilo, tunawaomba viongozi wa Serikali, wale wote ambao wanawashawishi Watanzania wasifanye kazi wachukuliwe hatua. Watanzania wafanyekazi na kila mmoja atimize wajibu wake na hii Tanzania itabadilika. Watu hawafanyi kazi, muda mwingu ni kulewa tu tangu asubuhi, saa mbili asubuhi unakuta mtu amelewa, shambani haendi, sasa wanafikiri Serikali itampeleke kila mtu hela? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Watanzania wenzangu tujenge tabia ya kufanya kazi na sana sana tuisisitize kilimo. Kilimo bado ndio uti wa mgongo wa Taifa letu, lazima tuhakikishe Watanzania wanalima, wanajitosheleza kwa chakula, mambo mengine ndiyo yafuate. Tatizo sasa njaa ipo, watu hawafanyi kazi, wanategemea Serikali ipeleke chakula, kwa kweli kuendelea itakuwa ni kazi kubwa sana. Mimi ninarudia kusema kwamba Watanzania, hata kama ni kuwalazimisha walazimishwe. Wenyeviti wa Vitongoji, Mabalozi, mpaka Wakuu wa Wilaya, wanafanyakazi gani? Hebu wahakikishe kwamba wakikuta watu wako vilabuni saa mbili asubuhi, kamata, weka ndani baada ya hapo sheria itafuata na watu watafanya kazi na hii nchi itaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema kwamba, nchi hii ni ya kwetu, tuna wajibu wa kuilinda kila mmoja wetu. Yeyote yule ambaye anategemea kwamba ye ye atawezakaingia au akasaka madaraka kwa kutumia vita, sisi vijana wa Watanzania tunasema kabisa kwamba hatuwezi tukakubali. Kama ni demokrasia, nenda kauze sera zako, ukiziuza barabarani ukashinda sawa lakini utegemee kwamba uingie kwa kutumia vita, kwa kushawishi watu wanafanya maandamano badala ya kukaa na kufanya kazi, ninasema kabisa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ifanye kazi na itemize wajibu wake kwa raia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekit, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Nyambari Nyangwine kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Rashid Nundu na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa ajiandae.

**MHE. CYTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja hii asilimia mia (100%). (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba niipongeze Serikali kwa kukubali kuungeza fedha katika sekta zile muhimu ambazo zinagusa wananchi. Zimetajwa kama kilimo, nishati vijijini, maji na Kadhalika. Naomba tu niseme kwamba nimejenga matumaini, maadam suala la nishati vijijini limewekwa katika msisitizo mkubwa, naamini kabisa vile vijiji vyetu vya kule Mkoani Mbeya, hususan Wilaya ya Rungwe ambavyo tumekuwa tukiviombea kila mwaka sasa vitapata umeme. Kama mjuavyo, Mkoa wa Mbeya ni mkubwa sana na unazalisha kwa kiwango cha juu sana, naamini sasa kwa mazao ambayo yanalinwa kule yatapata nafasi ya kusindikwa hukohuko vijijini na kuongezwa thamani na kusafirishwa nje ya nchi kwa kutumia uwanja ndege wa Mbeya wa Songwe, ambao umeanza kufanyakazi hivi karibuni, nashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaona kuna fedha kidogo ya barabara imeongezwa, naamini barabara ya lami ambayo tumekuwa tukiviombea fedha kila siku hapa ya Katumba, Rwangwa mpaka Tukuyu, sasa itajengwa. Haya ni matumiani yangu na ninawaombea sana wale Mawaziri wanaohusika wafanye kazi zao vizuri na tutawaonga mkono kwa asilimia mia (100%). (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja nizungumzie hoja ambayo iko mbele yetu. Nianze na Sera ya Mapato. Nashukuru kwamba Serikali imepokea

mapendekezo ya *Labs* ya namna ya kuongeza mapato ya Serikali. Kuna pendekezo moja ambalo moja kwa moja Serikali imekubali, nalo ni pendekezo la uvunaji wa vitalu vya misitu kwa njia ya mnada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na hilo lakini nachoamini hapa, ni kwamba tunachotazamia ni Serikali ipate fedha za kutosha. Kwa hiyo *bidders* wakubwa ambao watatoa fedha nyingi ndiyo watakaofanikiwa. Vilevile nachokiona mimi *bidders* hawa ni wale ambao watakuwa na uwezo mkubwa kifedha, kwa hiyo wata-*bid* kwa hela nyingi, lakini nina uwoga wa aina mbili. Moja, hatutapata *bidders* ambao ni wananchi wa Tanzania wa kawaida. Hao na mimi naamini kabisa watashindwa kwa sababu hili litakimbiliwa kwelikweli ninavyoona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watakuja hapa watu wenye hela zao wata-*bid* kwa viwango vikubwa sana na watashinda na tutapata fedha, hiyo sina tatizo lakini mimi hapa ninaona kuna jambo moja kubwa sana kwangu mimi ninavyoliona, ambalo linaweza likatoka na litatoka, kwa sababu hawa wawekezaji watakuwa wameshapata misitu ya kuvuna, woga wangu ni kwamba suala la mazingira hapa halijatazamwa vizuri. Hawa watakuwa na *interest* ya kuvuna miti ili wapate fedha. Suala la mazingira *they have no concern* na hilo kwa sababu wanachotaka ni fedha. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ituambie, itaweka utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba suala la mazingira pale, hii misitu yote haiondelewi, tukaachiwa jangwa. Kwa sababu ni kweli watavuna miti wataondoka, watakwendwa zao lakini sisi tutaachiwa jangwa halafu na sisi suala la mazingira linatuathiri sana, tena sana. Ukame tumeshaanza kuuona, uhaba wa maji tunauona, uhaba wa chakula tunauona, je, Serikali itaweka mikakati gani? Nachotazamia hapa lazima kuwepo na sheria na kanuni ambazo zitasimamia uvunaji huo wa misitu kwa njia hiyo ambayo imewekwa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisema kwa msisitizo, kwa sababu hata uvunaji wa kawaida ambao siyo wa misitu hii ambayo inasimamiwa na Maliasili, watu wanavuna miti

bila usimamizi wowote, wakiambiwa waende wakakate miti, wanakata wanavyotaka wao, hawajali miti midogo wala miti mikubwa. Hiki kizazi tunachokilea kinaenda wapi na tunakiachia nini hapa Tanzania kama tunaangalia tu suala la fedha bila kuangalia huko tunakokwenda, tunafanya nini? Hapa tunagombana kila siku, kila mtu anadai maji kwa nguvu kabisa, sina maji, sina maji au kwangu vimechimbwa visima hakuna maji yanayoonekana. Jawabu ndiyo hilo hakuna maji ni kweli tumeharibu mazingira kwelikweli. Hili mimi nimeliwekea woga huo lakini Waziri atakapokuwa anajibu atuambie Serikali kuititia Wizara inayohusika, itaweka mkakati gani wa kusimamia jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye suala la Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332. Wengi wamelizungumzia suala hili na mimi ninaomba nilizungumzie vilevile. Tumekuwa tukipata malalamiko makubwa sana kutoka kawa wafanyakazi wa kati, wafanyakazi wa chini, mishahara yao ni midogo kwa sababu kodi inayokatwa ni kubwa. Sasa hapa leo tunapunguza kiwango cha asilimia moja tu, kweli hii haiji. Naomba Serikali ilitaazame na mimi sitaki kuliachia hivihivi kwamba Serikali ilitaazame, mimi naenda moja kwa moja kushauri kwamba twende basi mpaka asilimia kumi (10%), tuanze nalo hilo ili hawa wafanyakazi wapate unafuu na wenyewe sasa tuwaambie ongezeni bidii ya kufanya kazi katika maeneo yenu, kwa sababu Serikali imewapenda, imewateremshia hata kodi ya mapato, wataongeza bidii ya uzalishaji katika maoeneo yao kazi. Kwa hiyo, naomba Serikali iende ikaliangalie hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hapa nitaulizwa sasa tunapata wapi fedha nyingine? Ni kweli swalii hili ni la msingi, tunapata wapi fedha nyingine. Katika hotuba hizi zote zilizotelewa suala la Kilimo Kwanza na masuala ya *SAGCOT* hayajapewa uzito unaotakiwa hata kidogo. Sasa tunahamia kwenye *Labs*, huku kwenye Kilimo Kwanza, kwenye *SAGCOT*, tuko a bit silent, hakuna herufi kubwa tunayoiweka ili kuweza kuzungumzia na kuona suala la kukuza uchumi katika masuala

haya. Vilevile kwenye *SAGCOT* ambako tunatazamia uzalishaji mkubwa wa chakula, tushitaji kuagiza chakula kutoka nje, halizungumziwi sana lakini kuna mikakati gani ya kuliwekea suala hili uzito ili kuongeza uchumi wa nchi, ili kuongeza uzalishaji wa chakula katika nchi hii, tumechoka kuombaomba chakula kutoka nje. Chakula kutoka nje siyo kitamu hata kidogo, chakula chetu hapa nchini ndiyo kizuri, chetu ni kizuri kwa sababu ni *fresh* lakini kile kimekaa miaka 20 mpaka 25, unaletewa Mtanzania ndiyo ule, kweli ni haki hiyo kweli? *SAGCOT* ndiyo kimbilio letu. Nashauri kwa uzito mkubwa Serikali ije hapa na mipango thabiti ya kuinua mkakati huu wa *SAGCOT*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika eneo hilihili la kilimo, hao vijana wetu kutoka Sokoine, bado hatujawatumia vizuri, ninasemea Sokoine peke yake, lakini kuna vyuo vingine ambavyo ni vya *Advance Diploma* au *Diploma* au *Certificate*, bado tunasitasita namna ya kuwatumia. Hawa ndiyo wataalam watakaongeza uzalishaji wa kitaalam ili uzalishaji uwе mkubwa katika nchi hii na tuweze kuwa na fedha ya kutosha, *both* kiuchumi lakini vilevile tujitosheleze kwa chakula. Watalaam tunao, tunawalipia kiwango kikubwa cha fedha wengine miaka mitatu (3), wengine miezi tisa (9), wengine miezi sita (6) lakini hatujawatumia vizuri. Tuje hapa na mkakati. Serikali ituambie ni namna gani kuanzia sasa hawa watu tutawa-*d/ploy* huko vijijini, waende watusaidie kwa nguvu moja ili nchi hii iweze kwenda mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, niliona haya machache niyachangie. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia (100%). Ahsante sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Nakushukru sana Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye. Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Omar Rashid Nundu na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa ajiandae.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Nianze kwa kuisifu safu ya Mawaziri wa Wizara ya Fedha, kwanza, kwa ushirikiano wao mkubwa na kazi kubwa wameifanya katika kipindi hiki kifupi. Uthibitisho wa hayo ni kuwa watu wa Magaoni huko Tanga waliokuwa wakidai fidia zao *RAHCO*, wamelipwa majuzi hivi. Barabara ya Horohoro imefunguliwa na wale waliokuwa wakidai fidia nao wamelipwa. Sasa hivi mradi wa maji unaendelea kwenye vijiji vya Geza, Kirare, Mapojoni na Mgwhisha. Pesa za Hospitali za Wilaya zimetolewa, hospitali inajengwa, lakini naomba ziongezwe ili imalizike upesi iwezekanavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumebakia malipo ya *EPZ*, sehemu ya Nema, ambapo sehemu hii iliunganishwa na Kurasini, Bagamoyo na Kigoma, kama sehemu ambazo zingelipiwa malipo mwaka huu 2013 kabla ya mwezi Juni haujafika. Naomba hili lifanyiwe bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika orodha ya vijiji ambavyo vinapata umeme, pamoja na kuwa iliamuliwa mwaka 2012, nguzo za umeme zinapopita vile vijiji vyote ambavyo viko katika mtiririko huo vipate umeme lakini bado vijiji vya Wilaya ya Tanga, Bagamoyo, Kirare, Mapojoni, Mgwhisha, Kisimatui, Mikweni, Mikocheni na vingine havijapata umeme. Nategemea hili litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa mfumo huu mpya wa bajeti. Nilisema hivyo nilipochangia Wizara ya Fedha na ninarudia, mimi nikiuangalia ni kama *speech* ya *GFK* tarehe 15 Julai, 1960 ya *New Frontier*. Tuko kwenye *New Frontier*, ye ye aliishi kwenye Urais kwa siku 1,036 tu lakini matokeo ya *vision* yake mpaka leo tunayaona yanaendelea. Sasa hii iwe ni *New Frontier*, twende huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vipaumbele. Katika vipaumbe hivi vilivyotajwa kimoja naona kinahusu Wizara hii moja kwa moja, kile cha kuongeza mapato lakini niongezee ikiwa ni pamoja na kudhibiti matumizi. Sasa mimi ninataka nikiongelee hicho. Nchi yetu tumebahatiika tunao wananchi takriban milioni 45 kwa sasa lakini wengi wa wananchi hawa

shughuli wanazofanya hazina tija, wanabangaiza tu, wanaauza vitumbua, wanaauza maandazi ili waweze kuishi, wanaendesha bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti nilipochangia kwenye Wizara ya Fedha nilizungungumzia suala la bodaboda, nikushukuru hapa kuwa ulielewa na umeondoa ada za leseni za bodaboda hizo, pamoja na pikipiki nyingine na bajaji. Lengo langu lilikuwa siyo hilo, lengo langu katika hii *New Frontier* tunaibuaje walipa kodi wa uhakika hapa nchini, tunafanya nini kupata *critical/massya* watu ambao watalipa kodi? Unapomlipisha kodi hata iwe ndogo kiasi gani, mtu ambaye biasahara anayoifanya kwanza ni ya hasara, ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niwashukuru Wabunge wote ambao kwa njia moja au nyingine katika michango yao wameunga mkono hatua ulizochukua kwa kuondoa ada za leseni za bodaboda lakini kwa wale ambao hawajaelewa, labda nilieleze hili kinagaubaga kidogo. Ninalielezea hili kama mfano tu wa biashara nyingi ambazo kutendwa kwao ni hasara tu. Watu inabidi wafanye ili wapate vihela vichache vyaa kuweza kuendeleza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua ukurasa wa 67 wa hotuba ya Waziri, amesema kwamba mapato ya jumla yasiyo zidi shilingi milioni 2,040,000/= haya hayakatwi kodi. Ukiwanja kwa siku 365, hicho ni kipato cha shilingi 5,500/= kwa siku. Kule Tanga ndiyo pesa ambazo mwenye bodaboda anapokea kutoka kwa dereva, Sh.5,500 kila siku lakini fedha hizi ndiyo hizohizo ambazo *amortisation* ya bodaboda ile inatakiwa itokee, *maintenance* ya bodaboda iwe humo, kununua matairia ya bodaboda iwe humo, gharama ambazo zinafika karibu Sh.4,000/= anabaki na Sh.1,000/=. Wale ambao wana shughuli nyingine wakibaki na Sh.1,000/= kama hiyo kama ndiyo pesa za kujilipa wala hawajafikiria kuweka kando pesa za kuweza kununua bodaboda nyingine ili biashara ikue, wataona kuwa biashara hii wanaweza kuifanya lakini wale ambao hawana kipato kingine haiwezekani. Fedha hizi kwa kiwango cha makusanyo

ya bodaboda kwa Tanga ni kuwa yule dereva anabaki na Sh.6,000/=, kijana akibaki na Sh.6,000/= alipie chumba, ale na aweke pesa za kuijendeleza, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelifanyia uchunguzi suala hili na nimekaa na bodaboda karibu vikao vitatu kuongea nao. Kuna mtu hapa siku niliyochangia akasema kwamba mimi nina bodaboda 15, sina bodaboda hata moja lakini nina bodaboda 300 za vijana wangu Tanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa nao, nimewafanyia hesabu, kuendesha bodaboda moja inagharimu zaidi ya shilingi milioni saba kwa mwaka, lakini kipato cha bodaboda Tanga cha Sh.16,000/= kwa siku ni Sh.5,600,000/=, kuna hasara hapo ya zaidi ya Sh.1,000,000/. Narudia, bodaboda ni kitengo kinachojitegemea, kila bodaboda moja ikipata hasara hivyo ukiwa na kumi una hasara ya shilingi milioni kumi. Kwa hiyo, hii inaonyesha wazi kuwa kama hawa wasiposamehewa kodi na inaonekana hapa mpaka ikifika shilingi milioni kumi ya mauzo kwa mwaka inabidi wasamehewe kodi na wasiposamehewe kodi baada ya muda mfupi hizi bodaboda zote zitakuwa kwenye vijiwe na biashara hiyo itakuwa imekufa. Kwa hiyo, naomba Waziri aliangalie suala hili. Mimi nimefanya utafiti huu na utafiti wa wauza karanga pia, siku ile nilitaja hapa, lakini napenda wengine wote waangalie ili mwisho wa siku tuibue watu ambaao kweli wanaweza kulipa kodi na wakawenza kuishi. Nasema hivyo kwa sababu, wapo watu ambaao wanaweza kulipa kodi lakini hawalipishwi kodi zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona bado watu wanaoleta gari za utalii wanasamehewa kodi. Nimesema biashara ya bodaboda sijafanya wala sitafanya lakini ya daladala nilijaribu mwaka 1998 nikiwa niko nje, nilinunua daladala nne kutoka *Simba Tours* nawajua hata watu wenyewe, vika-operate pale Arusha maana mimi makazi yangu pia yapo Arusha. Nilipovinunua *Simba Tours* nikaambiwa nilipe ushuru ambaao wao hawakulipishwa lakini mimi nikalipishwa, tena wakauchukua wao ushuru ule halafu hawakuulipa, vidaladala vile vikasimamishwa njiani, biashara

ile niliiacha mapema sana. Nilijaribu viwili vingine Tanga mambo hayohayo, zile biashara jamani watu wanaganga njaa ndiyo maana unakuta mtu anapostaafu akaendesha bodaboda kama hakuendesha mwenyewe baada ya muda bodaboda hakuna anapata shida.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Na ye ye mwenyewe pia anakwisha.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Na ye ye mwenyewe pia anakwisha kama anavyosema Mheshimiwa Ndassa, sasa hilo ni lazima liangaliwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunafanya hivyo, watu wanaotoka nje kuja kuanzisha biashara hapa wanapata mkopo benki na riba ile kubwa wanasamehewa ushuru miaka mitano. Kwa hiyo, ile mambo ya riba ya benki haiwa-*affect* kabisa wao. Tunafanya *affirmative action* kwa watu ambao siyo Watanzania, siyo sawa! Wote wanaokuja kuanzisha biashara nilisema na ninarudia hapa kwetu kama wanakuja kujaribu watozwe tozo zile ambazo zinastahili kuwatoza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuaongelea hilo, siyo misamaha tu, hii mikataba tunayoingia lazima tuwe waangalifu sana. Wengi wamesema kuhusu bandari zetu na mimi nilikuwa najaribu kukwepa sana kuongelea mambo ya uchukuzi lakini inabidi wakati mwengine niliongelee, hasa bandari ya Dar es Salaam. Tangu mwaka 2008 tulisema tunajenga Gati 13 na 14. Wakajiingiza hawa *CCCC* tangu mwanzo, wametuchelewesa kujenga Gati ile mpaka leo. Mwaka jana watu waliongea hapa mpaka walitoka mapovu kuwa lazima Gati ile iwe imejengwa Juni, 2012 halafu pakanyamaza kimya. Juzi hapa tunaambiwa wale *CCCC* kwa sababu *PPRA* waliwakataa basi tunawaacha kando tunapata mwekezaji mwengine anaitwa *CHEC*. Ukienda kwenye website ukisoma kuhusu *CHEC* inakwambia moja kwa moja kwamba hii ni *subsidiary* ya *CCCC*. Tena zipo tatu ni *CHEC, Bridge and Roads* na *CCCC* yenyewe. Hii *CHEC*

ilianzishwa mwaka 1980 lakini mwaka 2005 ikajunga na *Bridge* baada ya *Bridge* kupata matatizo kule Phillipines kama ambayo yamepatikana hapa ndiyo waka-form *CCCC* na ukweli ni kwamba hata ingepewa hii *CCCC* hii *CHEC* ndiyo ambayo ingejenga kwa sababu inasema wazi hapa kuwa *CHEC* ndiyo *International Operating Division of CCCC group*, leo naona bado *CCCC* inapigiwa debe. Sasa *PPRA* wafanyaje? Waisimamishe na *CHEC* nayo? Ndiyo maana vitengo vyetu hivi wakati mwingine vinalalamika kuwa havipewi nguvu ya kufanya kazi tunavikatisha tama. Nitaangalia *PPRA* wata-react vipi kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga tuna viwanda na kimoja ni kiwanda cha *cement* ambapo vipo kwingine pia. Mwaka juzi hapa tulipoomba tupewe idadi ya walipa kodi wazuri Tanzania viwanda vyta *cement* vilikuwa ni vimojawapo na hasa kile cha Tanga. Viwanda hivi sasa hivji vinazalisha tani karibu milioni 3,700,000...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite mchangiaji anayefuatia ambaye ni Mheshimiwa Yahya Kassim Issa atafuatiwa na Mheshimiwa Silvestry Francis Koka na Mheshimiwa Zarina Madabina ajiandae.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuleta mawazo yangu katika Bunge hili. Kwanza, sina budi kumshukuru Waziri pamoja na Manaibu Waziri wake wawili kutokana na jitihada wanazozifanza ili kufanikisha shughuli zetu za bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tatizo kubwa ambalo linatukabili ni ubinafsi na haya yote tunayozungumza hapa na mipango ambayo tunaipanga pasi na kuondoa ubinafsi, hatuwezi kufanikiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta nyingi kwa wale ambao tunawapa dhamana, kwa kweli hawatekelezi vizuri kubwa anatazama maslahi yake ya baadaye. Kutokana na hali hiyo, hatuwezi kufanikisha kwa sababu hakuna sababu Tanzania hadi leo kuwa tegemezi kwa misaada kutoka nchi za nje, hakuna sababu. Hii mimi binafsi, nilikuwa na rafiki yangu mmoja Mzungu, tulitembea sana katika sehemu mbalimbali na akaiangalia Tanzania, alishangaa sana kwamba mpaka leo sisi tunataka misaada kutoka nchi za nje yaani anahisi kwamba rasilimali za kutuendesha tunazo lakini tatizo kubwa lilitotukabili na ambalo limetutawala ni ubinafsi. Katika uchukuaaji wa hatua kwa wale ambao wanaokwenda kinyume, tunakuwa wanageri sana kuweza kuchukua hatua ambapo suala hili nalo linaturudisha nyuma yaani hapa tunaendesha mambo yetu kiujamaa sana. Hali hii hatuwezi kufika! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna wajibu wa kufunga mkanda ili kuweza kufanikisha mambo yetu haya ambayo tunayapanga kwa sababu sasa hivi tunapanga bajeti lakini mwisho wa mwaka hapa utasikia kwamba Wizara fulani fedha haikupata au imepata nusu yake. Tujiulize kwa nini?

**MBUNGE FULANI:** Na hizo zilizopatikana zimetumikaje?

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Na hizo zilizopatikana hazikutumika vizuri na hapana hatua zozote zinazochukuliwa. Sasa hali kama hii tutakuwa bila shaka tunakula fedha za wananchi lakini hakuna litakalokwenda. Kwa hiyo, Watanzania tuna wajibu wa kujirekebisha, kasoro zetu tuweze kuziondoa hapo tunaweza kufika mahali pazuri. (*Makof!*)

**MBUNGE FULANI:** Na kila mtu afanye kazi.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Na kila mtu ana wajibu wa kufanya kazi na hili ndiyo jambo ambalo Watanzania tunakuwa na matatizo, ni wavivu. Ninyl mnakwenda nchi mbalimbali nje ya nchi, hebu tuangalie wenzetu ni namna gani wanavyoendesha shughuli zao. Asubuhi utaona watu wanafanya kazi na mchana pia wanaingia wengine mpaka jioni na wengine jioni mpaka usiku na mimi nilitegemea meza za mbele huko mnakwenda nchi mbalimbali yale mnayoyapata kule mtayaleta huku ili kufanikisha lakini matokeo yake hakuna! Hali hii hatuwezi kwenda! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana tuna taratibu nydingi za kuwafanikisha, tuna ardhi ya kutosha, tuna bahari ya kutosha lakini hakuna linalofanzikana, sasa lazima vijana tuwaweke pamoja kwani hizi ndiyo nguvukazi. Vijana tukiwaweka pamoja katika shughuli za uvuvi, kilimo na kadhalika, tunaweza kufanikiwa. Pasina kufanya hivyo si kweli, tutakuja hapa, tunaondoka lakini hakuna litakalokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna haja gani vibua kuleta kutoka Afrika Kusini? Hawa ni samaki aina ya vibua kule kwetu tunawaita vibua, kuna haja gani ya kuleta vibua kutoka Afrika Kusini? Bahari tunayo ya kutosha, vijana wapo wa kutosha, vyuo vya uvuvi vipo, lakini kwa nini iwe hivyo? Kwa nini tusijiandae tukasema kwamba sasa hivi tunatafuta vyombo vinavyostahili ili kuweza kufanikisha mambo yetu, kwa nini tusifanye hivyo? Ndiyo maana Mzee akasema wakati huo bado hata madini kuchimbwa kwa matatizo kama haya, sasa watakaofaidika ni wale wa nje. Wale wa nje hawawezi kuja huku ila wana haja na wako katika uchumi, sasa wao bila shaka watataka mapato, sasa ikiwa tunakwenda kama hivi hatuwezi kufanikisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu wa kwanza aliyefariki, Mwalimu Nyerere siyo ilikuwa kwamba wakati huo madini hayapo lakini aliona muda bado na haya ndiyo matatizo tunayoyapata, muda bado, tuna haraka na ndiyo pale niliposema kwamba ubinagsi umetushika. Mfadhilli anakuja wewe umepewa dhamana, unapanga naye, unazungumza naye, una hakika kwamba hisa fulani utapata,

kwa hiyo, unachukua kila njia kuhakikisha kwamba mahitaji yake mwekezaji yule yanakwenda kwa sababu na wewe unapata chochote, hatufiki! Tukubali kwamba tunawaongoza wananchi, tukubali kwamba tunawaongoza wnaanchi na tunakuwa na dhima na tutakwenda kuulizwa mbele ya safari, tumewaongoza vipi watu wetu? Fedha ndugu zanguni mtaziacha hapahaha duniani! (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Waambie!

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Hao wenzetu labda sisi hatutumii masanduku lakini kweli ninyi mnatiliana pesa? Kweli mnatiliana mapesa kwamba katumie unakokwenda? Sasa hammwogopi Mungu? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda, tunataka kutoa elimu, vijana wetu kweli tumejikubalisha, tumeondoa kila kitu juu ya bodaboda, lakini hebu tutazame namna ya vifo vinavyotokea vya bodaboda. Wiki mbili *Area C* na *Area D*, vijana 20 wamepoteza maisha. Sasa hili suala inabidi tulizingatie na wapo bodaboda wanaendesha hawana hata leseni. Sasa tuliangalie, je, haya mapato ndiyo yatakwenda ikawa siku zote sisi tunatibu watu tu Muhimbili? Wapi tunawapeleka, kweli tutafanikiwa? Lazima iwepo taaluma maalum kwa vijana wetu, sisi tuliangalia pamoja tu kwamba tuna ajira lakini ajira ambayo kifo mbele ni ajira gani hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa tuhakikishe kwamba vijana wetu wanapata taaluma ya kutosha na Askari wetu wahakikishe kwamba wanafanya kazi ya kutosha, waelimishwe kwa kanda maalum na kwa kila sehemu, tukifika hapo tunaweza kwenda vizuri. Gari zina *speed* zake zilizowekwa lakini bodaboda hakuna *speed*, vijana wanakwenda vibaya sana na akina mama ndiyo wateja wao wakubwa, kabisa suala hili inabidi tulirekebishe, tukifanya hivyo nahisi tutafika mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi, vijana wengi hapa wamesema kwamba tupunguze kodi, tutapunguza viyi kodi na kodi ndiyo inayoleta uchumi wa nchi yetu?

**MBUNGE FULANI:** Bila kodi hatutakwenda.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Bila kodi kweli tutakwenda?

**MBUNGE FULANI:** Hatutakwenda.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mtu anasimama hapa anasema vinywaji vipunguzwe, vinywaji ni kitu cha starehe na huwezi kustarehe kama huna nafasi, mtu anastarehe kwa kupata nafasi, mambo yamemnyookea.(*Makof*)

**MBUNGE FULANI:** Starehe gharama.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Na starehe ni gharama! Sasa masuala haya nahisi hapa si ya kuzungumza kama watu wazima. Mimi kama mngekuwa mnasema kwamba tupunguze kodi kwenye *tax* ningekubali kwa sababu *tax* hivi sasa kwa kweli zimetawaliwa sana na bodaboda, hawana kazi.

**MBUNGE FULANI:** Na bajaji.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Wametawaliwa na bodaboda na bajaji, kwa hiyo hawana kazi. Kwa hiyo, tungesema hawa tuwapunguzie mzigo kwa sababu uchumi wao ni mdogo lakini vinywaji, vinywaji mwenzangu mambo yamekunyookea, mambo yako yamekwenda vizuri, pesa unazo mfukoni na nyininge zimebak, ukitaka starehe ni gharama! Ukitaka starehe ndugu yangu gharama, Mheshimiwa Mkuchika unajua hayo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kila mwaka tunakula hasara kutokana na mambo yetu ya barabara na hii ni kutokana na tatizo la kutokuwa na reli sehemu husika. Mizigo inakuwa mikubwa na nchi yetu tunajua tunaweka sehemu zile hata ikiwa mzigo mkubwa wakati mwingine unapitishwa.

Mtu akishapata chochote anamwambia nenda lakini huku barabara zinaharibika. Sasa tuna wajibu wa kukuza njia zetu za reli ili kuweza kuondoa matatizo haya. Kkila mwaka barabara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kwa mchango wake na hasa kwa kusisitiza suala la starehe ni gharama lakini sasa sijui huo usisitizaji wako una misingi ipi lakini tumepokea ujumbe huo.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema atakayefuata ni Mheshimiwa Zarina Madabida atafuatiwa na Mheshimiwa Silvestry Koka na Mheshimiwa Clara Mwatuka ajiandae.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na naomba niwapongeze Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mzuri, hususani Temeke, Mianzini kwa kuchukua kata yetu kiulaini pamoja na kwamba watu kutoka Kawe na Ubungo walikwenda kuchukua gesti na kulala hukohuko. Nawapongeza sana Mianzini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu mpya uliokuja wa kujadili bajeti. Kwa kweli sasa hapa tunaongezea nyama lakini bajeti tumeijadili kwa kina. Niipongeze sana Serikali kwa kuweza kukubali mapendekezo mengi sana ambayo yalitolewa na Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma bajeti ni nzuri sana, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake

kwa kuweza kuandaa bajeti nzuri. Kusema kweli ile nyongeza iliyofanywa itatoa tija nzuri ya umeme kwenye vijiji, maji, barabara Dar es Salaam na kote nchini, kwa hiyo, nawapongeza sana kwa hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ninayo machache kidogo. Jambo la kwanza, ni ongezeko la kodi kwenye petroli na dizeli. Pamoja na kwamba ongezeko hili ni dogo, lakini unapoongeza kodi kwenye *petrol* na dizeli umeongeza karibu kila kitu. Unasema kwamba ni ndogo lakini yale magari yanayobeba mizigo na abiria ni makubwa, kwa hiyo, ni lazima kila kitu kitapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waliangalie upya suala hili la ongezeko la kodi katika petroli. Nina hakika kabisa kama watu wakijipanga vizuri katika kukusanya kodi, kuna mahali ambapo tunaweza kufidia. Nimepeleka mchango mwingine wa maandishi ambao nimetoa mifano michache na Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza kuhusu hilo. Naomba hilo liangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo nimeomba iangaliwe sana ni kurudisha VAT katika utalii. Utalii unaingizia nchi hii pato la takribani dola bilioni 1.5 kwa mwaka na pia inachangia kati ya asilimia 17 na 19 ya pato la nchi yetu, lakini tuna ushindani mkali sana kutoka nchi jirani. Ongezeko linaweza likafanywa lakini kuongeza ghafla inaweza ikatuletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wazo kwamba hatua ya kuondoa VATisiwe ghafla, lakini waiangalie ni jinsi gani ile VAT itaathiri utalii wetu uki-*compare* na nchi nyingine. Kwa nini nasema isiwe ghafla? Wenzetu wa Ulaya wanapotaka kwenda kufanya utalii ambapo wanakuja huku Afrika, mtu anajiwekea fedha kidogo kidogo kwa mwaka mzima, anamlipa *agent* wa *tours* na wale wanakuwa wamefanya *booking* ya mwaka mzima. Sasa unapoongeza VAT ghafla maana yake unamwambia aende akamwambie yule mhusika aongeze, ukimwambia aongeze ni kama unamwambia asije. *Repercussion* yake inaweza ikawa

mbaya sana. Kwa hiyo, naomba sana tuangalie jinsi gani kama ni kuongeza basi tuwape *notice* kisha tuongeze baadaye lakini siyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka vipaumbele tofauti ikiwa ni pamoja na barabara mbalimbali. Kusema kweli naishukuru sana Serikali kwa sababu mwaka jana Dar es Salaam tumepata barabara nyingi sana na hii yote ilikuwa ni katika kujaribu kuondoa msongamano Dar es Salaam. Hata hivyo, naomba nirudie tena na Serikali inisikilize kwa sababu barabara tulizofungua bila kufungua daraja la *Salender*, bado hatujafanya kazi nzuri kwa sababu wote tunaondoka huku kwenye barabara zilizofunguliwa na kwenda kukutana pale *Salender Bridge* na tunatumia saa kadhaa kufika mjini na nguvu kazi kubwa sana inatumika pale. Maana yake wewe kama una kitabu au *paper* unasoma unaweza ukaimalizia palepale kabla hujavuka *Salender Bridge*. Kwa hiyo, naomba sana huku kwenye bajeti inawezekana haikuandikwa lakini Serikali itafute fedha mahsus kwa ajili ya kulihudumia daraja la *Salender Bridge*.

**MBUNGE FULANI:** Ni Daraja la *Salender* siyo Daraja la *Salender Bridge*.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Ni daraja la *Salender*, naambiwa siyo Daraja la *Salender Bridge*, naongea Kiswahili na Kiingereza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kidogo katika fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya benki ya akina mama pamoja na maendeleo yao, zile shilingi bilioni mbili (2) zilizoongezwa. Ukizitaja fedha hizi unaona ni nyingi sana lakini kusema kweli fedha hizo ni ndogo sana hasa ukitilia maanani kwamba kwa kipindi cha zaidi ya miaka minne au mitano, hizi fedha hazikutolewa. Sasa sielewi watakwendwa kuzigawaje fedha hizi kwenye Wilaya mpaka ziwatoshe wanawake? Niombe Serikali iangalie jinsi gani inavyoweza kuongeza fedha hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hizo tu, hata zile za Manispaa hatuzipati, Manispaa hawazitoi. Juzi kwenye bajeti tulikuwa tunawaambia wakasema mtatusamehe lakini hiyo *five percent* mnazosema hatuna. Sasa tunafikiria kwamba zile fedha za Manispaa zimepangwa *five percent* lakini hakuna, kwa hiyo hii shilingi bilioni mbili ndiyo wanawake wote watakaa chini kuiangalia, ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho, kumekuwa na kubadilisha vipaumbele vya Halmashauri. Nazungumza hili kutokana na *experience* yangu kwenye Halmashauri ya Kinondoni. Halmashauri inapeleka mipango yake na maombi ya fedha. Sawa umeniambia sikupi shilingi bilioni tano nakupa shilingi bilioni nne, ile shilingi bilioni nne pia unanipangia kwamba usiende kutengeneza barabara ya Kachube, nenda katengeneze barabara ya Masaki. Hili tunasema hapana! Mtuachle kama ni vipaumbele toa kwa kipaumbele, sasa ukiishaniambia nisitekeleze kipaumbele changu inamaanisha umenibadilishia na kile kipaumbele ambacho umenipa nikitekeleze. Sasa kwangu mimi kama Wilaya hicho ulichonipa wewe siyo kipaumbele. Hii ni kero ambayo sisi pale Manispaa tunayo kwamba tumeomba fedha kwa ajili ya kutekeleza kitu kingine, tumepanga tutatengeneza barabara hii na hii, lakini inapokuja unapewa barabara ambayo kwako si kipaumbele, hiyo ni kero ambayo naomba Serikali iiangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho kabisa ni riba kubwa sana kwenye fedha za mikopo zinazotolewa hasa ukienda kwenye *microfinance*. Ukienda kwenye *microfinance* mpaka unashangaa kwamba hivi huyu anayechukua anakwenda kufanya biashara gani ambayo atapata faida maana yake ukiweka *cumulatively* inafika mpaka asilimia 48? Ndiyo maana utasikia huyu kanyang'anywa *TV*, huyu sijui kitu gani, akina mama wanahangaika kwa ajili ya kupata mikopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri suala hili walialangalie sana. Naibu Mawaziri wote ni wanawake wanajua jinsi wanawake

wanavyohangaika. Naomba sana *rates* za riba kwenye *microfinances* ziangaliwe ili kusudi ziwe *realistic* mtu anapokwenda kuchukua mkopo afanye biashara apate, lakini mtu anakwenda kuchukua mkopo halafu anashindwa hata kulala nyumbani kwake kwa ajili ya kuogopa riba na kwamba akii-*default* vitu vyake vitakuja kuchukuliwa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niipongeze tena Serikali na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zarina. Sasa nitamwita Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, atafuatiwa na Mheshimiwa Clara Mwatuka na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla ajiandae.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kutoa shukrani na pongezi kwa Serikali pamoja na Bunge letu Tukufu kwa kazi nzuri inayoendelea kufanya kwa ajili ya nchi yetu na wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na kuipongeza *TRA* kwa utaratibu walioufanya dhidi ya vijana wetu na hususan kwenye bodaboda. Hata hivyo, naomba vilevile kwa utaratibu huo, *TRA* waweze kutambua na kutoa maelekezo ambayo ni *uniform* kwa nchi nzima hususan kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wanaofanya biashara zao katika masoko madogo madogo ya kuuza vyakula pamoja na wale wajasiriamali wadogo wadogo wanaofanya kazi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na stendi, kwa mfano, pale kwangu Maili Moja, Kibaha Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ulifika wakati *TRA* wakawa wanakwenda kutaka kudai kodi ya mapato hata kwa wale wafanyabiashara wadogo

wanaouza mchele katika vizimba nya soko dogo lile la Maili Moja. Kwa hiyo, naomba kuitia *spirit* hiihii ya kuwaangalia hawa wafanyabiashara wa bodaboda, basi na hao wengine waweze kuangaliwa ili na wenyewe waweze kufaidika na shughuli ndogondogo wanazofanya za kiujasiriamali na waweze kujijenga ili hatimaye waweze kuwa wafanyabiashara wakubwa na waweze kushiriki vyema katika kulipa kodi na kuchangia katika pato la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie namna nzima ya kuchangamsha uchumi. Tunafahamu nia na madhumuni ya bajeti ni pamoja na kuchangamsha au *ku-stimulate* uchumi wa nchi. Tunaona wazi kwamba tumekuwa tukipanga mipango mingi, hususan ya kilimo, tumenuna vifaa mbalimbali yakiwemo matrekta kwa wingi katika harakati za Kilimo Kwanza kwa maana ya kuboresha kilimo. Hata hivyo, ni ukweli usiofichika kwamba hata kama tungeendelea kununua matrekta mengi kiasi gani pamoja na mitambo mingine mbalimbali kwa ajili ya kilimo ili tuweze kwenda kwenye kilimo cha biashara (*commercial farming*), kama Serikali haitaamua kwa makusudi kabisa kuweka utaratibu wa kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kilimo, bado tutaendelea kutegemea mvua zisizofahamika na zisizokuwa na msimu maalum na matokeo yake hata tungelima na haya matrekta bado mkulima ataendelea kupata hasara kubwa na hataweza kuvuna mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu, naiomba Serikali kama tunavyokaa hapa tunapanga, fedha zinaenda kwenye miundombinu ya barabara na mingeneyo, sasa umefika wakati wa kupanga fedha ziende katika miundombinu ya umwagiliaji. Napenda kuona Serikali inatengeneza miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo mwafaka ya kilimo ili wananchi na wale wote wanaotaka kuendesha kilimo cha kisasa na kikubwa waweze kupata maji ya umwagiliaji katika namna rahisi na kuweza kukuza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu, tunazungumzia ukuaji wa uchumi mara kwa mara, lakini ukweli ni kwamba ukuaji huu tumeshindwa kuu-*translate*

kwenda kwa wananchi wengi wa Tanzania ambao ni wakulima na wafugaji. Maana yake tunafahamu zaidi ya asilimia 70 ni wakulima na wafugaji na hawa katika suala hili bado hatujaweza kuwagusa katika kukuza uchumi wao. Kwa hiyo, ni wazi kama tutafanya mapinduzi na hasa katika umwagiliaji tutawagusa hawa wakulima. Kama tutafanya hivyo, tutaondokana na utaratibu wa vijana wengi wenye nguvu kuhama kutoka vijijini na kukimbilia mijini, maana hata hizi bodaboda karibu vijana wengi wanatoka vijijini. Sasa mwisho kila kijana atakuwa na bodaboda na hata wa kuipanda atakuwa hayupo. Nina imani tukiimarisha kilimo na hususan tukienda katika kilimo cha kisasa ikiwa ni pamoja na kuimarisha umwagiliaji, ni wazi vijana hawa watabaki vijijini, watazalisha na nchi yetu itakuwa na chakula cha kutosha na ziada, tutauza na hapo mkulima au mfugaji ataona ni namna gani uchumi unakua. Kama tutafanya hivyo, tutaondokana na migogoro kati ya wakulima pamoja na wafugaji, lakini na ule uhamiaji wa watu kwenda mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusisitiza hilo kwa sababu ukiangalia *trend* ya mfumuko wa bei kwa mfano mwaka 2010/2011 na 2011/2012, *average* tulikuwa tumekwenda mpaka kwenye *inflation* ya *digits* mbili, tulifika mpaka 19, lakini uki-*analyze* utaona kabisa mchango mkubwa wa mfumuko huu wa bei ulikuwa unasababishwa na chakula ambapo kilienda mpaka asilimia 40. Kwa hiyo, kama tutajikita sasa na kuhakikisha tunakwenda kwenye ukulima wa kisasa na Serikali ikawasakiwanananchi katika kutengeneza miundombinu hii ambayo ina gharama kubwa, ni wazi kuwa sasa hata ule ukuaji wa uchumi utamfikia mwananchi wa kawaida na wale walio wengi vijijini na kwa maana hiyo kila mtu atakuwa anafurahia ukuaji wa uchumi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba bado tunalo tatizo kubwa katika kusimamia hata hizifedha kidogo ambazo tunazikusanya. Naamini kama tutatangeneza mfumo mpya na hususan kwa vijana wetu wengi

wanaomaliza shule na vyuvo, tutafika mahali kutakuwa na nidhamu ya usimamizi wa fedha na hata hizi chache ambazo tunazikusanya zitasimamiwa kwa ubora zaidi na zitawenza kuleta tija. Tuchukulie mfano leo kijana anayemaliza chuo kikuu au chuo chochote na anaenda kufanya kazi, anakabiliwa na mambo chungu nzima. Jambo la kwanza anatakiwa atafute usafiri au gari, gari lile anatakiwa alinunue kwa fedha taslim (*cash*). Bado anakabiliwa na kujenga au kupanga nyumba ambapo anatakiwa alipe kodi ya mwaka mzima na yenyewe ni *cash*, hata kama ni kujenga nyumba ni kwa fedha taslimu. Kwa kweli katika hali hii tunasababisha vijana hawa wanashindwa kuwa na nidhamu ya kusimamia kwa uadilifu fedha na kazi ambazo tunawapa. Nashauri kama kweli tunataka kuona vijana wetu wanakuwa waadilifu na tunajenga kizazi kipya ambacho kitakuwa kinafanya kazi kwa uadilifu na kuifanya nchi yetu iweze kusonga mbele na kuthamini fedha ambazo zinatokana na kodi zetu, ni wazi kwamba sasa Serikali ianze kuangalia utaratibu mzima wa kusaidia mfumo mzima ili vijana hawa wanapoingia katika maeneo ya kazi waweze sasa kuingia katika utaratibu wa mikopo na ili kuwaondolea adha na tamaa na ulazima wa kukusanya fedha kwa haraka haraka ili waweze kupata mahitaji muhimu ambayo wanahitaji ili kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasema hayo kwa sababu huo ndiyo ukweli ambao uko katika shughuli zetu za kila siku. Nina imani kama Serikali itajikita katika kuyaangalia haya, tutafika mahali tutajikuta wote kwa ujumla wetu wakulima, wafanyakazi na wafanyabiashara, tunakwenda pamoja, tunaimba wimbo mmoja na hata ile *gap* kati ya walionacho na wasionacho itapungua. Tukifikia hapo, nina imani tutaishi kwa amani na utulivu na tutaheshimiana na nchi yetu itaendelea kuwa kisiwa cha amani na maendeleo tutayapata kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ninaomba kuunga mkono hoja, tuko pamoja. (*Makof*)

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka Mwongozo wa Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy unasemaje?

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7) kinasema kwamba mtu anapozungumza asiwepo mwingine anayezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya Wizara ya Fedha, hapa kuna vitabu viwilli; kitabu cha Makusanyo na Matumizi. Wabunge wengi wanazungumza tu namna ambavyo Serikali isikusanye mapato, hawaelezi Serikali ipate wapi mapato. Sasa sijui inakuwaje kwani sijasikia hata Mbunge mmoja anasema hapa Waziri wa Fedha umesahau sehemu fulani mapato yanavujishwa, wenyewe kazi yao ni kusema punguza hiki, hiki na hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ikipunguza kila kitu, huku tunaomba maji, umeme, barabara, fedha zitatoka wapi? Sijasikia hata Mbunge mmoja anasema tumesahau kwenye kodi ya ng'ombe, hamna hata mtu mmoja ambaye amezungumza hilo hapa, wafugaji wa kuku hatujasungumza, lakini Wabunge wote ni mafuta shilingi mbili (2), sijui hiki na hiki. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria ya bajeti ya Wizara ya Fedha lazima tuzungumze namna Serikali itakavyopata mapato, ndiyo sheria. Mambo ya kuzungumza sijui hivi yalikwisha wakati wa Wizara, tulichangia wakati wa Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Wizara ya Mifugo, zote tumechangia. Sasa hapa tuisaidie Serikali yetu namna itakavyokusanya pesa ili tujitegemee kwa asilimia mia kwa mia au tupate asilimia 120, ndiyo tunavyotaka Wabunge

tuchangie namna hii. Kama hatuna uwezo, tukae kimya, tuwaache Wabunge ambao wana mawazo ya kuchangia Serikali yetu ipate fedha. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo Mwongozo wangu.

**WABUNGE FULANI:** Sema naomba.

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Ndiyo naomba namna hii, tuendelee kuchangia kusaidia Serikali, wapi Waziri wa Fedha kasahau au Kamati ya Bajeti imesahau wapi pa kupata fedha, tuchokonoe tupate fedha ili tuiwezeshe Serikali. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. (*Makof/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, majibu ya Mwongozo huo nitautoa baadaye, ingawa na wewe umenishangaza leo umeongeza hapa kodi ya kuku, tutoze kodi kwenye kuku na kwenye ng'ombe, sasa sijui lengo lako lilikuwa kuomba na kuku nao watozwe kodi lakini nitatoa majibu ya Mwongozo huo baadaye. Tuendelee na uchangiaji halafu nitatoa majibu ya Mwongozo wa Mheshimiwa Keissy baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Clara Mwatuka atafuatia Martha Umbulla na baadaye nitazungumza huo Mwongozo wa Keissy Mohamed tusipoteza kwanza muda wa kuchangia.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kusema machache juu ya bajeti iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mungu kwa jinsi anavyonipigania na kunishindania katika mengi. Pia nikushukuru nawe kwa kunipa nafasi. Nachukua nafasi hii kuwapongeza Waziri na jopo lake zima kwa juhudhi waliyoifanya kuweza kuokoteza pesa hapa na pale kuweza

kuongezea kwenye Wizara zile ambazo zilikuwa zina mapungufu. Nawapongeza sana, muendelee na moyo huo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, napenda nitoe masikitiko yangu nikujulisha wewe na Bunge nzima juu ya mambo yanayofanyika Mtwara hivi sasa kwamba watu wanapigwa tangu wiki iliyopita hii wanapigwa mpaka juzi sababu haijulikani. Sasa najiuliza ni yapi, ni ya gesi yaleyale na kama ni gesi kweli tupo katika nchi hii, kwa kweli sina amani. Najiuliza hivi tupo nchi gani, Kusini kule au Mtwara hii ni watu wa aina gani na hao wengine sehemu zingine wakoje? wa kweli ninasikitika, nasikitika hali hii ni mbaya sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza ni kwamba hata vyombo vya habari kimya, watu wamepigwa, wameumizwa, wamelazwa hospitalini, lakini hakuna taarifa yoyote nchini juu ya matukio haya. Ina maana kwamba watu wa kule hawatakiwi katika nchi hii. Navyojieleza mimi, nafikiri hata wenzangu nao wanasema eeh sisi siyo wa Tanzania hii. Kwa kweli Serikali naiomba ifanye juu chini jamani, tumeambiwa amri kuu ni upendo, tupendane, kwa nini tunachukiana? Yawepo hayo kwa sababu, lakini unakwenda kumpiga mtu, Wanajeshi kwenda kuwapiga wananchi, raia, hawana silaha hawana nini. Mitutu, vifaru vimejaa huko Mtwara, wanapigwa mpaka Newala Mjini, sababu haijulikani. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilitazama hili, ione na itende haki yaani wale wanaotumwa kufanya kazi wanapitiliza. Juzi Uchaguzi Mdogo wa Kata ya Nima, magari matano ya Wanajeshi na vifaru juu eti kwenye Uchaguzi wa Kata jamani, tunatoka wapi, tunakwenda wapi? Nasikitika sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kidogo tu juu ya bajeti iliyopo au hali iliyopo mbele yetu. Kwa kweli sipati la kusema kwa jinsi nilivyokatizika raha na nilivyo na huzuni juu ya hali inayoendeshwa kule Mtwara. Juzi hapa wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipotueleze hizo nyongeza, nyongeza zilizopatikana Wabunge hapa tulipiga makofi vizuri sana, kushangilia kwamba kazi imefanyika nzuri. Ni kweli juhud

wamefanya kubwa ya kupata fedha za kuongezea katika sehemu mbalimbali lakini tumeshangilia kitu chenyewe wakati bado hatuna hakika kwamba itakuwa hivyo au imesemwa tu kama kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Mheshimiwa Waziri na jopo lako iwe ni kweli hili ulilotufikishia kwamba fedha zitatorewa ndani ya wakati na kule zinakokwenda zikafanyiwe kazi kama ilivyokusudiwa, isiwe zinatolewa kama zilizopita zingine, inaonekana huku zilitolewa lakini zinapotakiwa kwenda hazijafika, haitakuwa na maana yoyote. Jamani kufanikisha kwa jambo siyo lazima pawe na kitu kwa wingi sana, kidogo hichohicho kinaweza kufanyiwa kazi kwa makini kikaleta ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa wengi wamelalamika kuhusu madeni ya Walimu, ni kweli siyo kwamba fedha hazikuwepo huko nyuma maana sasa nina imani kwa wingi wa fedha zilizopatikana sasa hivi madeni yote yatakwisha lakini fedha zilikuwepo huko nyuma, mafisadi walikuwa wakizitoa wapi si hizo hizo? Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu, tukawa tunasema hapa ooh, Waziri ajiuzulu, ni kumwonea, kwa nini hatumwambii Rais basi ajiuzulu si mtu wake huyu, si kweli. Watoto wetu tumewapa Walimu wawafundishe, sasa Mwalimu hatujampa mazingira mazuri ya kuipenda kazi yake, atafanya kazi? Mshahara mdogo, anapitwa hata na Bwana Shamba, Bwana Afya amba wanafanya kazi usiku na mchana, hawapati mshahara wa kutosha, ataipenda kazi hii, ataifanya kwa moyo, haiwezekani. Nyumba ya kulala tabu, anahangaika vijijini ajitafutie mwenyewe, apange huko kijijini na maisha yaende. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamedai kwa muda mrefu wakatishia wakati ule watafanya mgomo, mkawatisha wakaacha, Walimu wavumilivu lakini mjue kwamba unapomchukua mtoto wako ukampa Ngaliba, wote tunamfahamu Ngaliba, jandoni kule, unawapeleka watoto, unakabidhi yule, kama hatakuwa na upendo na kama hutamwekea mambo yake vizuri, anajua mwenyewe cha

kuwfanya wale watoto. Sasa na Walimu nao hivyo hivyo, kwa sababu hawatekelezewi yale wanayotaka basi hawawezi kuipenda kazi wakaifanya kwa moyo. Hebu tujaribu sasa tuwaongezee mishahara, madeni yao wanayodai tuwalipe, wapate nyumba, wale wanaoishi kwenye mazingira magumu wapate hizo posho kwa ajili ya mazingira magumu tuwape, hakika tutasema tulichelewa wapi lakini tukibaki tu hivihivi mambo yatakwenda hivihivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa wenzangu wakulima, hapa wamesema wameongeza hela kwenye kilimo lakini sijui itakuwa kama tunavyotegemea au wanavyotegemea wakulima baada ya kusikia bajeti hii kwamba imeongezewa sijui kama itakuwa hivyo. Kwa sababu mkulima anaonekana kwamba ni nyuma toka zamani lakini ni mchangiaji mzuri kwenye maendeleo ya nchi hii, hana cha kusema hiki Serikali imenisaidia, hakuna. Tumesema tunawatafutia masoko, makoso yapi, haya wanayokwenda kukopesha. Sasa tuwasimamie vilivyo hizo fedha zifike huko zikafanyie kazi. Nilisema juzi hapa kwamba vijana wameacha uvivu hivi sasa wanafanya kazi za kujidendeza na kujipatia kipato. Sasa hapo walipoamua mwenyewe vijana kufanya kazi basi tuwasimamie, wapewe mitaji ili wafanye kazi vizuri waweze kujitegemea. Tukiwaacha hivihivi ndio pale wanapokimbilia mijini kufikiria kwamba kule ndio kuzuri lakini wengi walishaona kwamba hakuna faida ya kwenda mijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia wenzangu wamezungumzia juu ya misahama ya kodi. Mimi kitu hiki nami bado ninashangaa. Kwanza, niulize uwekezaji huu wananchi hawawezi, wakipewa sehemu labda kwenye machimbo ya madini au sehemu yoyote ile, hawawezi wakawekeza, wakazalisha vizuri na Taifa likapata pato nzuri? Kwa sababu hivi sasa uwekezaji wote ni wa nje tu wakati wananchi wenyewe uwezo wapo hata ndani humu wapo wengine amba wanaweza wakashika sehemu fulani hata kwenye machimbo humu wakaendesha vizuri, kwenye hoteli wanaweza wakawekeza, kwenye bahari humo, lakini kote huko tumewapa wagoni. Sasa kinachosikitisha ni kwamba eti

asilimia tatu, wewe mwenye chako upewe Sh.3 katika kila Sh.100, hivi inaingia akilini jamani, yaani hatujihurumii? Sasa tunapata shida, nchi maskini wakati utajiri umejaa, tunaukalia tu, tunawapa wenzetu wananaufaika, wanakuja kuchukua wanakwenda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini mikataba hii inakuwa miwili, kwamba ule wa asilimia tatu ndiyo wa kujulikana Kitaifa, lakini upo mkataba wa siri, haiwezikani, tutafika wapi? Basi tuwape wananchi wao wawekeze ili wakila hao ni afadhali kwamba watalia nchini humuhumu kuliko wale wanaochukua na kwenda nje huko. Jamani, kwa kweli Tanzania tunasikitisha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yale ya kusema kwamba tuchukue hiki hapa tufanyile hiki kwa ajili ya nje tunaweza sana, lakini kwa ajili ya Taifa tupo mbali sana. Mimi naomba safari hii bajeti hii iliyoongezwa vizuri wote tukafurahia hapa ndani basi na iwe hivyo, wale waliopewa nafasi hizo waone kwamba hapa mimi ni kama nyabara, nasimamia kitengo hiki kifanye kazi vizuri iwe manufaa kwa nchi na siyo kwamba unafanya hivyo kwa faida yako, hapana. Tumekula viapo kuanzia kwenye vyama na hapa kila siku tunakula viapo, tuwe waaminifu na utii pia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu hivi sasa inaonekana kwamba aliyepata amepata, wengine kama wewe hukupata usipige kelele, ukipiga kelele, wanasesma ulie tu, watu wanakwenda, siyo kweli. Mheshimiwa Yahaya amesema hapa kwamba hakuna anayekwenda nazo kwenye sanduku au watamfungashia mzigo huo kwenye sanduka akaenda nao, hakuna, haya yote tunayaacha hapahapa. Tufanye kwa manufaa ya nchi, wote wajisikie kwamba hapa leo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kila mmoja ambaye amepewa nafasi ya kuongoza na kwa mfano nyie wenzangu Mawaziri maana ndiyo mlioshika usukani, naomba Mungu awabariki, awapeni afya njema na muwe na moyo hasa wa

uzalendo maana Wizara yako ikifanya vizuri ni sifa yako wewe Waziri. Kwa hiyo, mfanye kazi kwa uchungu, watu wale tunaowasimamia wa chini yetu basi tuwasimamie vizuri ili wewe unufaike pamoja na watu wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ahsante na Mungu awabariki. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mama Clara Mwatuka. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Charles Mwijage ajiandae, halafu tutamsikia Rukia Kassim Ahmed.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha mimi kumudu majukumu yangu yote nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii pia kuwapongeza wananchi wa Dongobeshi, Wilaya ya Mbulu, kwa kukipa kura nydingi Chama cha Mapinduzi japokuwa hazikutosha, lakini iwe fundisho kwetu na kujipanga upya, wasife moyo, ipo siku Mungu atatusaidia tutaikomboa Kata yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba njielekeze katika kuchangia bajeti yetu. Nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wake, ni watu makini na Watanzania wana imani kubwa nao kwa kuwa bajeti hii inaweza ikawakomboa katika lindi la umaskini walionao na kwa ubunifu wao naamini kwamba bajeti ndiyo njia pekee ya kuweza kuwasaidia wananchi ili watokane na umaskini. Kubuni namna bora ya kutengeneza na kutekeleza na kusimamia bajeti, ndiyo njia pekee ya kuweza kuinua uchumi wa nchi yetu na pato la Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tukipanga bajeti nzuri namna gani kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema kama bajeti haigusi mtu wa chini ama

wananchi walio wengi maskini vijijini bado bajeti hiyo haiwezi kuwa na manufaa kwa Watanzania. Nasema hivyo kwa sababu umaskini wa nchi unapimwa kwa vigezo vyta umaskini wa wananchi wake, namna wanavyoishi katika nyumba zilizo duni vijijini, namna ambavyo hawana uhakika wa chakula na namna ambavyo wana matatizo mengi ya hapa na pale, hiyo bado inaweka nchi katika *rank* ya kuwa nchi maskini kutokana na hali duni ya wananchi wake. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuangalia ni namna gani bajeti zetu tunazopanga mwaka hadi mwaka ziweze kugusa moja kwa moja wananchi walio wengi vijijini. Naipongeza Serikali kwa namna ya pekee kwa kuwa, imeweza kusikia kilio cha Wabunge, wameongeza fedha katika maeneo mbalimbali ambavyo Wabunge walisisitiza ili kupunguza ukali wa umaskini vijijini, lakini bado ninaishauri Serikali kwamba iendelee kupanga mwaka hadi mwaka ili hatimaye tujikomboe na lindi la umaskini unaowakabili wananchi watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru bajeti hii pia imeweke vipaumbele, najua kwamba vipaumbele huwa vinatokana na mahitaji ya jamii husika. Kwa mfano, vipaumbele vya Mkoa wa Kigoma haviwezi kuwa sawa na vipaumbele vya Mkoa wa Manyara. Ukimuuliza mwananchi wa Wilaya ya Kiteto, atakwambia umeme kweli ninauhitaji, maji ninayahitaji, barabara ninahitaji, lakini kusema kweli mimi ardhi yangu ambayo inanililisha, inanipa maisha, inasomesha watoto wangu bado imeporwa na kwa miaka mitano nina migogoro hii ambayo haitatuliwi. Sasa naishauri Serikali vilevile kwamba isiendelee kufumbia macho migogoro ya ardhi. Migogoro ya ardhi imefika mahali pabaya, inapoteza maisha kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Serikali kwamba iweke namna ambavyo bajeti sasa itaelekeza wataalam waweke mipangilio ya matumizi bora ya ardhi ili tuondokane na migogoro ya ardhi. Leo hii ardhi inapoteza maisha ya Watanzania. Katika miaka mitano, kumi ijayo itaendelea kupoteza maisha ya Watanzania kwenye maeneo yenye migogoro kwa sababu ardhi haiongezeki na Watanzania tunaongezeka kwa asilimia saba hadi kumi. Sasa bila

kupangilia vizuri ardhi tuliyonayo, kwa kuweka wataalam na bajeti ambayo inaweza ikasaidia katika eneo hilo, italeta matatizo na wananchi wataendelea kupata migogoro mingi, watapoteza muda wa kuzalisha na hilo litakuwa siyo jambo ambalo litaleta maendeleo kwa wananchi kulingana na vipaumbele vyao. Serikali yetu ipangilie bajeti kwa kujali vipaumbele vya jamii katika maeneo yao ili ilete utulivu na kuongeza uzalishaji kwa sababu kwa namna hiyo pia wananchi wataweza kuongeza kipato na mapato ya Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la lingine ambalo nataka kuchangia ni la kunusuru maisha ya vijana. Ubunifu wa kutekeleza mipango ya bajeti ufanyike ukilenga vijana wa leo. Kwa muda mrefu, Serikali yetu imelenga wanawake, tunashukuru na matatizo ya wanawake siyo dhahiri kulingana na matatizo ya vijana. Kwa sababu wanawake hawawezi kuzurura mitaani pamoja na shida walizonazo, kwa sababu wana majukumu mengi ya kulea lakini vijana wanazurura mitaani kama hawana shughuli ya kufanya na wanapanga mipango mibovu kwenye magenge ambayo yanahatarisha siyo maisha yao tu bali hata ya Taifa. Kwa hiyo, naomba na naishukuru pia Serikali kwa kuwa imeshaangalia kipaumbele cha vijana lakini basi iendelee kubuni ni kwa namna gani vijana hawa kwa wingi wao wanaweza wakawezeshwa ili waweze kuendeleza Taifa letu kwa sababu ni kundi kubwa na kundi muhimu katika jamii ya Watanzania. Naomba kundi hili lilengwe zaidi si tu ili kunusuru maisha yao bali maisha ya Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano Mkoa wetu wa Manyara, tunashukuru Mungu vijana wetu wanapenda sana kulima na kufuga lakini hawana mitaji. Ndiyo maana hata ukiangalia maambukizi ya VVU katika Mkoa wa Manyara yako chini, tunamshukuru Mungu ni kwa sababu vijana wanajishughulisha sana ukilinganisha na vijana katika maeneo mengine. Tunaomba mitaji iweze kupatikana kwa ajili ya vijana, ile benki iliyotajwa ya vijana basi iweze kuwekewa fungu la kutosha ili vijana basi iweze kujisaidia

katika kuendeleza maisha yao na kuzalisha kwa wingi ili tuweze kuinua pato letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni la barabara. Sambamba na pongezi kwa Serikali kujenga barabara katika nchi yetu lakini naomba ujenzi wa barabara sasa uelekezwe zaidi katika maeneo ya uzalishaji. Kuna maeneo kwa sababu kuna fursa tu ya kujenga barabara na barabara zimejengwa mpaka vichochoroni, lakini kuna maeneo hawajawahi kuona lami mfano katika Wilaya zetu za Mkoa wa Manyara. Tunashukuru Wilaya mbili au tatu hivi zina barabara zinazopita kutoka kwa mfano Wilaya ya Hanang ina barabara ile inayotoka Arusha kwenda Singida ni barabara ya lami, hali kadhalika na Babati lakini Wilaya ya Kiteto hawajawahi kuona lami na kama, tunavyojua kati ya Wilaya zinazozalisha sana katika nchi yetu ni Wilaya ya Kiteto. Barabara ya kutoka Kibaya kuja Njiapanda ya Dar es Salaam na Dodoma ni barabara muhimu sana na tunaomba chondechonde Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi atanisikia huko alipo, barabara hii iwekewe lami kwa sababu inasomba mazao ambayo yanakwenda soko kubwa la Kimataifa la Kibaigwa na barabara hii inaharibika kila mara kwa sababu ya magari mengi yanatosomba mazao. Kwa hivyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri aiwekee bajeti ili barabara hii itengenezwe ni muhimu sana kwa uzalishaji wa mazao kutoka Wilaya yetu ya Kiteto lakini vilevile iweze kurahisisha usafiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayotoka ndani ya Wilaya ya Mbulu kupita kwenye mlima wa Magala kwenda mpaka Njiapanda ya kwenda Arusha. Hata Marais wetu wameshapita barabara hii, najua ni ya *TANROAD* lakini nikiangalia baadhi ya Wilaya zina barabara za lami mpaka vichochoroni, najiuliza kulikoni. Kwa nini barabara za maeneo yanayozalisha mazao kwa wingi ambayo inainua pato la Taifa letu zisiweze kupewa kipaumbele na bajeti zetu na Serikali lakini zinaweza kujenga barabara ambazo zina manufaa lakini basi si kipaumbele cha Taifa letu? Naomba kwa nafasi hii Serikali iweze kuangalia kipaumbele kwa barabara za maeneo yanayozalisha kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wilaya ambazo miaka 50 ya Uhuru hazijaweza kuona lami. Mfano Wilaya ya Mbulu ilikuwa na lami ya Mjerumani, ya zamani sana na ikatoboka mpaka tukaomba kwamba waikwangue bora tubaki na barabara ya vumbi lakini basi kwa bahati nzuri wamejenga barabara lakini ndio laini hiyo moja hatuna barabara zinazokwenda kwenye maeneo ya uzalishaji. Wilaya ya Mbulu inazalisha mazao kwa maeneo mengine hata mara mbili kwa mwaka na mazao mengine yanaozea vijijini. Kule Mbulu Kwerumus na Maisara wanalima mazao mengi viazi mviringo na viazi vitamu, lakini vinaozea kule kwa sababu barabara ni za shida na millima na mabonde. Kwa hiyo, naomba kwa nafasi hii nimwombe Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia barabara zile zinazokwenda kwenye maeneo ya uzalishaji zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilliona nichangle maeneo haya machache, napenda kuunga mkono hoja, nakushukuru kwa kunipa nafasi ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla. Mheshimiwa Charles Mwijage alikuwa azungumze Mheshimiwa Gaudence Kayombo lakini simwoni ndani ya ukumbi nitampa nafasi ya Mheshimiwa Rukia Kassim.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yametokea maambuzi makubwa, mlipuko wa ugonjwa wa malaria katika Wilaya ya Muleba. Nachukua fursa hii kuishukuru Serikali hasahasa Wizara ya Afya namna mlivyoitikia na kuwajali watu wa Wilaya ya Muleba, Mwenyezi Mungu awaongezee moyo huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa pole wananchi wa Muleba ambaao mmepeata matatizo hayo, tulipojikwaa tunajua na mkirejea swalii langu la Mkutano huu wa Kumi na Moja nilouliza Wizara ya Afya ikashindwa kunijibu ilichopaswa

kunijibu ndiyo hayo majanga yametupata tutakaa chini tutazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia bajeti ya Serikali, niwapongeze Mheshimiwa Dkt. Kapteni Chiligati, Alhaj Keissy na Professa Msolwa, ndio mimi nitaazima busara zao katika kuboresha au kusherehesha mchango wangu.

**MWENYEKITI:** Alhaj Keissy yupi Mheshimiwa Mwijage?

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Ally Keissy Mabodi sijui nyie mnamwitaje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge Keissyl!

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mbunge wa Nkansi.  
(*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, busara nyingine nitaazima busara ya rafiki yangu Mama Chichi, Mama Chichi ni mama wa Kichina, nilikutana naye siku moja nikamwuliza nipe siri ya maendeleo ya China. Akasema China imeendelea kwa sababu ya mambo matatu. China iliwekeza kupita kiasi katika elimu, elimu hii mnayoijua lakini zaidi elimu ya Mafundi Mchundo. Ndio maana nampongeza sana Profesa Msolwa kwa mchango wake. Tunahitaji kuwa na wanafunzi wengi, watu wengi walifundishwa ufundu stadi ambao wanapokuja kufanya kazi wanaweza kufanya kazi zilizo nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akasema zaidi Wachina walitoa elimu ya uzalendo yaani mtu anakwenda shulenii unafundishwa uzalendo na una-*disco* mpaka unauelewa uzalendo. Akaenda zaidi, Wachina walifanikiwa hapo walipofika kwa sababu walitunga sera, falsafa kubwa ya Wachina kutunga sera lazima utunge sera ambayo inawalenga watu, ukitunga sera na haiwalengi watu umekosea. Kitu cha tatu, Wachina waliwekeza katika *sound* au propaganda. Wamepiga propaganda sana ukichanganya mambo hayo matatu mambo yanakwenda.  
(*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa Mheshimiwa Keissy. Serikali kupitia *TRA* imeanzisha utaratibu wa kufungua mizigo ya watu na kuikagua, mfumo huo ni *subjective*. Serikali imewahi kufanya hivyo miaka ya 1980, mimi niko kwenye maeneo ya bandari tangu mwaka 1984 iliwhahi kufanya hivyo. Suluhisho ni lipi Waziri wa Fedha? Nenda kanunue *scanners*, funga *scanners*, sasa hivi kuna *scanner* nyingine ni *mobile*, kwa nini pembe za ndovu zinapita Tanzania? Mozambique wamefunga *scanners*, Namibia wafunga *scanners*, Kenya wamefunga *scanner*, *scanner* kwa mizigo yote inayoingia na mizigo yote inayoondoka. Wananchi wataishiwa mashaka kama *container* linapita watu wanadhani kuna matofali ya dhahabu, linasimamishwa inaletwa *mobile scanner* wana-scan kila mtu anakuwa na amani ya moyo *fullstop*, kufungua mizigo, utafungua mizigo mingapi? Sheria ya Forodha, inasema utoe jora la nguo upime yadi kwa yadi wewe utapima makontena 100 utayaweza, *that is subjective*. Leta *scanner*, ni rahisi ukakopa *scanner* hata kama ni za shilingi bilioni 100 ukaweza kuokoa hayo mabilioni ambayo unapoteza kwa mwaka. Ushauri wangu ndio huo, nadhani kwa kufanya hivyo tutapata fedha nyingi na mnaweza kukuta fedha mtakazookoa mtaweba kupunguza tozo na ushuru mwingine kwa wananchi, pale tunapoteza fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kwenye Wizara ya Uvuvi na Maendeleo ya Mifugo. Mimi ni mvuvi na niko kwenye Mambo ya Maendeleo ya Mifugo. Tuliomba fedha ziongezwe, tumeongezewa shilingi bilioni ishirini, nashauri katika fedha zile zichukuliwe angalau shilingi bilioni tano ziwekezwe makusudi katika kilimo cha samaki. Wachina wamejifunza kilimo cha samaki Tanzania. Tuwekeze katika kilimo cha samaki ambao wananchi wakifuga samaki basi watapata kile kipato. Kilimo cha samaki kikikua wananchi watakuwa na uchumi utakua na wananchi wenyewe. Bwawa la samaki la mita 20 kwa 30 liliowekewa vinyoleo vya kuongeza *oxygen* ukiwekeza shilingi milioni kumi unapata milioni sitini katika miezi minne, hakuna biashara inalipa kama hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye shughuli ya Mheshimiwa Waziri ya kuongeza bei ya mafuta ili yaweze kupata kipato. Mwaka 2007, Serikali ililweka gharama ya mafuta *fuel levy* ili kujenga na ku-*maintain* barabara. Sh.200 ya mwaka 2007 sio Sh.200 ya leo. Naunga mkono Serikali kwa kuongeza Sh.63 kwenye *fuel levy* ili tujenge barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Ujenzi alisimama Bungeni akasema Mwijage barabara yako ya Muhutwe, Kamachumu itajengwa, jungu kuu halikosi ukoko, nakuunga mkono kusudi ujenge barabara yangu, nakuunga mkono kusudi mpate fedha ya kutosha kujenga daraja la Kishara, nakuunga mkono kusudi Wabunge wote hawa wanaotaka barabara zao zipandishwe daraja waweze kupandishiwa daraja. Ni kwa misingi hiyo tunakuunga mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi hamsini za *REA*, kimsingi mimi ningekuwa na uhuru wa kusema ningesema hizi fedha ziongezwe. *REA* kwa miaka mitatu kila wanachoahidiwa hawapewi. Busara ya Kamati ya Nishati ni kwamba *REA* sasa ipewe *fixed amount* kama tozo kusudi tuwe na uhakika kiasi gani tumemtengea *REA* na ile fedha izuiliwe iwe *ringfenced*. Naunga mkono ongezeko la shilingi hamsini kama fedha ya umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Keissy amesema sisi hatuna mjomba Ulaya, hatuna shangazi, wajomba wengine anasema watatumiza, kwa hiyo tujifunge mkanda sisi kusudi tuweze kuwekeza katika sekta hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuwa ameweka michanganuo yake hiyo katika bei za mafuta atakuja kuona kitu ambacho si cha kawaida katika soko. Atakuwa ame-*load* ushuru Sh.713 kwenye petroli na Sh.515 kwenye pampu haitapendeza. Lazimaachezee hesabu zake, apunguze kwenye petroli kusudi awasadie zaidi hawa watu wanaolalamikiwa wa bodaboda lakini upunguze kuna wafanyakazi wa Serikali,

Walimu wamenunua vile vigari vidogo vinavyotumia petroli uweze kuwasaidia hawa watu kusudi na wenyewe waweze kupata nafuu. Waziri asiwe na wasiwasi,achezee *matrix*,achezee tarakimu zake ataweza kuona kabisa atabaki na kiasi cha fedha anachokitaka cha shilingi trillioni 1.714, hamna tatizo ataweza kuzipata. Afanye *homework*, awatume vijana wake wafanye *homework* atafika pale lakini mimi naunga mkono zoezi la kujinyima, kujifunga mkanda kusudi tuweze kupata fedha za kuendeleza nchi zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mazao ya wakulima. Naishukuru Serikali imetoa tamko kwamba Sheria ya Ushirika italetwa Bungeni na iletwe, wakulima wana hali mbaya, ushirika unapashwa kuangalia upya. Nimekuwa nikipata *message* leo kwamba mkulima wa kahawa anachopata ni asilimia 30 ya bel ya soko la dunia, kilichobaki hapa ni ukiritimba wa *Tanzania Coffee Board* na Vyama vyaa Ushirika. Naomba hiyo sheria ije na inapokuja ilenge mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo la watu wa korosho, nimewahi kulisema hapa katika swalii la nyongeza. Tunapashwa Serikali tuwekeze fedha nyingi, tuokoe zao la korosho kwa kui-*brand* korosho ya Tanzania, tuache watu wa kati, twende sokoni, tumia fedha nyingi, *it will be costly*, peleka watu waende kwenye soko Marekani na Ulaya wakiitengeneza na kuiiza na kui-*brand* korosho ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru leo asubuhi Waziri wa na Biashara na Viwanda ametangaza ujio wa kiwanda kikubwa cha Kijapan kitakachokula pamba yetu. Ni matumaini yetu kwamba kitaleta na ma-*designer* wa nguo nzuri, tusingependa kuona mwekezaji anakuja kuwekeza Tanzania anatengeneza nguo ambazo sisi hatuzipendi, tumeshazoea suti nzuri nzuri. Kwa hiyo, waje watengeneze nguo hapa lakini watutengenezee nguo nzuri, wakitutengenezea nguo ambazo hazivutii na yenyewe hiyo itakuwa *counter productive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa watu wa *TRA* tena. *TRA* baada ya mabadiliko haya ya bei, mtakuwa na *exposure* ya Sh.530 kwa dizeli ukilinganisha na mafuta ya ndege. *TMMA* mnapaswa muisaidie *TRA* na *EWURA* muisaidie *TRA* ili tuweze kudhibiti kimsingi mafuta ya dizeli yanayoingia kwenye migodi. Haiwezekani jenereta iliyopangia kutumia dizeli lita 10,000 kwa mwaka ikatumia lita 100,000. Tungetaka hizo Mamlaka za Serikali ziweze kusimamiwa, ziweze kuhakikishiwa kwamba zinatumia mafuta yale ambayo wale *manufacturers, OEM (Original Equipment Manufacturers Recommendation)* waliyoyasema na lazima hizi Mamlaka ziwe *taxed*. Nashauri Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti muwaite hawa watu wa *TMMA*, muwaite hawa watu wa *TRA* muwaalize watafanya nini? Kwa sababu Sh.530 ni motisha tosha kwa mtu kuweza kufanya kitu anachotaka kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napokuja kwa Mheshimiwa *Comrade Chiligati* tuzungumze *tax culture*. Inaweza kuleta mashaka uongezaji wa kodi. Serikali inafanya vibaya au inakwenda kinyume na kanuni za uchumi kwa ku-*tax raw materials*, kwa ku-*tax* petroli, lakini iko haja sasa tutumie mbini zote...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Nilikuwa namsikia Mheshimiwa mmoja kule anasema kwa sababu ya busara za Mheshimiwa Keissy Mabodi, nikuongezee dakika 10 lakini Kanuni hairuhusu. Kwa hiyo, naomba tu tuendelee na mchangiaji anayefuata. Atafuata Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Richard Ndassa ajiandae na kama muda utaturuhusu Mheshimiwa Kilufi naye atapata nafasi ya kuchangia.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kunipa fursa hii nikaweza kuchangia katika bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia, napenda nikipongeze chama changu cha *CUF* kwa ushindi mkubwa tulioupata kule Pemba na kesho tutaingiza medali ya dhahabu Bungeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naanza na kuchangia bajeti ya Serikali. Mimi naanza na kusema kuwa fedha za bajeti ya maendeleo ni ndogo sana, ni asilimia 31. Katika hizi asilimia 31, asilimia 21 inategemewa kutoka kwa wafadhili. Hali za wafadhili wetu tunazijua zina masharti magumu. Je, pale ambapo fedha hizi hazitopatikana ina maana hakutokuwa na shughuli zozote za maendeleo katika nchi hii? Mwaka jana tuliahidiwa kupewa shilingi trillioni 1.89, lakini matokeo yake tulipata shilingi trillioni 1.23 sawa na asilimia 65. Je, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ikiwa tutakosa fedha hizi tutafanyaje? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo, nataka sasa nizungumzie vyanzo vya mapato. Siku zote Serikali inang'ang'ania na vyanzo vya mapato hivyo hivyo, hatubadilishi. Kila siku tukitaka kuongeza mapato tunaanza kusema kama tutaongeza ushuru katika vinywaji baridi, bia, soda, sigara na kadhalika. Mimi nasema hivi kila siku tutaendelea kutwanga maji kwenye kinu? Kuna sentensi moja mimi inaniudhi sana katika bajeti kila mwaka naiona wanasema kama ushuru wa *cigar* utaendelea kubakia palepale asilimia 30. Mimi nataka nikulize Mheshimiwa Waziri wa Fedha hivi ni Watanzania wangapi wanaovuta *cigar* hapa nchini? Nataka uniambie ni kiasi gani cha mapato tunachoingiza kutoka katika hizo *cigar* hata ikawa kila siku tunang'ang'ania na mambo haya? Tunaacha kuzungumzia ni kiasi gani cha mapato tunayoongeza kutoka katika sekta ya madini, tunakwenda ku-deal na *cigar*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina madini mengi sana. Mimi nataka niseme katika Mkoa unaoongoza kwa

umaskini uliokithiri ni Geita. Ukiacha Geita ni Bunda na Igunga lakini Geita kuna migodi miwili mikubwa, hivi jamani hatuwaonei huruma Watanzania wale walioko Geita? Hakuna maji, hakuna umeme, nyumba zenyewe ziko '*dhoofulihali*', hivi kweli Serikali haioni tunawaachia wawekezaji wakubwa wanakuja wakichukua dhahabu zetu wakipeleka nje, lakini Watanzania wale wabakia katika hali ya umaskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi jamani tutakwenda kusema nini kesho mbele ya Mungu? Serikali iwapatie maji safi na salama kutokana na kile kinachopatikana kule kwao. Wapatiwe barabara ingawa mambo haya mimi nasema kuwa si maendeleo wakipewa mambo haya kwa sababu ni wajibu wa Serikali kuwapatia maji safi na salama pamoja na barabara. Sijapata kusikia mkono ukipewa shukrani na mguu kwa kuutoa mwiba, huu ni wajibu wake. Pia tukiwapatia wale watu wa Geita maji safi na salama, hatuvezi kusema ni maendeleo ni sawasawa na nyumba kwenye nyumba lazima kuwe na mwiko na sufuria, ni kitu cha kawaida katika nyumba kuwemo. Sasa leo tunawaachia wawekezaji wakubwa, wale hawakuja hapa kutembea wamekuja kwa biashara, kwa nini Serikali haiwatozi ushuru? Kila siku kilio cha Watanzania ni hiki, tutaiacha nchi inateketea, twaachiwa mashimo na mpango, watu wanabakia tukiangalia, wanakwenda kutumia watu huko ulaya. Jamani tumuogopeni na '*mchana kusudi atavaa kusudi*' tutakuja kusutwa huko tunakokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi nataka niende kwenye kodi ya mishahara. Serikali imesema kuwa imewapunguzia mishahara kwa 1% yaani kutoka 14% mpaka 13% huku ni kuwadhihaki watumishi wa Serikali. Tunasema kama uchumi unakua, ni kweli unakua lakini bado chakula kiko vilevile, bei iko juu, kuna gharama za usafiri, kuna gharama za kodi ya majumba wanazo kodi, kuna gharama za maji, kuna gharama za umeme, hivi 1% hii tunayoitoa ni kweli tumewapa unafuu hawa wafanyakazi wa Serikali? Huku ni kuwadhihaki na naiomba Serikali itafute ni nmanaa gani ya kuwasaidia watumishi hawa wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatoa ushauri, naomba tuwapunguzie kwa 3%, nakisi hii tuitoe kwenye vocha za simu. Matumizi ya simu Tanzania yamekuwa makubwa na ni kwa sababu hizi vocha ni rahisi. Humu tuna watu wana miaka 65 kazi yao ni kusikiliza simu na kudanganywa na watoto wadogo wakiitwa baby. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ndoa zinavunjika kwa sababu ya simu hizi za mkononi. Watoto wetu wanafeli kutokana na kuchati kwenye simu, kila wakati wanachati na kutuma *message*. Mimi naiomba Serikali tuongeze kodi kwenye vocha za simu, 3% tupeleke kwenye mishahara ili tusaidie watu, anayetaka kuitwa *baby* basi atagharamika. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo, nataka niende kwenye sekta ya elimu. Karibu 80% ya watoto wetu wameacha kusoma masomo ya sayansi na wanasoma masomo ya *arts*, hivi kweli sisi wenye hatujaliona hili? Wataalam wengi tulionao ni kuanzia miaka 60 na kwenda juu, umri wetu ni mfupi, hatusomeshi watoto na hii yote inatokana na mwanzo mbovu wa watoto kwenye masomo ya hisabati na sayansi. Mimi naishauri Serikali ili kuondokana na hili na ili tuweke akiba vizuri, tusomeshe watoto wetu masomo ya sayansi. Naishauri Serikali kila Wilaya ittengwe shule moja ipewe vifaa vya maabara vya kutosha na Walimu wazuri tuwasomeshe watoto wetu sayansi ili tuwe na akiba ya baadaye. (*Makofii*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kengele siyo yangu niambie niendeleee.

**MWENYEKITI:** Hiyo siyo ya kwako ni ma-*baby* tu walikuwa wanakusikiliza kwa makini. (*Kicheko*)

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa tutawasomesha watoto wetu masomo ya sayansi,

tutakuwa tumejiwekea akiba ya baadaye lakini inavyoonekana Serikali hili hawajaliona. Hebu tufanyeni tathmini, tuangalie watoto wetu namna wanavyokuwa wanaacha masomo ya sayansi na kusoma masomo ya *arts.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo, naomba niseme hivi jamani Serikali haioni jinsi Wazanzibar tunavyonyanyasika katika Jamhuri hii ya Muungano? Wazanzibar sisi Wabunge tulioomo humu ndani tunashindwa kuleta magari yetu hapa kwa sababu ya kutozwa ushuru mkubwa. Mkenya anaweza kutoka na gari lake Kenya akalipa dola ishirini na akaweza kutembea na akafanya shughuli zake. Sisi tunaoambiwa kama ni Watanzania tuliojamilika, tunashindwa kuleta magari yetu hapa kutokana na ushuru ulivyo mkubwa. Sasa kila tukisema kuwa hii ni kero wenzetu hamulioni? Jamani '*mwajua kuwa ukerezwao mwisho wake huanguka*' au ndiyo nia mliyoikusudia hiyo? Mimi naishauri Serikali sana kwa nia safi kabisa kuwa kero hii tuondosheeni, tumechoka, tena tumechoka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kukaa kitako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Rukia. Kwa kweli leo misamiati yako imetuacha hoi kabisa, '*ukerezwao mwishowe huanguka*'. Waheshimiwa Wabunge, nimwite Mheshimiwa Ndassa na nadhani Mheshimiwa Kilufi anaweza kupata nafasi, Mheshimiwa Ndassa tafadhali.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii ya jioni na mimi nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitamke kuwa naiunga mkono hotuba ya Waziri wa Fedha, hotuba ya Waziri wa Mahusiano Mheshimiwa Wasira lakini niipongeze sana Kamati ya Mtemi Chenge kwa mapendekezo mazuri sana ambayo nina uhakika Serikali itayafanyia kazi vizuri. Naomba sana Serikali, kuna mapendekezo ya muda mfupi, ya muda

mrefu na ya kati. Kwa hiyo, yale ya muda mfupi Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Wasira basi mngeyachukua na kuyafanyia kazi, hivyo hivyo na mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kuhusu umeme. Nenda popote pale duniani, nenda uendako, umeme ni kila kitu. Maendeleo yoyote duniani pasipo umeme, usitegemee utapata maendeleo. Kwa hiyo, mimi naomba sana Wizara ya Fedha, pesa ambazo zimetengwa kwa ajili ya umeme, zitumike kwa kazi nyingine yoyote ile ila ziende kwenye umeme. Narudia, pesa ambazo zimepitishwa kwa ajili ya umeme, kwa maana ya ujenzi wa miundombinu na kujenga umeme vijiji kupitia mpango wa *REA*, zisitumike kwa nyingine yoyote ile ila zifanye kazi ya kujenga miundombinu ya umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niiombe Serikali kwa sababu kutakuwa na bomba la gesi, tufanye juu chini ili ndani ya miezi 18 bomba hilo liwe limekamilika. Likishakamilika, nina uhakika ghamama za umeme kwa Watanzania zitapungua sana. Tusifanye ajizi, kama tunavyopanga vitu kwa vipaumbele hivyo hivyo, naomba Serikali isisite kutekeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine ambalo nafikiri wenzetu Wizara ya Fedha na Wizara ya Mawasiliano sijui huwa kunakuwa na kigugumizi gani. Bandari ya Dar es Salaam, ule ni mgodi, ni sehemu ambayo Tanzania tunaweza kuvuna pesa nyingi kwelikweli lakini nashangaa tumeachia tu. Ukichukua nchi sita zinazopitisha mizigo yake pale Dar es Salaam kama kungekuwa na usimamizi mzuri na Waheshimiwa Wabunge kila mara tumekuwa tukisema lakini hakuna kinachofanyika. Bandari ya Dar es Salaam baada ya kwenda pale Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ambaye ninampongeza sana kwa kazi yake nzuri anayofanya mapato yaliongezeka sana lakini unajiliza hivi huko nyuma kulikuwaje? Kama mapato yaliongezeka, tatizo liliikuwa ni nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa liko sehemu mbili *TRA* na *TPA* rushwa imezidi. Niiombe Serikali na nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja wakati anafanya majumuisho, atuambie ana mikakati gani ya kuboresha bandari ya Dar es Salaam, ana mikakati gani kuzuia wizi uliopo, ana mikakati gani kuzuia upotevu wa mizigo bandari ya Dar es Salaam mizigo, pale mizigo inapotea sana na kila mtu anafahamu. Nimesema Bandari ya Dar es Salaam ni mgodi ambaao unawenza kutuingizia pesa nyingi sana hasa tukisimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni misamaha ya kodi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha bado hujaamu kuhusu suala la misamaha ya kodi.

**MBUNGE FULANI:** Wako *holiday*.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Naambiwa huku sijui mko *holiday*. Katika kitabu chako, ukurasa wa 44 unasema kuangalia upya misamaha ya kodi kwa lengo ya kuipunguza. Ukienda ukurasa wa 62, unasema aidha, Serikali inakamilisha kazi ya utafiti wa kuchambua misamaha. Hivi mnachambua mpaka lini, ni utafiti ni upi ambaao hamuuju mpaka leo? Mnatafiti, mnachambua, mnatafiti, mnachambua, hivi misamaha hii hamujui? Hivi mnataka Wabunge waseme nini ndio muelewe? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnalalamika kuhusu mapato, mapato yako pale, yanavuja pale kwa sababu ya misamaha mingi na kila Mbunge amekuwa akisema humu, tumekuwa viziwi. Naomba sana Mheshimiwa Dkt. Mgimwa, Waziri wa Fedham, ili tupunguze utegemezi ni pamoja na kupunguza mianya ya misamaha ya kodi. Tukifanya hivyo, nina uhakika tutafika mbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiomba Serikali kwa sababu kutakuwa na bomba la maji kutoka Ziwa Victoria, Waziri wa Maji tafadhalii sana, maji yanatoka Magu. Katika Kata ya Mwabomba, Kalalo, Nyambiti, Wala, Bhujingwa, bomba hilo lipite sehemu hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
(*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ndassa. Mchangiaji wetu wa mwisho nilisema atakuwa Mheshimiwa Kilufi.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Spika kwa utaratibu huu mpya wa bajeti ambao umetushirikisha vya kutosha Waheshimiwa Wabunge na michango yetu mingi imefikiriwa na ninashukuru sana kwamba kwa sasa tunaweza tukaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kinachoweza kufanyika katika Taifa lolote lile kama uchumi wake siyo mzuri. Ni uchumi tu unaoweza kutufanya Walimu wetu wapate mishahara ya kutosha, Idara zote za Serikali ziweze kufanya kazi vizuri, barabara zetu ziweze kutengenezwa vizuri, kilimo kiweze kuendeshwa vizuri. Hakuna nchi iliyoendelea kiuchumi bila kuwa na miiko. Tanzania tutacheza, tutasema sana hapa lakini kama hatujiwekei miiko ya kudhibiti hali ya uchumi katika nchi hii, hatuwezi kupata maendeleo hata kidogo. Nina uhakika hata nchi zilizoendelea zina miiko. Tanzania hatuna miiko na sijui tunaogopa kitu gani. Tuna uchumi mzuri, sisi siyo maskini nchi hii siyo masikini kama ni umasikini basi tunao wa aina nyingine siyo umasikini wa rasilimali. Rasilimali tunazo za kutosha, sasa ni jukumu letu kujuliza wapi tunakwama na wapi tunajikwaa. Tatizo hatuna miiko, watu wanafanya wanavyotaka hakuna uwoga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale bandarini, namshukuru sana Mheshimiwa Mwaijage alikuwa anasema kuna chombo kinaitwa *scanner* kinatazama kila kitu kilichopo kwenye kontena, ni kitu ambacho kingetuokolea uchumi mkubwa sana pale bandarini lakini Mheshimiwa Mwaijage amezungumza mara nyingi, ukienda kwenye *Hansard*

utakuta, nimelikuta mimi lakini ushauri huo hauchukuliwi. Kuna nini pale bandarini tunapoteza fedha nyingi? Watu wanaofanya kazi Bandari, wameishi peponi kwa muda mrefu sana na hawakutegemea kama kuna siku kutakuja mabadiliko. Tupeleke *scanner* ikachunguze makontena yale yanapoingia waone kila kitu kilichomo mle ndani ili watu wasikwepe, tunapoteza fedha nyingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye migodi yetu kuna fedha nyingi zinapotea kule. Nchi hii kama tungedhibiti uchumi, siyo maskini sisi. Kwa nini Watanzania tunawavisha umaskini sisi tuliopewa majukumu ya kusimamia uchumi wa Taifa hili? Tofauti ya mapato inajenga chuki katika jamii. Watanzania hawatatuvinilia kuona rasilimali zao hazisimamiwi vizuri, watu wanaishi kwa shida, watumishi mishahara haitoshi, Walimu wanahangaika, wafanyakazi wastaafu wanapata shida, tumethubutu hata Wanajeshi wastaafu kutowalipa vizuri, wanalamika, tunakwenda wapi na uchumi tunao? Tatizo ni kudhibiti tu. Mimi naunga mkono yejote atakayehusika na ubadhirifu wa mali ya umma anyongwe kama Mheshimiwa Keissy alivyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahakikishieni ndugu zangu, hakuna Mtanzania atakayepinga kuwa anayehujumu Taifa hili anyongwe na kufilisiwa mali zake hata tungepiga kura za maoni, wote wanetuunga mkono. Tunaogopa nini kufanya maamuzi haya makubwa ili tulinde uchumi wa nchi hii, tunachoogopa kitu gani? Kwa nini tusiweke sheria tupitishe hapa Bungeni, Wabunge wote tupo tupitishe kwamba yejote atakayejihuisha na uhujumu uchumi wa Taifa hili anyongwe na afilisiwe mali zake, tukifanya hivyo, nina uhakika tutakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapo kama Mbunge kutoka Jimbo la Mbarari, nimetumwa na Wanambarari kuangalia keki hii, wanasikiliza shilingi trilioni 18 Mbarari ni nini kitafanyika. Wanaangalia na wenyewe kuwa tumempeleka mwenzetu kule je, Mbarari tunapata kitu gani? Nawaomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, rasilimali hizi zigawanywe sawasawa. Kama tatizo la maji liko Mkoa

fulani na Mbeya na Mbarari vilevile tuna tatizo la maji. Kama kipaumbele ni maji basi na Mbarari kipaumbele hicho kiangaliwe. Kama tatizo ni barabara basi na Mbarari ziangaliwe. Katika shilingi trilioni 18 haiwezekani mimi Mbarari nikarudi sina kitu, barabara hakuna, bahati mabaya Mheshimiwa Magufuli hayupo nilimwomba barabara ya Rujewa – Madibila ni ahadi ya muda mrefu lakini utekelezaji wake ni hadithi, Wanambarari tumechoka kusikiliza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba kabarabara kadogo tu, kana sifa zote za kiuchumi ka kutoka Igawa kwenda Ubaruku kuchukua mchele unaokobolewa kwenye viwanda pale ambao unaingia Dar es Salaam kila siku na yenye naahidiwa, inajengwa nusu kilomita kwa mwaka, kilomita kumi na name itajengwa kwa miaka mingapi? Kama ni sifa uchumi upo, barabara ile kila siku mchele unapitishwa kwenda Dar es Salaam kwa nini barabara ile isijengwe? Sikubaliani na Wanambarari hawakubali kabisa. Kama ni uzalishaji tunafanya, Mbarari tunaongoza kwa *scheme* nydingi za umwagiliaji lakini barabara zake ndiyo hizo haziimariswi, kwa nini? Kuna nini? Kuna upendeleo kwenye kugawa rasilimali za Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiangalia Wizara ya Elimu, shule za msingi, shule za sekondari namna zitakavyoboreshw. Mbarari mimi sina shule nydingi sana lakini nimepewa shule tano, saba. Kuna mahali wana shule 150 wamepewa shule 100, hivi kwa nini uwiano huu wenye shule chache zisichukuliwe zote? Hata na mimi mnanipa hesabu za shule saba, shule zangu hata 30 hazifiki, kwa nini shule zote zisipewe hiyo huduma? Ili wenye shule 100 watusubirie sisi wenye chache zinazozidi ndiyo wachukue wenye. Ni upendeleo ambao haukulaliki, keki ya Taifa ni lazima tugawane sawasawa, haiwezekani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Mheshimiwa Waziri wa Elimu kama ananisikiliza, shule za Mbarari kama ataiacha hata moja mimi sitakubaliana hata kidogo. Nina shule chache, watu wamepewa shule 100, watu wamepewa shule 50, Mbarari chache zile eti nimepewa tano, sita, kwa nini?

Kama kweli tunataka kugawa uchumi wa wananchi wa Tanzania kwa usawa, kwa nini? Haiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mingi ya kilimo cha umwagiliaji, Mwenda mtitu inakwenda vizuri, ni ahadi ya Serikali, naishukuru sana Serikali kwamba ule mradi unakwenda vizuri na nina uhakika utakamilika. Tuna ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, naishukuru Serikali unakwenda vizuri, naomba jitihada hizo ziendelee. Tuna mradi wa kujenga bwawa kubwa Madibila pale ambalo litamwagilia hekta 3,600 Mheshimiwa Rais aliahidi, nashukuru sana na jitihada nimeona zinaendelea na mahali pengine pengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tatizo la umeme katika Wilaya ya Mbarari. Katika Kata 20 ni Kata nne tu zimepitawi na umeme hivi mnataka kusema Mbarari ni wapi?

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. MODESTUS D.KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Miongozo tena.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo tu naomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68 (7) na ninaomba niseme yale yaliyonisukuma kuomba Mwongozo huu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, akitoa maelezo yake hapa wakati akichangia, alieleza masikitiko yake na akasema anakosa imani na nguvu ya kuweza kuchangia ambapo kuna baadhi ya Watanzania wenzetu ambao wanaendelea kunyanyasika, kupigwa na kuumizwa. Hili ni jambo kubwa,

halistahamiliki, linahitaji kupatiwa ufumbuzi wa kudumu na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Clara Mwatuka wakati akiendelea na mazungumzo yake alieleza waziwazi kuwa tatizo hili linasukuma hata Wanajeshi kuingia katika nyumba za watu. Je, Serikali katika hili, kwa nini linaachiwa linaendelea hivi na Watanzania wanaendelea kuumizwa na hawa ni wananchi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako juu ya tatizo hili ambalo linaendelea kutokea huko Mtwara, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. Kesho ni Alhamis ...

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(7). Kesho ni Alhamis, sisi Wabunge tuna fursa ya kumuuliza Waziri Mkuu maswali moja kwa moja lakini hii ni wiki ya tatu hatujapata nafasi hiyo, tunaomba ufanuzi kama kesho tutapata nafasi hiyo?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona muda umebaki kidogo lakini nitajibu hiyo miongozo ya Wabunge.

Mheshimiwa Kombo, kesho ni Alhamis na ni kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu, kwa taarifa ambazo zilikuwa rasmi kabisa ndani ya Bunge Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa safarini na si taarifa tu ndani ya Bunge na sisi wote tumekuwa tukimshuhudia akifanya kazi mbalimbali kuititia kwenye vyombo vya habari. Kwa hiyo, kwa taarifa hii naomba niarifu Ofisi ya Katibu wa Bunge, wataendelea kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kama atakuwa yupo kwa ajili ya maswali kesho asubuhi, utaratibu wa shughuli za Bunge Wabunge wote tunaupata kuititia muundo mpya wa

utendaji kazi wa Bunge kwenye simu zetu huwa tunapewa ajenda za shughuli za Bunge za siku inayofuata. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa amerudi, ratiba hiyo tutaipata na tutapewa taarifa rasmi na niwaombe Makatibu wangu mnaonisaidia kuniongoza hapa mbele leo, hilo suala pia milipatie ufafanuzi ili Waheshimiwa Wabunge wajue kama wanatakiwa kuja mapema kwa ajili ya shughuli hiyo ama viyi.

Mheshimiwa Masoud umezungumzia suala la hotuba ya Mhesmiwa Clara, naomba nimwombe Mheshimiwa Clara awasilliane na Waziri husika, amweleze kile ambacho alikuwa anakizungumza kwa sababu hata hivyo katika kuchangia hotuba hii, nimechukua tu nafasi yangu kama Kiti kumvumilia kwa sababu ajenda aliyokuwa anazungumza kwa mujibu wa Kanuni ilikuwa siyo ajenda ambayo iko Mezani. Kwa hiyo, kwa nafasi yake angeweza kutumia Kanuni nyingine na akalizungumza suala hilo lakini kwa uzito wa jinsi alivyosema, namwomba sana Mheshimiwa Clara awasilliane na Waziri husika, nadhani anaweza kupata maelezo mazuri na ya kina na ninaamini kwa jinsi ninavyomjua Waziri husika atapata nafasi ya kumsikiliza vizuri na atawea kupata suluhu ya nini kinachofanyika na anaweza akasaidia kujua nini cha kufanya.

Mwongozo mwingine ambao nilikuwa nimeombwa hapa ndani niliombwa na Mheshimiwa Keissy na Mheshimiwa Keissy alitaka kujua kwa nini hawa Waheshimiwa Wabunge wanapochangia hawazungumzia kutoa na wao ushauri kwa Serikali ni namna gani Serikali ifanye ili kuweza kuongeza mapato badala yake wanachangia tu na ndipo hapo alipokuwa anashauri hata yeye kuwa mpaka kuku wanawea kutozwa kodi ili kuongeza uchumi na pato la Taifa.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 106 inasimamia mjadala kuhusu hotuba ya bajeti na nitasoma Kanuni ya 106 (1) ambayo inasema:-

*"Mjadala kuhusu hotuba ya bajeti ya Serikali utaendelea kwa siku zisizozidi saba ambapo dakika zisizozidi*

*kumi zitatolewa kwa kila Mbunge anayetaka kuchangia hotuba hiyo".* Hiyo tunakwenda nayo hivyo.

Kanuni ya 106(2) inasema:-

*"Katika hatua hii, majadiliano yatahusu mambo ya jumla kuhusiana na hali ya uchumi..."*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanachokifanya hapa ni kuzingatia ile Kanuni, kuzungumza mambo ya jumla kuhusiana na hali ya uchumi lakini hata hivyo ushauri pia na busara alizozitoa Mheshimiwa Keissy nazo zina manufaa. Tunapozungumza hali ya jumla ya uchumi wetu, ni vizuri sana Waheshiumiwa Wabunge kama pia tutajikita kuishauri Serikali, nini kifanyike ili kuongeza mapato, kubana matumizi na kujenga uchumi imara wa nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, hayo pia ni mawazo yenye busara tu ambayo nadhani tukiyafuata pia yana nafasi nzuri ya kuweza kujenga na kuisaidia Serikali yetu.

Niendelee kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, Wabunge wanapochangia wanazingatia Kanuni nilioisoma na Kanuni hiyo inasema ni lazima kuzungumzia mambo ya jumla yanayohusiana na hali ya uchumi wa nchi yetu. Baadaye tutakapokuja kwenye kuhitimisha, Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja au watoa hoja, watayatizama mambo haya yote na kuona namna gani tunaweza kufanya ili kuboresha uchumi wa nchi hii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, naomba niwashukuru kwa siku hii ya leo, naahirisha shughili hizi za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya ukumb huu wa Bunge.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 20 Juni, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*